ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/\Jimbo la Jang'ombe
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando

20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake

41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 23 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhamed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba kuweka hati mezani kuhusu Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 80

Elimu ya Utabiri wa Hali ya Hewa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Kwa kuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini inafanyakazi juu ya hali ya hewa na kwa kuwa wavuvi wengi na wenye vyombo vya kupakia abiria wanapaswa wafahamishwe juu ya hali ya hewa ilivyo.

a) Je, serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba watu hao wanaelimishwa.

b) Je, ni sababu gani za msingi zinazoipelekea Mamlaka ya Hali ya Hewa ishindwe kuandaa taarifa ya utabiri wa miezi mitatu mbele.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba radhi kidogo sauti yangu haipo vizuri sana, ndio tunakaribisha Ramadhani visomo na visimamo vinakuwa virefu.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa kama wakala wa serikali ina wajibu wa kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mamlaka ya Hali ya Hewa inaendeela kutoa utabiri wa kila siku kwa muda kipindi cha siku tano, kwa muda wa kipindi cha siku kumi, kwa muda wa kipindi cha mwezi mmoja na kwa kipindi cha miezi mitatu. Unaosaidia utekelezaji wa shughuli mbali mbali za kiuchumi na kijamii kama vile uvuvi, kilimo na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa ina jukumu la kutoa tahadhari ya majanga yanayosababishwa na hali ya hewa mbaya katika maeneo mbali mbali nchini kwa ajili ya usalama na maisha pamoja na mali zao. Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:

a) Tunakubaliana na suala Mhe. Mjumbe, kuwa elimu ya hali ya hewa ni muhimu sana kutolewa kwa wananchi wote ikiwa ni pamoja na watumiaji wa bahari kwa ajili ya usalama wa maisha ya watu na mali zao.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa inatoa utabiti na taarifa za hali ya hewa ikiwa pamoja na kiasi cha upepo na mweleko wake nchi kavu na bahari. Hali ya bahari kwa maana ya ukubwa wa mawimbi, kiasi cha mvua na kadhalika. Baada ya kupima, kukusanya na kuchambua taarifa za hali ya hewa kutoka vituo viliopo ukanda wa pwani ya bahari ya Hindi ili kujumuisha visiwa vya Unguja na Pemb. Viashiria vinavyoonesha kuna

uwezekano wa kutokea kwa upepo mkali, ama mawimbi makubwa na mvua kubwa, Mamlaka hutoa tahadhari hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutoa elimu kwa wasambazaji na watumiaji wa taarifa za hali hewa hapa nchini. Ofisi zote za hali ya hewa ziliopo katika pwani ya bahari ya Hindi ikiwa pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba vimekuwa wazi kwa muda wote kupokea masuala ya watumiaji wa bahari na kuyapatia majibu. Ofisi ya Hali ya Hewa iliopo Bandari, hapa imeendelea kutumia vyombo vya baharini na kutoe elimu kwa wote wanaotembelea Ofisi hiyo. Aidha, wakati wa Sikukuu za hali ya hewa duniani, yaani tarehe 23 Machi ya kila mwaka Mamlaka ya Hali ya Hewa inakaribisha wananchi wote, ikiwa na pamoja watumiaji wa bahari kutembelea Ofisi za Mamlaka na kupata elimu ya umuhimu wa huduma za hali hewa.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeandaa mkakati wa kufanya warsha na watumiaji wa taarifa za hali hewa katika bahati na maziwa makuu ambazo zinatarajirwa kufanyika katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015. Mkakati huo unalenga kuwakutanisha watoa huduma na watumiani wa huduma za hali ya hewa ili kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinatumika katika mipango ya maendeleo na hiyo kuleta tija na ustawi wa jamii. Katika mkakati huo, mamlaka imekusudia kuandaa warsha, kuendesha vipindi maalum kwenye vyombo vya habari ili kutoa elimu kwa watumiaji wote wa hali ya hewa ikiwa pamoja na watumiaji wa bahari.

b) Mhe. Mwenyekiti, napenda kuhakikisha kuwa taarifa za hali ya hewa ni za muda mrefu, ni muhimu kwa mipango ya maendeleo. Taarifa hizo hapa nchini zimeendelea kuwa bora zaidi kutokana na kuongezeka kwa vifaa vya upimaji na uchambuzi wa hali ya hewa. Pia, kuongezeka kwa wataalamu wenye taaluma ya hali ya hewa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ofisi za Hali ya Hewa Zanzibar ina wataalamu 21 ambao wanatosha kuhakikisha taarifa za hali ya hewa zinatolewa kwa muda muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa imekuwa ikiandaa na kutoa taarifa za hali hewa za msimu, yaani miezi mitatu. Taarifa hizi zimekuwa zikisambazwa katika taasisi mbali mbali ili kuzisaidia taasisi hizo katika kupanga mipango yao mbali mbali ya kimaendeleo. Aidha, taarifa hizi zimekuwa zikitolewa katika vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na tovuti ya mamlaka ili wananchi na watumiaji wa bahari wazipate kwa wakati. Sambamba na taarifa hizi, Mamlaka ya Hali ya Hewa imekuwa ikitoa taarifa mahususi za hali ya hewa za muda mfupi na muda wa kati kwa watumiaji mbali mbali ikiwemo wavuvi, wasafirishaji, wahandisi na kadhalika. Taarifa hizi za muda mfupi na muda wa kati zinatolewa kwa watumiaji wa baharini ni za uhakika zaidi na ndizo zinazofaa katika shughuli zao za kila siku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza maswali mawili madogo sana ya nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kutoa taarifa ni kazi ya kwanza na kusimamia utekelezaji wa taarifa ni kazi ya pili. Ni chombo gani chenye mamlaka na wajibu wa kusimamia taarifa ya hali ya hewa, hatari inapotokea hali ya hewa inapobadilika. Hilo ni swali la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, la pili, wavuvi na wakulima wangapi wameshanufaika na mafunzo ya kuzingatia taarifa za mabadiliko ya hali ya hewa hasa wakulima kwa kuzingatia, wengi wao hupata muda wa kusikiliza matangazo, ni mdogo na wengine wakiishi katika nyumba hata umeme wakiwa hawana na kukaribia kutumia televisheni za mafuta ya taa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, suala la maswali ya Mhe. Mjumbe, swali mama alikuwa anaulizia masuala ya hali hewa na swali lake la kwanza amesema kwamba kutoa taaluma ni jambo moja, kusimamia ni jambo la pili.

a) Ninakubaliana naye na wajibu wa *TMA* wanatoa taarifa na taaluma kujuulisha umma juu ya athari ya hali ya hewa kwa muda wa masaa, siku, siku tano, wiki, mwezi na miezi mitatu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa wanapotoa taarifa, kwa mfano kwamba kesho bahari itakuwa na hali mbaya, mawimbi yatakuwa na urefu zaidi ya mita, kwa maana ya kwamba usafiri hautokuwa mzuri. Ni wajibu wa *ZMA* sasa kwenda kusimamia kwamba kwa kesho musifanye safari. Kama utabiri wa hali ya hewa utakuwa umeonesha kwamba kesho kutanyesha mvua kubwa katika maeneo ya mashamba, maana yake ni wajibu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili kuwaelekeza wakulima kuweza kuutumia neema hiyo ya mvua. Kwa hivyo, *TMA* wao wanachukua ni kutoa taarifa. Kila taasisi inayohisi kwa namna moja au nyengine inahusika na taarifa ile, wao watapaswa kusimamia.

b) Swali jengine ameuliza kwamba ni wananchi wangapi wavuvi na wakulima ambao wamenufaika na taarifa za *TMA*. Mimi nadhani jambo la msingi la *TMA* sio mtu kunufaika. Wao wanachokitoa ni taarifa ili sasa mtumiaji aweze kutumia vizuri taarifa zile kuweza kufanya harakati zake za kimaendeleo, kwa mfano kama *TMA* watasema kama kipindi kinachokuja mbele, kitakuwa kina mvua kubwa sana kiasi hata kama utalima utaathirika. Kwa hivyo, msingi ni mkulima kuweza kujikinga na mvua zile. Kama kuna upepo ni hivyo hivyo, wasafiri wanapaswa kuwa na tahadhari na kama kutakuwa na suala jengine la bahari kuchafuka, maana yake na mvuvi na yeye aweze kutahadhari.*Visa vie* kama kutakuwa na shwari nzuri, maana yake mvuvi ajipange kwenda kutumia fursa hiyo ya shwari. Kwa hivyo, kusema ni watu wangapi wamenufaika, mimi siwezi kusema, sina takwimu hizo.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, anasema hana takwimu. Mimi nitampa muda aniletee kwa maandishi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, siwezi kuleta kwa maandishi. Kinachozungumzwa hapa ni taarifa za hali hewa. Kuja kueleza hapa ni watu wangapi wamenufaika na hali hewa hakuna jambo hilo, maana yake tukarande nchi nzima, tukatafute kila mtu wewe umenufaika na jua, wewe umenufaika na mvua, hakuna kitu hicho.Msingi wake ni kufuata taarifa zile ili kujikinga na kuongoza shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kusema kuwa nimletee kwa maandishi ni kitu gani. Siwezi kuleta taarifa hizo kwa maandishi. Kinachozungumzwa hapa ni hali ya hewa. Watu wangapi wamenufaika na hali ya hewa, huwezi kuleta hapa kwamba watu kumi wamenufaika na taarifa za hali ya hewa.

Mhe. Mwenyekiti, tumesema kwamba taarifa ya hali hewa kwa upande wa usafiri wa baharini *ZMA*, wanachukua tahadhari baada ya kupata taarifa. Hali ya Hewa kituo chao kipo *Airport*, kipo kituo bandarini, kipo kituo Chuo cha Kilimo. Kwa hivyo, tukawatafute wakulima wote walioambiwa kwamba keshokutwa kunakuja mvua limeni uzuri, tuwahakiki. Hatuwezi kufanya jambo hilo. Kwa hivyo, kama ana swali aelekeze hasa swali lake anakusudia kitu gani. Vyenginevyo, tutakuwa hatumuelewi.

Mhe. Mbarou Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi na mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri, swali la nyongeza. Kwa kuwa mawasiliano ya kujua taarifa za hali ya hewa ni muhimu na hasa kwa wavuvi wetu. Kama ujuavyo kwamba wavuvi wetu wadogo wadogo kule, vifaa vya mawasiliano huwa ni tatizo.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wavuvi wetu wale wadogo wadogo kuwapatia vifaa vya mawasiliano ili kupata taarifa za hali ya hewa pindi zinapobadilika wakiwa baharini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wananchi wetu ni wanyonge, hawana uwezo wa kuwa na vifaa vya kisasa vya kuweza kupata taarifa hizi za hali ya hewa. Sasa kwa kuzingatia msingi huo, serikali ina utaratibu, taarifa hizo za hali ya hewa kila siku ya Mungu, kila baada ya taarifa ya habari kwenye televisheni, magazeti na redio zinaelezwa. Kwa msingi kwa wavuvi wetu hawa wajenge desturi ya kusikiliza vyombo vya habari ili waweze kupata taarifa hizi sahihi. Kwa sababu kutokuwa kwake na chombo hichi cha kisasa, hakumaanishi kwamba yeye atashindwa kusikiliza redio ambayo itaweza kumsaidia kupata taarifa hizo.

Mhe. Mwenyekiti, sisi serikali tunachokifanya ni kuweza ku-*co-ordinate* baina ya *TMA* na taasisi zetu, kwa *Airport* watu wanaongoza ndege pamoja na *ZMA*, pamoja na watu wa kilimo ili kuweza kupanga mipango ya miongo mikubwa, kwa mfano wa watu wa kilimo kwa kipindi cha miezi mitatu, kuweza kujua kwamba kwa kipindi hichi taarifa ambazo zinazotoka *TMA*, zitaweza kutuongoza kiasi gani katika ukulima. Kwa hivyo, kuhusu suala la wavuvi kuweza kuwapatia vyombo maalum, kimsingi ninaweza kusema kuwa wajenge utamaduni wa kusikiliza vyombo vya habari, taarifa hizi watazipata.

UTARATIBU

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Mwenyekiti, nakusudia pale wavuvi wetu wapo baharini, sio suala kwamba wapo juu, wanapokuwa baharini, labda hali ya hewa huku imetokezea kwamba inabadilika, ndio

nilikuwa ninataka kujua serikali ina mpango gani wa kuwasaidia ili kuweza kupata taarifa wakiwa kule baharini waweze kurudi, kwa sababu wanakuwa masafa makubwa kidogo kutoka huku usawa wa ardhi tuliopo.

Sasa wanapokuwa kule, yaani nilikuwa nataka kujua serikali ina mpango gani wa kuweza kusaidia kupata taarifa wakiwa kule na sio huku juu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi hili swali nimelielewa vizuri na ndio nikajibu vile. Kwa sababu ukizungumza kwamba mvuvi yupo baharini, umpe chombo akiwa bahari, maana yake hicho chombo ni cha kisasa. Tunachokisema ni kwamba *TMA* wanatoa tahadhari kwamba leo bahari itakuwa na mawimbi ukubwa huu, maana mvuvi unakwenda tayari una taarifa, lakini ukisema kwamba tuweke vyombo vya *emergency*, maana yake hicho chombo ni lazima kiwe na vifaa vya kisasa kama zilivyo ndege, kama zilivyo meli za abiria.

Mhe. Mwenyekiti, maana yake linapotokea tokea popote, lazima hicho kiweze kuripoti. Sasa kwa kipindi hichi serikali hatuna hilo jambo, ndio maana nikasema kwamba kabla ya kuondoka kwake mtu awe na taarifa zile za ziada ambazo amezipata kwa vyombo vya habari, lakini kusema kwamba kila chombo kinakwenda kuvua tufunge vifaa vya kisasa, hilo jambo halipo serikalini, kwa sababu suala la vifaa ni suala la kibiashara. Kina chombo kinachotumika kitakuwa kina uwezo wa kuwa na vile vifaa, kama vile vyombo vya usafiri, hicho ndicho nilichokieleza.

Mhe. Mwenyekiti, sio kwamba sijamfahamu, suala lako unaposema kwamba mvuvi anapokwenda, anapotoka Mkwajuni au anapotoka Mkokotoni,ameshapita Mwanawamwana, anakaribia Tanga Kitumbwi, akipata athari za hali ya hewa, sisi hatuna uwezo wa kumpa taarifa. Isipokuwa yeye anapoondoka pale kwake bandarini, ni lazima awe na taarifa za hali ya hewa, kwamba leo bahari inategemewa itakuwa shwari au itakuwa na mawimbi. Kwa hivyo, anapokwenda kuvua anajua, nina tahadhari kwamba leo bahari haipo vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, namshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kufika hapa tukiwa na afya na wazima. Pili, nampa Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pole kwa kubanwa na kifua na Mwenyezi Mungu atampa shufaa *Inshaallah.*

Mhe. Mwenyekiti, tatu mimi nilikuwa na swali moja la nyongeza, kwa sababu swali mama ni Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania na mamlaka hii ni ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inafanya kazi kama mamlaka nyengine zilizokuwa chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa mimi swali langu la kwanza nilikuwa ninauliza kikawaida hizi mamlaka zilizokuwa chini ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania huwa zinakuwa na Mjumbe mmoja au wawili wa Bodi kutoka Zanzibar. Je, mamlaka hii ina Mjumbe wa Bodi kutoka Zanzibar. Kama yupo jina lake ni nani.

Mhe. Mwenyekiti, pili, mara nyingi mamlaka kama hizi zinatakiwa kuwa karibu na wananchi zaidi. Kwa kule Dar-es-salaam Ofisi yao ipo *Ubungo Plaza* na wana *information centre* ambayo huwa wanatoa taarifa mbali mbali kwa wananchi kuhusu hali ya hewa na mambo kama hayo. Kwa hapa Zanzibar hawa wapo ndani ya *high security zone*, yaani kwenye eneo la *Airport*. Je, Mhe. Naibu Waziri, naomba kumuuliza kwamba anaweza kuwa na sehemu nyengine yoyote au ana sehemu nyengine yoyote ambayo wanawafikia wananchi kutoa taarifa hizo pamoja na wavuvi. Kwa sababu sidhani kama wavuvi wanaweza kupita kwenye ma-*fence* yale ya pale kwenye *Airport*. Kwa hivyo, je, wana *information centre* nyengine yoyote ambayo wanawafikia wavuvi moja kwa moja, kwa sababu alisema mambo ya *website* na nini, sijui kama wavuvi wana-*access* hizo *website.*

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba mamlaka ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (*TMA*) ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inapaswa kwa mujibu wa sheria kuwa na Bodi ya kuweza kuisimamia. Bodi hiyo *components* yale ni lazima iwe na watu wanaotoka pande zote mbili za Muungano na ndivyo ilivyo kwa bodi hii. Suala la majina ya Wazanzibari, naomba tu Mhe. Mwakilishi anipe muda, ikiwezekana hata kesho nimpatie kwa maandishi taarifa hii ya Wajumbe wa bodi.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili, aliuliza kuwa vituo vya *TMA* kwamba vipo katika sehemu yenye ulinzi mzuri, kwa maana katika *High Security Zone Airport*. Ni kweli kwamba *TMA* ina vituo vitano hapa Zanzibar. Kituo

kimoja kipo *Airport,* kituo cha pili kipo bandarini, kituo cha tatu kipo Kizimbani Chuo cha Kilimo. Kwa Pemba kituo kimoja kipo Matangatuani kwenye Chuo cha Kilimo na kimoja kipo *Airport.*

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, naamini kwamba bado wananchi wana nafasi ya kutosha ya kwenda kuuliza na kupewa taarifa hizo pasi na ulazima wa mamlaka hii kujenga Ofisi nyengine katika maeneo ya wazi, kwa sababu malengo makubwa ni kutoa taarifa na ziweze kuwafikia wananchi waliolengwa, lakini kwa maumbile na taarifa hivyo zinavyopatikana tunaamini kwamba nafasi za Ofisi hizi zinakidhi. Atakayekwenda bandarini atapata taarifa, tunaotoka vijijini tunaweza kutumia Chuo cha Kilimo cha Kizimbani kwa taarifa, halikadhalika na kwa upande wa Pemba watakaokwenda katika maeneo ya Chuo cha Kilimo Matangatuani, basi watapata taarifa nzuri na sahihi zinazohusiana na hali ya hewa.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wao sio kwamba kile kituo kilichopo Chuo cha Kilimo, kitakuwa kina-*compose* kwa ajili ya vipindi virefu, lakini hata taarifa za kila saa utaweza kuzipata kama kilivyo kituo cha *Airport* na kama kilivyo kituo cha bandarini. Kwa hivyo, tunaamini kwamba vituo vyetu hivi mwananchi anayehitaji taarifa za hali ya hewa atazipata na zitamridhisha.

Nam. 89

Meli ya Jitihada Kupakia Abiria

Mhe. Jaku Hashima Ayoub: (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) - Aliuliza:-

Mhe.Mwenyekiti, ahsante sana kwa niaba ya Mhe. Saleh Nassor Juma (Mwakilishi wa Jimbo la Wawi). Naomba swali lake nambari 89, lipate jawabu na Mhe. Naibu Waziri, nimsisitize sana akijibu swali hilo aangalie Katiba ya Zanzibar, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wana haki bila ya ubaguzi wowote, kulinda na kupata haki mbele ya sheria. Naomba jawabu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba hivi karibuni meli ya *LCT* Jitihada ilipakia abiria wasiopungua 500 kuelekea Kisiwani Tumbatu, katika Sherehe za Maulid. Katika Baraza hili Mhe. Waziri, dhamana alipinga vikali meli zisizokuwa za abiria kupakia abiria.

(a) Je, meli ya Jitihada tangu asili yake iliundwa kupakia abiria.

(b) Je, kauli ile ya Mhe. Waziri si sawa na kugeuka maneno yake kwa kutosimamia utekelezaji.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, swali lake nambari 89 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Mwenyekiti, suala la usafiri wa baharini kwa hapa kwetu Zanzibar ni jambo linalohitaji taadhani na busara kubwa ili kuweza kufanikisha kazi hiyo kwa usalama na ufanisi unaohitajiwa. Kwa kawaida kwa mujibu wa sheria nambari 6 ya mwaka 2005 ya usalama na usafiri baharini imeainisha vyombo maalum vya kuweza kutumika kwa ajili ya matumizi ya kibiashara, hasa kwa madhumuni ya kubeba abiria. Kwa msingi huo huo, usalama wa abiria huo umepewa kipaumbele maalum katika fursa na usimamizi wake ili kuona unaimarishwa. Kwa bahati nzuri sana nchi yetu imebarikiwa kuwa na visiwa vidogo vidogo ambavyo pia ni sehemu ya Zanzibar. Wananchi wanaoishi katika maeneo hayo, wote wana haki na fursa sawa na wananchi wengine wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hadi muda huu njia pekee inayotumika kuwaunganisha wananchi hao na visiwa vikuu vya Unguja na Pemba, ni kwa njia ya usafiri wa baharini, ingwa vyombo vinavyotumika ni vile vile vya asili, yaani mashua, mitumbwi na ngalawa.

Mhe. Mwenyekiti, tunatambua ukizungumzia kupeleka mali, maana yake unazungumzia uwekezaji mkubwa sana, pamoja na miundombinu yake, yaani bandari. Kutokana na mahitaji maalum na kwa siku maalum, serikali hulazimika kuruhusu meli ya *LCT*, ambazo hazilazimiki kufunga katika geti maalum kwa ajili ya matumizi ya msaada maalum unaoombwa katika maeneo hayo. Hali hiyo inatokana na mrundikano ama mahitaji maalum ya wananchi katika matukio maalum. Majibu.

(a) Mhe. Mwenyekiti, meli ya *LCT* Jitihada tokea asili yake ni meli ya kupakia mizigo na sio meli ya kupakia abiria.

(b) Kauli ya Mhe. Waziri na kauli ya serikali kwa jumla ziko sahihi, kwamba meli zote zilizoundwa kwa ajili ya kupakia mizigo tu, hazitoruhusiwa kupakia abiria. Sababu ya *LCT* Jitihada kuruhusiwa kupakia wananchi kwenda Tumbatu ni mazingira maalum na kwa siku maalum.

Mhe. Mwenyekiti, ikumbukwe kwamba kila siku ya Mwenyezi Mungu wananchi wa Tumbatu wanavuka kuja Mkokotoni na kutoka Mkokotoni kwenda Tumbatu, bila ya *MV*. Jitihada kufanya kazi hii. Kwa hivyo, siku ambayo *MV*. Jitihada ilikwenda Tumbatu kupeleka wananchi iliombwa itowe msaada ule kutokana na wingi wa watu, pamoja na baadhi ya vifaa ambavyo vilipaswa kusafirishwa. Aidha, tunaamini kuwa kupeleka kwetu *MV*. Jitihada kwa siku ile ilikuwa ni sehemu ya kuimarisha usalama na sio kinyume chake.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu ya rafiki yangu Mhe. Naibu Waziri ya kusikitisha na ya kutokuwa na afya na yeye mwenyewe alikuwa akipiga kelele humu ndani ya chombo hiki, kwa muda mrefu na vile vile, kwa niaba ya Mhe Saleh Nassor Juma, naomba nimuulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, katika msingi wa utawala bora, watu wote ni sawa mbele ya sheria, kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kwa nini meli nyengine zizuiwe na nyengine zibebe abiria.

Mhe. Mwenyekiti, pili, Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri, mtakuwa tayari kujiudhulu kutokana na majibu yenu hayafahamiki ndani ya chombo hiki?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi namsikiliza yeye. Kwa hivyo, asiwe na papara aseme taratibu. Mimi nafahamu vizuri anayokusudia kuyasema.

Mhe. Mwenyekiti: Mjumbe rejea taratibu ili Mhe. Naibu Waziri, aweze kukufahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi ningemuomba vile vile, jawabu atakalonipa anipe kidogo kidogo ili nipate kufahamu.

Mhe. Mwenyekiti, katika msingi wa utawala bora, watu wote ni sawa mbele ya sheria kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, kwa nini meli nyengine zinazuiwa kubeba abiria hasa *landgraft,* lakini *LCT* Jitihada haina sifa ya kubeba abiria, alipokuwa akijibu swali hilo alikiri na kwa nini kapakia na chombo hiki kilipiga marufuku. Imekuwa hiki chombo kinapotosha watu.

Je, Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri, mko tayari kujiuzulu kutokana na kauli mnazotoa tofauti katika chombo hiki. Leo mnasema vyengine na kesho mtasema vyengine na mlipitisha sheria katika chombo hiki na wananchi wanatusikiliza kwa kupitia chombo hiki au “mkuki kwa nguruwe tu kwa binadamu unauma”.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, lakini uliyouliza swali la nyongeza, Mhe. Naibu Waziri, alipokuwa akijibu hoja alijaribu kutoa ufafanuzi na akaelekeza kwamba sheria nambari 6, inaelekeza kama hivi ambavyo wewe unataka kutuelekeza, lakini suala lile la *LCT* Jitihada alizungumzia kwamba ni kwa sababu ya kulinda usalama maalum kwa siku maalum. Kwa hivyo, haikuwa na hoja kwamba kulikuwa kuna suala la abiria ambayo inaweza kwenda sambamba na hoja yako. Pamoja na yote wacha tuendelee kumsikiliza Mhe. Naibu Waziri, ili atusaidie zaidi Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba Zanzibar ni nchi yenye amani na ni nchi ya demokrasia, inayoongozwa kwa msingi wa utawala bora na hakuna nchi au taasisi iliyo juu ya sheria. Sote tunatawaliwa kwa mujibu wa Katiba ya mwaka 1984. Kwa hivyo, hakuna taasisi yoyote ambayo iko juu ya sheria kwa mujibu wa Katiba hiyo. Naomba nimtowe hofu Mhe. Jaku Hashim Ayoub, kwamba anapouliza swali, akijenga utamaduni wa kusikiliza majibu hatopata tabu lakini anapouliza swali akijenga utaratibu wa kuja na majibu, basi atakuwa anapata tabu, maana atashindwa kutufahamu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tulichokieleza tumeeleza wazi kabisa kwamba sheria nambari 6 ya mwaka 2005 imeeleza, ipi sifa ya chombo cha baharini kuweza kubeba abiria, ni meli zipi zinaruhusiwa kubeba abiria na meli zipi haziruhusiwi kubeba abiria.

Mhe. Mwenyekiti, tulieleza hapa kwamba *MV*. Jitihada ilikwenda kubeba wananchi kwa mahitaji maalum na kwa siku maaalum. Siku ya Maulid ya Tumbatu mrundikano wa watu uliokuwepo, halafu ukiwaruhusu kwamba watu waruke na mashua, maana yake mashua hiyo iende zaidi ya mara 10, inategemea upepo na siku zote za Maulid ya Tumbatu, ni siku ambazo kunavuma upepo, mkusanyiko wa watu unakuwa mkubwa. Maji ya kichwa, maana yake wale watu watashindwa kwenda upande wa pili, ndio maana serikali ikawa inaandaa utaratibu maalum kwa siku ile.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, tulisema kwenye majibu kwamba zaidi ya siku ile watu wa Tumbatu kila siku ya Mwenyezi Mungu wanavuka, kutoka Tumbatu kuja Mkokotoni, kutoka Mkokotoni kwenda Tumbatu, lakini *MV*. Jitihada haiendi kwa sababu ule mrundikano ambao ulipelekea kupelekwa meli haupo. Kwa hivyo, tunapoiruhusu *MV*. Jitihada kwenda kuwachukua wale wananchi, haturuhusu *MV*. Jitihada kupakia abiria.

Mhe. Mwenyekiti, au kama atakuwa na ushahidi kwamba *MV*. Jitihada imeondoka Unguja imepakia abiria wa kwenda Pemba, *MV*. Jitihada imeondoka Unguja imechukua abiria kwenda Dar-es-salaam hilo ni kosa, lakini sisi kama ni serikali tutakapoona pahala popote pale kama panahitajika msaada maalum wa serikali ni lazima tufanye na ndivyo ilivyo kwa kwenda Tumbatu siku ya Maulid tulifanya hivyo, tulipokuwa na uandikishaji wa vitambulisho vya Mtanzania siku ya *NIDA*, tulifanya hivyo, ni kwa sababu ya mahitaji maalum. Mitambo ambayo ilibebwa na watu wa *NIDA*, ukitia kwenye mashua ikiroa, maana yake tumekula hasara sisi wenye serikali na wananchi huduma yao wataikosa.

Mhe. Mwenyekiti, mrundikano wa siku ya Maulidi ya watu wanaokwenda Tumbatu ni zaidi ya watu 4,000. Watu 4,000 ukiwachukua kwa ngalawa, maana yake *trip* ngapi za ngalawa, usalama haupo, ndio maana tukaruhusu chombo kile kwa siku maalum kubeba abiria. Kwa hivyo, mimi siamini kama kuwapakia watu kutoka Tumbatu kuja Mkokotoni na kuwapakia watu kutoka Mkokotoni tutakuwa tumekiuka Katiba, kwa msingi tu wa kuimarisha usalama wa watu wale kwa siku ile kuweza kwenda kushiriki katika shughuli za Maulid.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kama unataka tubaki sawa kwa msingi wa Kikatiba. Mimi naamini tuko sawa, hakuna aliye juu ya Katiba, hakuna aliye juu ya sheria, lakini ukiwa una ufahamu wako maalum kichwani aah! hiyo itakupa tabu, maana yake ili uendeshe taasisi vizuri, ni lazima kila jambo uangalie na mazingira yake. Mazingira yaliyoruhusiwa *MV*. Jitihada haikupakia abiria kibiashara, ilipakia watu kwa ajili ya kwenda kuwavusha kwenda kwenye shughuli maalum na siku maalum.

(b) Mhe. Mwenyekiti, mimi niko tayari kama itakuwa kauli zetu zinagongana, hazina ukweli, hazina msingi, basi mimi niko tayari kuondoka katika nafasi yangu. Kama kauli zangu zitakuwa hazina ukweli, hazisimamii maelekezo ya serikali, basi mimi niko tayari kufanya hivyo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuongezea jibu la nyongeza la swali la Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Mwakilishi wa Jimbo la Muyuni).

Mhe. Mwenyekiti, nataka kwanza nikubaliane na Mhe. Naibu Waziri, kwa kusema kwamba meli ya *MV*. Jitihada ilikwenda Tumbatu kwa ombi maalum na kibali maalum, hasa kwa kuzingatia kwamba siku kubwa kwa wananchi wa kisiwa cha Tumbatu, ni siku ya mwezi 27 na siku ya mwezi 28, ambapo siku hiyo huwa tunasherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (*SWA*), kwa kusoma Maulid makubwa sana ambayo huwajumuisha Waislamu wanaofika 10,000.

Mhe. Mwenyekiti, idadi hiyo ya Waislamu hao hupaswa serikali kuzingatia kupeleka nguvu maalum kati ya Mkokotoni na Kisiwani Tumbatu. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, kwamba watu 10,000 kuwavusha kwa vyombo vya kawaida, ni watu wengi sana na hasa ikizingatiwa nyakati hizo huwa ni nyakati za upepo wa Kaskazi, ni hatari kuwavusha kwa vidau au kwa mashua ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu watu wa Tumbani ni sehemu ya Wazanzibari ambao wanatakiwa wazingatiwe kupata haki zao, kwa kuzingatia Katiba na sheria na kuzingatia utawala bora, basi ni vizuri zaidi serikali ikawa inajali kwamba kule wanakwenda watu, hasa kwa siku hii tukufu ya kusherehekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad (*SWA*).

Mhe. Mwenyekiti, *MV*.Jitihada haikwenda Tumbatu kupeleka abiria, ilipeleka wananchi kwa dharura maalum. Ahsante sana. (*Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, swali langu mimi ni kuwa Mhe. Waziri, alipojibu kasema kulikuwa na ombi maalum na kibali maalum, sawa, lakini leo tunaendelea wananchi kutoka Mkokotoni na Tanga wanaacha usafiri wa uhakika,kwa mfano meli na jahazi lipi lililokuwa bora na watu wanaendelea kuteseka na kupoteza maisha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nafikiri baada ya majibu ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, naomba uridhike.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hamna tabu wananchi wameshatusikia huko.

Nam. 82

Sensa ya Mifugo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante, pamoja na Kanuni za kuuliza maswali, kulikuwa kuna Wajumbe wengine walikuwa wanataka kuuliza swali la nyongeza, lakini nafikiri muda unafanya haraka, tuendelee. Naomba swali langu nambari 82, lipate jawabu.

Kwa kuwa ni muhimu kujua idadi ya mifugo yote Zanzibar na kwa kuwa sensa hiyo ina umuhimu mkubwa kwa ustawi wa sekta hiyo.

Je, serikali ina mpango gani wa kupata takwimu *data* sahihi za wanyama ili zitumike kwa wakati ujao?

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, ahsante kabla ya kujibu swali hili napenda kuwafahamisha Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Zanzibar, inashirikiana na Ofisi ya Taifa ya takwimu ya Tanzania na kufanya sensa ya kilimo na mifugo, ambayo hujumuisha idadi ya mifugo na mazao ya mifugo kwa kila baada ya kipindi cha miaka 5.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa maandalizi ya sensa hiyo yapo katika hatua nzuri na inategemewa kufanyika baada ya mpango huu kukamilika. Mbali na kukusanya taarifa za idadi ya mifugo mbali mbali na mazao ya mifugo kama vile mayai, maziwa, ngozi na kadhalika, hufanyiwa uchambuzi kwa ajili ya matumizi mbali mbali Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba sasa kujibu swali nambari 82 kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, idadi ya mifugo yetu katika mchanganuo mbali mbali, kama ngombe wa maziwa, ng'ombe wa nyama, kuku wa aina tofauti tunazo na zinatumika kupanga mambo mbali mbali ya kitaifa. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa mara ya mwisho sensa ya mifugo ilifanyika lini Zanzibar?

Kama takwimu zipo kwa nini zibaki kwenye Kamati wakati swali langu linahitaji kujua *data* na manufaa kwa wananchi na wataalamu wengine?

Kwa kuwa Mhe. Waziri, anasema wako mbioni kufanya sensa, ni lini zoezi hilo litakamilika na kuletewa taarifa hiyo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, tunazo takwimu za mwaka 2013 na kama nilivyoeleza kwamba takwimu zinafanyika kila baada ya miaka 5 na huwa tunashirikiana na takwimu ya sensa ya Tanzania kwa jumla. Takwimu tunazo na nafikiri kwenye bajeti tumetowa. Kwa hivyo, huo ni ushahidi kwamba tunazo takwimu.

Mhe. Mwenyekiti, la ziada ni kwamba kila wilaya kwa Mkuu wa Wilaya, basi kunakuwa na takwimu za mifugo. Kwa hivyo, ukihitaji takwimu zaidi, nenda kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya utazikuta takwimu zetu. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, mimi naomba kwanza Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri wanapotujibu maswali yetu, basi usiwape muda mrefu wakatupa dibaji, sisi tunataka jibu tu. Tunakuwa tuna hoja nzuri ya kuweza kusema tunakosa wakati wa kuweza kuwajibu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu yake mazuri Mhe. Waziri, naomba kwamba atakubaliana na mimi kuwa inaonesha katika wizara yake hakuna *data* maalum kutokana na sensa waliyoifanya ya mwaka huu 2013.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nimemsikia Mhe. Mjumbe, kwa kweli tunazo *data* maalum na ndio maana kwenye bajeti tumetoa zile *data*, kwa mfano tulitoa takwimu za ng'ombe, kuku, mbuzi, maziwa na hata nyama tumezitoa na hiyo ina maanisha kwamba tunazo *data* na wala hatukubahatisha tu.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, swali moja dogo la nyongeza. Sasa kama *data* zipo na suala hili analo zamani, kwa nini hapa asizitaje? *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutaja *data* hizo, tulitoa kwenye bajeti na hapa nitakumbusha zaidi kwa mwaka 2013. Kwa kweli tumesema kwamba tunao ng'ombe 16,200, kuku 1,078,963, mbuzi 68,953, maziwa tumezalisha tani 4,966, mayai na nyama ya ng'ombe, zote tumezitaja kwenye bajeti na hapa ninazo pia, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

HOJA ZA SERIKALI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri, kwa ajili ya kuja kutusomea hotuba yake. Kwanza kuna tangazo kidogo, leo katika ukumbi wetu wa juu tunao wageni kutoka Asasi za Kiraia, ambao wanaoshiriki kwenye Maonesho katika Viwanja vya Baraza la Wawakilihi, hapo nje kuanzia tarehe 22 hadi 24 Juni, 2014. Asasi hizo ni kutoka Pemba, Unguja na Dar-es-salaam, lakini wote wanaongozwa na ANGOZA ya Zanzibar. Sasa kama wapo hapo juu tunawaomba wasimame tuwaone. Ahsante kaeni. *(Makofi)*

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Audhubilahi Minashatwani Rajim, Bismillah Rahman Rahim. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu, sasa likae kama Kamati ya Mapato na Matumizi, kwa ajili ya kupokea, kuzingatia, kuchangia na hatimaye kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi za kawaida na maendeleo kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hotuba yangu hii yote ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2014/2015, iingizwe kwenye *Hansard* kwa ukamilifu wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutuwezesha kufika katika ukumbi huu, hii leo tukiwa wazima na afya njema. Aidha, naomba kuchukuwa fursa hii kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa, michango na ushauri mliotupatia kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa malengo ya wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi (Dk. Ali Mohamed Shein) kwa kuongoza nchi yetu kwa uadilifu, hekima na upendo mkubwa ulioziwezesha nchi yetu kuwa na amani, utulivu na mshikamano uliowafanya wananchi kuendelea kutekeleza shughuli zao za kiuchumi, biashara na uwekezaji bila wasiwasi wowote.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, napenda kumpongeza pia kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inawatumikia wananchi kwa usawa. Kadhalika, nachukua fursa hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais (Mhe. Maalim Seif Shariff Hamad) na Makamu wa Pili wa Rais (Mhe. Balozi Seif Ali Iddi) kwa jitihada zao za dhati wanazozichukua za kumsaidia Mhe. Rais wa Zanzibar katika kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, napenda vile vile, kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati ya moyo wangu Naibu Waziri wangu Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi, Katibu Mkuu Ndg. Julian Banzi Raphael, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Rashid Ali Salim, Viongozi wote wa taasisi na mashirika yaliyo chini ya wizara yangu, pamoja na wafanyakazi wote kwa juhudi zao kubwa za kuchapa kazi, pamoja na mashirikiano makubwa wanayonipatia. Hakika bila ya msaada wao, ningeshindwa kufanya kazi zangu ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, matayarisho ya bajeti hii yamezingatia misingi na sera mbali mbali za nchi zinazosimamia uchumi na maendeleo ya sekta ya biashara na viwanda pamoja na uwezo wa raslimali uliopo. Sera hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2020;
(ii) Mpango wa Ukuzaji Uchumi na Kuondoa Umasikini Zanzibar (MKUZA);
(iii) Maelekezo ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika Hotuba yake ya ufunguzi wa Baraza la Wawakilishi;
(iv) Mpango Mkakati (*Strategic Plan*) wa Wizara 2012 – 2015;
(v) Miongozo ya Kisera inayosimamiwa na Wizara; na
(vi) Utekelezaji wa Mkakati Maalum wa Serikali wa Kuimarisha Sekta ya Utalii nchini, Mazingira ya biashara na ukusanyaji wa rasiliamli fedha.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mazingatio hayo, utayarishaji wa mapendekezo ya bajeti hii, kama ilivyo kawaida umezingatia pia matokeo makubwa yaliyojitokeza ulimwenguni na ambayo yamekuwa na athari za moja kwa moja katika mwenendo wa biashara duniani, uchumi, fedha na pia hali ya kisiasa katika nchi na maeneo mbali mbali duniani, pamoja na athari zake kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mapendekezo ya bajeti hii yamepitia katika ngazi mbali mbali za uzingatiaji wa awali na hususan Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi. Naomba kuchukua nafasi hii kuishukuru sana Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni) kwa kuchambua mapendekezo ya bajeti hii, kuikubali na hatimae kuridhia kuwasilishwa mbele ya Baraza lako tukufu kwa kujadiliwa na kuidhinishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu kuhusu bajeti hii, nitaanza kwa kufanya mapitio ya jumla ya mwenendo wa biashara ulimwenguni na jinsi ulivyogusa hali ya biashara ya Zanzibar, kufanya mapitio kuhusu hali ya viwanda, utekelezaji wa bajeti ya wizara kwa mwaka 2013/2014, hali ya Mashirika ya Serikali yaliyo chini ya Wizara, kubainisha changamoto mbali mbali na hatimae kubainisha malengo kwa mwaka 2014/2015 na sura ya bajeti ya Wizara kwa kipindi hicho.

MWENENDO WA BIASHARA

Hali ya Biashara Ulimwenguni

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu kama hii kwa mwaka 2013/2014, nililiarifu Baraza lako tukufu kuhusu kuendelea kuyumba kwa uchumi na biashara duniani kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo kudorora kwa uchumi wa nchi za magharibi na migogoro ya kisiasa. Hali ya mwenendo wa uchumi wa dunia na biashara, bado haujatengemaa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014, mwenendo wa jumla wa biashara duniani (*World Merchandize Trade*) umeonesha ongezeko la asilimia 0.1 kutoka ongezeko la asilimia 2.0 mwaka 2012 hadi kufikia ongezeko la asilimia 2.1 kwa mwaka 2013. Hali hii imesababisha mwenendo wa biashara duniani kuendelea kuwa wa kasi ndogo. Hata hivyo, matarajio ya jumla kwa mwaka 2014 ni kuibuka kwa biashara ambapo inatarajiwa kuwa kasi ya ukuaji wake itafikia asilimia 4.7. Matumaini hayo yanatokana na matarajio ya kuongezeka kwa mahitaji ya uagiziaji kutoka Uchina na Marekani.

Usafirishaji Bidhaa Duniani

Mhe. Mwenyekiti, kiwango cha usafirishaji bidhaa duniani kilifikia *USD* 18,794 bilioni kwa mwaka 2013 kutoka *USD* 17,849 bilioni ikilinganishwa na mwaka 2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 5.3. Kwa upande wa usafirishaji wa huduma, ulifikia *USD* 4,625 bilioni kwa mwaka 2013, kutoka *USD* 4,360 bilioni kwa mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 6.

Uagiziaji Bidhaa Duniani

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uagiziaji bidhaa kwa mwaka 2013 ulifikia *USD* 18,906 bilioni kutoka 18,146 bilioni kwa mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 3.8. Kwa upande wa uagiziaji wa huduma, ulifikia *USD* 4,340 bilioni kwa mwaka 2013, kutoka *USD* 4,173 bilioni kwa mwaka 2012 sawa na ongezeko la asilimia 4. Mwenendo wa usafirishaji na uagiziaji bidhaa huo ni kama unavyoonekana katika Jadweli Nam. 1 hapa chini.

Jadweli Nam. 1:
Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa Duniani 2013
(*USD* bilioni)

Kanda	Usafirishaji	Asilimia	Uagiziaji	Asilimia
Ulaya	6,640	35.3	6,590	34.9
Asia	6,290	33.5	6,370	33.7
Marekani/ kaskazini	2,420	13	3,200	16.9
Mashariki ya Kati	1,330	7.1	770	4.1
Jumuiya ya Madola	778	4.1	575	3
Marekani/Kusini	737	3.9	773	4.1
Afrika	599	3.2	628	3.3
Jumla	18,794	**100**	**18,906**	**100**

***IMF/Word Bank* na *WTO*.**

Mhe. Mwenyekiti, usafirishaji na uagiziaji kwa upande wa nchi za Afrika umeendelea kuwa wa kiwango kidogo ikilinganishwa na kanda nyengine. Kwa mwaka 2013 usafirishaji wa nchi za Afrika ulifikia *USD* 599 bilioni ikilinganishwa na usafirishaji wa *USD* 626 bilioni kwa mwaka 2012. Kwa upande wa uagiziaji nchi za Afrika, ziliagiza bidhaa zenye thamani ya *USD* 628 bilioni mwaka 2013 kutoka bidhaa zenye thamani ya *USD* 604 bilioni mwaka 2012 ikiwa ni ongezeko la asilimia 3.3

Hali ya Kibiashara Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, mchango wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa ni asilimia 9.3 mwaka 2013 kutoka asilimia 9.5 mwaka 2012. Kwa upande wa ukuaji wa sekta hiyo ya biashara mchango wake umepungua kutoka asilimia 10.2 kwa mwaka 2012 na kufikia asilimia 7.7 mwaka 2013. Upungufu huo umetokana na kupungua kwa uagiziaji wa bidhaa hasa wa mitambo kwa mwaka 2013.

Usafirishaji na Uagiziaji Bidhaa

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar imesafirisha bidhaa zenye thamani ya *TZS* 87,799.65 milioni kwa mwaka 2013, kutoka bidhaa zenye thamani ya *TZS* 67,390.5 milioni kwa mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 30.3. Bidhaa zilizosafirishwa ni pamoja na karafuu, mwani, mpira, mazao ya baharini na bidhaa nyengine za kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uagiziaji, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya *TZS*. 208,051.87 milioni kwa mwaka 2013 ikilinganishwa na uagiziaji wa *TZS.* 271,273.1 milioni mwaka 2012, sawa na upungufu wa asilimia 23.3. Upungufu huo wa uagiziaji bidhaa kwa kiasi kikubwa umesababishwa na kupungua kwa bidhaa za ujenzi na mitambo hasa ya uwekaji wa umeme. Bidhaa zilizoagizwa kwa kiasi kikubwa kutoka nje ni pamoja na vyakula, vifaa vya ujenzi, na magari.

Biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara (*Inter-state Trade Balance*)

Mhe. Mwenyekiti, mwenendo wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa mwaka 2013 unabainisha ongezeko la usafirishaji kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Usafirishaji kutoka Zanzibar uliongezeka kutoka *TZS.* 224,400.5 milioni mwaka 2012 hadi kufikia *TZS.* 501,204.2 milioni mwaka 2013 sawa na ongezeko la asilimia 123.4. Kutokana na ongezeko hilo, wizara inaendelea na uchambuzi wa takwimu za bidhaa zilizosababisha ongezeko hilo.

Mhe. Mwenyekiti, aidha kwa upande wa uagiziaji, Zanzibar iliagiza bidhaa zenye thamani ya *TZS* 61,869.3 milioni mwaka 2013 ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya *TZS* 79,666.2 milioni kwa mwaka 2012 sawa na upungufu wa asilimia 22.3.

Usafirishaji Bidhaa kupitia Bandari Huru

Mhe. Mwenyekiti, usafirishaji bidhaa kupitia utaratibu wa Bandari Huru (*Free Port*) nao umeongezeka kwa mwaka 2013 ambapo thamani ya usafirishaji huo ilifikia *TZS*. 2,400.0 milioni ikilinganishwa na *TZS.* 2,211.0 milioni mwaka 2012. Hili ni ongezeko la asilimia 8.6 kama inavyoonekana katika Jadweli Nam. 2. hapa chini.

Jadweli Nam. 2
Usafirishaji kwenda na kutoka Tanzania Bara na kupitia Bandari Huru TZS. (Milioni)

Mwaka	2010	2011	2012	2013
Kuja Zanzibar	23,268.7	74,738.3	79,666.2	61,869.3
Kwenda Tanzania Bara	2,203.8	71,396.8	224,400.5	501,204.2
Urari wa Biashara	-21,064.9	-3,341.1	144,734.3	439,334.9
Uhaulishaji (Bandari Huru)	1,099.7	1,307.6	2,211.0	2,400.0

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali

HALI YA MASOKO

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kama zilivyo nchi mbali mbali duniani inafanya biashara na Mataifa kadhaa ulimwenguni katika Mabara ya Asia, Ulaya, Marekani na hata nchi jirani za Afrika Mashariki. Sehemu kubwa ya bidhaa zinazosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda nje zinatokana na mazao ya kilimo na mazao ya baharini ambayo ni karafuu, mpira, mwani na mazao mengine ya baharini. Kwa upande mwengine, Zanzibar inaagiza kutoka nje bidhaa za chakula, umeme, ujenzi na nguo.

Mwenendo wa Bei za Chakula Muhimu Duniani

Mhe. Mwenyekiti, mwenendo wa bei za chakula muhimu katika soko la dunia kwa mwaka 2013, ulipungua kwa wastani wa asilimia 8.2 ikilinganisha na mwaka 2012. Mwenendo huo ulisababisha kuwepo kwa utulivu wa bei katika masoko hayo. Jadweli la Nam. 3 hapo chini linaonesha mwenendo huo wa bei.

Jadweli Nam. 3
Wastani wa Bei za chakula muhimu katika Soko la Dunia 2013 (*USD*/MT)

Bidhaa	2012	2013	Mabadiliko (%)
Mchele	517	465	-10.1
Sukari	785	750	-4.5
Unga Ngano	500	450	-10
Mabadiliko (%)			**-8.2**

Chanzo: www.indexmundi.com

Mwenendo wa Bei za Chakula Muhimu katika soko la ndani

Mhe. Mwenyekiti, mwenendo wa bei za bidhaa za chakula muhimu uliendelea kuwa wa utulivu kutokana na kupungua kwa bei katika soko la dunia, pamoja na hatua za udhibiti zinazoendelea kuchukuliwa na serikali za kushauriana na wafanyabiashara wa bidhaa hizo na kukubaliana bei za uuzaji rejareja. Jadweli Nam. 4 linaonesha wastani wa bei za bidhaa hizo.

Jadweli Nam. 4
Wastani wa Bei za Reja Reja za Chakula muhimu katika soko la Zanzibar (TZS/Kilo)

Bidhaa	2012	2013	Mabadiliko (%)
Mchele	1150	1100	-4.3
Sukari	1700	1350	-20.6
Unga Ngano	1100	1100	0
Mabadiliko (%)			**-8.3**

Chanzo: Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi hicho cha mwaka 2013/2014, hata hivyo, kulijitokeza tatizo la kutokuwepo utulivu wa bei kwa baadhi ya bidhaa zengine za vyakula hasa tungule, vitunguu, mbatata, mboga na viungo vyengine vinavyotumika kwa wingi hapa Zanzibar. Hali hiyo, ilitokana na uzalishaji mdogo wa ndani ya Zanzibar na uagiziaji mdogo kutoka Tanzania Bara, uliosababishwa na kuwepo kwa hali mbaya ya hewa na ugumu wa upatikanaji wa bidhaa zenyewe. Mabadiliko ya hali ya hewa yaliathiri usafiri na usafirishaji wa bidhaa hizo kwa njia ya bahari.

Mwenendo wa Bei ya Karafuu na Mwani

Mhe. Mwenyekiti, wastani wa mwenendo wa bei za mazao makuu yanayozalishwa Zanzibar na kuuzwa katika masoko ya dunia ulikuwa wa mchanganyiko:

Bei kwa kilo moja (*USD*)

	2012	**2013**
Karafuu	10	11.5
Mwani	0.3	0.3
Mpira	3.03	2.5

Mhe. Mwenyekiti, sura ya mwenendo huo inaonesha zao la karafuu bado linaendelea kuwa na soko zuri licha ya kuwepo hali ya kupanda na kushuka. Kuwepo kwa soko hilo zuri kwa zao la karafuu, kumeiwezesha serikali kuweka bei nzuri ya kununulia karafuu kwa wakulima ambapo kwa kila kilo inayouzwa nje, mkulima analipwa asilimia 80 ya bei hiyo. Kwa upande wa mazao ya mwani na mpira, bado bei zake ziliendelea kuwa za kiwango cha chini na hivyo kuleta athari kwa tija ya mazao hayo na ajira. Mazao hayo ya mpira na mwani yanatoa ajira nyingi kwa sasa hasa wanawake.

Urahisishaji Biashara (*Trade Facilitation*)

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu kama hii kwa mwaka 2013/2014, nilielezea kuhusu ongezeko la biashara, uagiziaji na utoaji wa makasha (*containers*) katika bandari ya Malindi Zanzibar na jinsi ongezeko hilo linavyoathirika na ufinyu wa vifaa na nafasi katika bandari hiyo. Nilielezea pia dhamira ya serikali ya kuchukua hatua za muda mfupi na zile za muda mrefu zitakazo husisha ujenzi wa bandari nyengine mpya. Hatua hizo ziliendelea kuchukuliwa kama zitakavyofafanuliwa na Wizara husika. Hata hivyo, bado uwezo wa bandari yetu ni mdogo ikilinganishwa na ongezeko la biashara na hivyo, kusababisha msongamano mkubwa wa makasha ya bidhaa katika eneo la bandari.

Mazingira ya Kufanya Biashara

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2013/2014, nililiarifu Baraza lako tukufu kuhusu utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia kuhusu mazingira ya ufanyaji wa biashara ambapo Zanzibar ilishika nafasi ya 155 kati ya nchi 183 ilizolinganishwa nazo. Serikali tayari imeanza kuchukua hatua za kutekeleza mapendekezo ya utafiti huo.

Mhe. Mwenyekiti, hatua hizo ni pamoja na kuandaa Sheria mpya za Biashara, Sheria ya Usimamizi wa Utoaji leseni za Biashara, Sheria ya Usajili Makampuni na Mali na kuimarisha miundombinu mbali mbali. Pamoja na hatua hizo, serikali pia imeandaa programu maalum ya kuimarisha mazingira ya biashara kama sehemu ya mkakati wake wa kuimarisha sekta ya utalii hapa nchini.

HALI YA VIWANDA

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa 2013, sekta ya viwanda bado imeendelea kuchangia chini ya asilimia kumi (asilimia 8.2) katika Pato la Taifa. Kwa upande wa sekta ndogo ya usarifu wa bidhaa mchango wake nao uliendelea kuwa mdogo ambapo kwa mwaka 2013 ilichangia asilimia 3.2. Juhudi mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa na serikali kwa dhamira ya kuhuisha sekta ya viwanda zikiwemo kutenga maeneo ya viwanda ya Fumba, kuimarisha nishati ya umeme, kujenga mfumo wa vivutio kwa uwekezaji katika sekta ya viwanda. Kwa kipindi kirefu mwitikio wa uwekezaji na wawekezaji wazalendo ulikuwa mdogo. Katika siku za karibuni hata hivyo, dalili za kukua kwa sekta hiyo zinazojitokeza kutokana na mambo yafuatayo:-

a. Kuanzishwa kwa viwanda mbali mbali vya maji ambavyo vinaendelea kusarifu bidhaa hizo na kuuza katika soko la ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara;

b. Kuanza uzalishaji kwa kiwanda cha sukari Mahonda baada ya Kiwanda hicho kufanyiwa uwekezaji mkubwa;

c. Uwekezaji unaofanywa na Kundi la Makampuni ya Bakhressa wa kujenga kiwanda kikubwa cha kusarifu bidhaa za maziwa (*Azam Diary Factory*) ambapo kiwanda hicho kimefikia hatua za mwisho za kukamilisha ujenzi na kuanza kutoa huduma;

d. Uanzishaji wa kiwanda cha kusarifu mafuta ya mimea na chumvi unaofanywa na *ZSTC* kwa kushirikiana na Kampuni ya *Land* ya Japan; na

e. Kuendelea kukua kwa viwanda vidogo vidogo vya wajasiriamali hasa katika usindikaji wa vyakula, kazi za mikono, viwanda vya ujenzi na viwanda vya Samani.

Kusita kwa Uzalishaji wa kiwanda cha *CocaCola*

Mhe. Mwenyekiti, wakati hali ya uwekezaji katika viwanda ikianza kushamiri, kiwanda cha *CocaCola* kimesimamisha uzalishaji bidhaa hapa Zanzibar. Kwa sasa kiwanda hicho kinaendelea na shughuli za uuzaji wa bidhaa zake zinazotengenezwa katika viwanda vilivyopo nje ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya wawekezaji ni kwamba usimamishaji huo umetokana na kuchakaa kwa mitambo ya kiwanda ambayo kwa sasa haiendi sambamba na mahitaji ya soko, pamoja na kutohimili ushindani unaotokana na uingizaji wa soda kutoka nje bila ya kulipa kodi stahiki. Baada ya mazungumzo na serikali, wawekezaji wa kiwanda hicho wameahidi kufanya uwekezaji mpya wa mitambo hiyo ili iendane na mahitaji ya sasa ya soko. Hata hivyo, serikali bado inaendelea na majadiliano na wamiliki wake ili kuona ahadi hiyo inatekelezwa kulingana na ratiba itakayokubalika.

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo ya jumla ya hali ya biashara, mwenendo wa bei za bidhaa muhimu pamoja na maendeleo ya viwanda kwa mwaka 2013. Naomba sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, wizara yangu iliidhinishiwa kutumia kiasi cha *TZS.* 4,990 milioni. Kati ya fedha hizo TZS 1,610 milioni ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, *TZS.* 930.0 milioni ni kwa ajili ya mishahara na *TZS.* 1,150.0 milioni ni ruzuku kwa taasisi zilizo chini ya Wizara na *TZS* 1,300.0 milioni kwa kazi za maendeleo. Mgawanyo wa matumizi hayo ulikuwa kama ifuatavyo:-

Bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2013-2014 (TZS Mil)

FUNGU	BAJETI YA MWAKA	KILICHOINGIZWA	ASILIMIA YA BAJETI
Matumizi ya Kawaida	2,540.00	1,635.24	64.4
Matumizi ya Maendeleo	1,300.00	268.64	20.7
Ruzuku	1,150.00	628.63	54.7
Jumla kubwa	**4,990.00**	**2,532.51**	50.8

Mhe. Mwenyekiti, mgawanyo wa fedha hizo kwa kila Idara ni kama inaonekana hapo chini.

Idara	Bajeti ya mwaka	Kilichoingizwa	Asilimia ya Bajeti
A: Kazi za Kawaida (TZS Milioni)			
Afisi Kuu Pemba	346.95	216.3	62.3
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	372.95	106.77	28.6
Idara ya Biashara	367	197.85	53.9
Idara ya Viwanda	260.9	102.32	39.2
Idara ya Utumishi na Uendeshaji	1,192.20	1,012.00	84.9
Jumla	**2,540.00**	**1,635.24**	**64.4**

B: Ruzuku (TZS Milioni)			
Baraza la Biashara	300	104.93	35
Kamisheni ya Ushindani	100	44.5	45
Mamlaka ya Vipimo	150	0	0
Taasisi ya Viwango	600	479.2	80
Jumla	**1150**	**628.63**	**54.7**

C: Kazi za Maendeleo			
Eneo Tengefu (*SEZ development Strategy*)	130	14.78	11.4
Kukondoesha Maendeleo ya Biashara Zanzibar	300	70	23.3
Kuimarisha Shirika la Viwango (*ZBS*)	500	85.86	17.2
Mkakati wa Maendeleo ya Karafuu	150	50.26	33.5
Kuweka Mazingira mazuri ya Viwanda	220	47.74	21.7
Jumla	**1,300.00**	**268.64**	**20.7**
JUMLA KUU (A+B+C)	**4,990.00**	**2,532.51**	**50.8**

Ukusanyaji wa Mapato:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ilikadiria kukusanya *TZS* 90.0 milioni katika chanzo chake ada za ukaguzi wa Mizani na Vipimo. Hadi kufikia mwezi wa Mei 2014, mapato ya *TZS* 83.57 milioni yalikuwa yamekusanywa. Kiasi hicho cha makusanyo ni sawa na asilimia 92.86 ya makisio ya makusanyo yote kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Utekelezaji wa Malengo

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara ilijipangia kutekeleza malengo kumi na tano (15) kama inavyoonekana katika Kiambatisho Nam 1. Hata hivyo, kwa madhumuni ya kurahisisha ufafanuzi wa utekelezaji wa malengo hayo, naomba kutoa maelezo yake kiidara kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/14, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipanga kutekeleza malengo manne (4) ambapo utekelezaji wake uko kama hivi ifuatavyo:-

i. Kukuza ushindani wa kibiashara ili kuweka usawa na kuimarisha ustawi wa mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Wizara imekamilisha utungaji wa Sheria mpya ya Biashara ya mwaka 2013 na Sheria mpya Usimamizi wa Utoaji wa Leseni ya Biashara 2013. Kwa upande wa Sera ya Biashara ya mwaka 2006, Wizara inaendelea kufanya mapitio ya Sera hiyo kwa kushirikiana na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*ZIFA*).

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Wizara ilipanga na kuanza maandalizi ya awali ya kuandaa Sera ya Ushindani. Hata hivyo, ilibainika kuwa kuna uhusiano mkubwa na wa kipekee kati ya masuala ya ushindani na masuala ya kumlinda mtumiaji. Hivyo, masuala haya yatazingatiwa kwa pamoja na kwa mujibu wa matamko ya kisera katika maeneo haya mawili.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa serikali imechukua hatua kadhaa za kutekeleza mapendekezo ya Utafiti wa Benki ya Dunia kuhusu hali ya mazingira ya biashara Zanzibar, Wizara yangu kupitia Idara hii ilishiriki kikamilifu katika kuandaa programu maalum katika utekelezaji wa Mkakati wa Serikali wa kuimarisha Sekta ya Utalii. Katika programu hiyo miradi mbali mbali imeibuliwa inayohusisha ukuzaji wa ujasiriamali, taratibu za usajili biashara, utoaji wa leseni za biashara pamoja na mpango wa matumizi ya ardhi.Utekelezaji wa miradi hiyo utaratibiwa na Idara hii.

ii. Kufanya utafiti wa bidhaa na masoko.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili Wizara kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo (*ITC, UNIDO*) na Taasisi ya Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*) imefanya tafiti zifuatazo:

a. Kufanya tathmini ya matumizi sahihi ya teknolojia katika uzalishaji na ukaushaji wa chumvi kwenye Kiwanda cha Chumvi cha Wawi, Pemba;

b. Kufanya upembuzi yakinifu na kutayarisha mpango wa ufufuaji wa Kiwanda cha Mafuta ya Makonyo kilichoko Pemba;

c. Kufanya Upembuzi yakinifu wa kuongeza thamani wa mazao ya mwani; na

d. Kufanya upembuzi yakinifu juu ya kuongeza thamani mazao ya viungo.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo ya tafiti ya ukulima wa chumvi na kiwanda cha makonyo yamezingatia zaidi matumizi ya teknolojia mpya ya uzalishaji. Kwa upande wa matokeo ya utafiti wa mwani na viungo, tafiti zimebaini uwezekano wa kuwepo matumizi mapya ya mazao hayo ambayo hatimaye yataongeza thamani kwa wakulima. Hatua inayofuata hivi sasa ni utekelezaji wa mapendekezo ya tafiti hizo katika hatua za majaribio.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inaendelea na jukumu lake la kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa usafirishaji bidhaa nje (*NES*). Madhumuni ya Mkakati huo ni kuongeza usafirishaji nje kwa lengo la kupunguza nakisi katika urari wa biashara. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imekusanya taarifa zinazohusiana na sekta ndogo za uzalishaji zifuatazo:

Sekta ndogo ya viungo (*Spice Sub sector*)

Mhe. Mwenyekiti, hatua zilichukuliwa katika eneo hili ni pamoja na:

- Kuandaa mazingira ya kuongeza thamani ya mazao ya viungo kwa kutumia tasnia ya Haki Miliki;
- Kuanzisha Taasisi ya Viwango;
- Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu; na
- Kuanzisha mpango wa kusaidia wajasiriamali wa kuimarisha ubora wa vifungashio na ufungashaji bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa shughuli hizo, umefanyika kwa kuanzisha mpango wa kuongeza thamani za bidhaa za viungo kwa kuzifanyia *branding* karafuu na mazao mengine ya viungo. Aidha, serikali imekwishaanzisha Taasisi ya viwango ambayo itaweka na kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Mfuko wa Maendeleo ya mazao ya viungo, serikali imetunga Sheria ya Maendeleo ya karafuu, ambapo kwa kuanzia mfuko huo utashughulikia karafuu.

Masuala Mtambuka

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Masuala Mtambuka, Mkakati huo umeainisha maeneo muhimu yafuatayo:

- Kuimarisha usimamiaji wa Sheria na Kanuni za Biashara;
- Kuanzisha mfumo wa ushindani wa kibiashara;
- Kuunganisha umeme kutoka gridi ya Taifa kwenda kisiwani Pemba;
- Kufanya matengenezo ya barabara za ndani za miji; na
- Kufanya ununuzi wa vifaa katika bandari na viwanja vya ndege.

Mhe. Mwenyekiti**,** maeneo yaliyofanyiwa kazi na kukamilika katika eneo hili ni pamoja na kupeleka umeme wa uhakika kutoka Tanga mpaka Kisiwani Pemba, Sheria zinazosimamia biashara ambapo Sheria za Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara, Sheria ya Biashara, Sheria ya Makampuni zimetungwa. Aidha, barabara za ndani za miji zinaendelea kufanyiwa matengenezo na vifaa katika bandari na viwanja vya ndege vinaimarishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Wizara pia iliendelea kufuatia makubaliano ya kibiashara ya Kikanda kuhusiana na masuala ya utekelezaji wa Itifaki wa Soko la Pamoja la *EAC*, Uondoshwaji wa vikwazo vya kibiashara visivyokuwa vya kodi (*NTBs*), utayarishaji wa Sera ya *SEZ* ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki pamoja na kuianisha vivutio katika maeneo ya uwekezaji. Wizara itaendelea kufuatilia masuala hayo na yale ya kanda nyengine za kiuchumi ili kuimarisha uhusiano wa kibiashara.

Kuandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa malengo ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Wizara imefanya mapitio ya mpango mkakati wake kwa madhumuni ya kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu yake na kuyazingatia katika utayarishaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015.

Utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi ya *ZSTC*.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara inaendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Mageuzi wa *ZSTC* ambapo kwa mwaka 2013/2014, ilisimamia mambo yafuatayo:

a. Kutunga Sheria ya Maendeleo ya Karafuu;
b. Kupunguza wafanyakazi na kuwalipa stahiki zao;
c. Kuratibu shughuli za Kikosi Kazi cha Karafuu ili kupambana na magendo ya karafuu; na
d. Uimarishaji wa vituo vya ununuzi wa karafuu.

Utekelezaji wa masuala mtambuka.

Mhe. Mwenyekiti, katika utekelezaji wa masuala mtambuka, ya *UKIMWI*, Jinsia na Mazingira, Wizara ilitekeleza mambo yafuatayo:

a. Iliendelea kutoa mafunzo na uelewa juu ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi, pamoja na kuwahamasisha wafanyakazi kuhusiana na umuhimu wa upimaji wa hiari (*Voluntary Care and Testing – VCT*);
b. Ilishiriki katika Tamasha la Kijinsia lililoandaliwa na Tanzania *Gender Network Program*; na
c. Ilishiriki katika mafunzo ya mabadiliko ya tabia nchi katika nchi za visiwa.

Mradi wa Mkakati wa Kuendeleza Zao la Karafuu

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza mradi huu, Wizara inajukumu la kuifanyia *branding* karafuu ya Zanzibar. Katika kutekeleza mradi huu, imeonekana kuna haja ya kujumuisha mazao ya mdalasini, pilipili hoho na pilipili manga. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imetekeleza kazi zifuatazo:

- Kutoa mafunzo kwa wataalamu wa taasisi za serikali na sekta binafsi kwa ajili ya utayarishaji wa Mkakati huo. Mafunzo hayo yalipelekea kuandaliwa kwa taarifa ya hali ya upatikanaji wa karafuu na viungo vyengine;
- Kuandaa Kanuni za Sheria ya Haki Miliki ya 2008 (*Zanzibar Industrial Property Act*, 2008);
- Kuandaa mpango majaribio (*Test phase*) wa kuuza karafuu na bidhaa za viungo kwa soko la ndani;
- Kununua vifaa vya kufungashia bidhaa zitazouzwa kwa ajili ya awamu ya majaribio;
- Kununua bidhaa za mdalasini, pilipili hoho, pilipili manga na karafuu kwa ajili ya awamu ya majaribio; na
- Kuandaa kitabu cha muongozo (*inspiration book*) kwa ajili ya '*branding'* ya mazao ya viungo.

Mhe. Mwenyekiti, hatua zinazofuata ni kuandaa vigezo vya ubora na uthibitishaji (*standards and certification*), kuandaa Historia ya karafuu, Jiografia, sifa ya karafuu ya Zanzibar na jinsi inavyotofautiana na karafuu za nchi nyengine ili karafuu ya Zanzibar iweze, hatimae kulindwa kwa kutumia "*geographical indication – GI*"

Mradi wa Kujenga uwezo wa kukondoesha Biashara Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, katika mradi huu, Wizara ilikusudia kuandaa Mpango Mkuu (*Master Plan*) ya ujenzi wa mradi wa kujenga kiwanja cha maonesho ya biashara. Napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Wizara kwa kushirikiana na *UNDP* iliandaa na kutangaza zabuni ya kumpata mshauri mwelekezi wa kutayarisha

Mpango Mkuu (*Master Plan*) ya kuendeleza kiwanja hicho. Kazi ya matayarisho ya Mpango huo kwa ajili ya uwanja inaendelea.

Mradi wa Mkakati wa Kuifanya Zanzibar kuwa Eneo Tengefu la Uchumi - *SEZ*

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza mradi huu, Wizara ilipanga kuandaa Sera ya *SEZ*, kuandaa Sheria ya *SEZ*, pamoja na Mkakati wa utekelezaji wa Mpango. Kutokana na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa mwaka huu kazi hii haikuweza kutekelezwa kwa ukamilifu kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, Wizara inaendelea na mazungumzo na wataalamu walioandaa Utafiti wa Maendeleo ya *SEZ* ili kuangalia njia bora ya utekelezaji wa mapendekezo yake hatua kwa hatua.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

Kuimarisha Rasilimali watu

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha rasilimali watu, Wizara imewapatia wafanyakazi 7 mafunzo ya muda mrefu katika fani za biashara, Sheria, uhasibu na wafanyakazi saba (7) walipatiwa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, utayarishaji wa muundo wa utumishi na mfumo wa urithishaji madaraka unaendelea kutayarishwa na Wizara ya Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma.

Kuimarisha vitengo vya Manunuzi, Ukaguzi wa hesabu za ndani, Elimu Habari na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuimarisha vitengo vya Wizara, Idara imefanya ununuzi wa vifaa mbali mbali kama vile Kompyuta, printa, kamera na vifaa vyake pamoja na kutoa mafunzo.

Kukuza ushiriki wa Zanzibar katika majadiliano ya kibiashara ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara iliratibu safari za kikazi za Viongozi wa Wizara na watendaji wake na kuweza kushiriki mikutano ya majadiliano ya Kikanda na Kimataifa yanayohusiana masuala ya utekelezaji wa Itifaki wa Soko la Pamoja la *EAC*, Uondoshwaji wa vikwazo vya kibiashara visivyokuwa vya kodi (*NTBs*).

Kusimamia masuala ya utumishi na utawala kwa kuimarisha mazingira ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kusimamia masuala ya utumishi na utawala kwa kuimarisha mazingira ya kazi, Idara iliendelea na ukarabati wa majengo yake ya makao makuu na Idara ya Viwanda, ambapo majengo hayo kwa sasa yamekamilika na kutumika. Aidha, Idara imefanya ununuzi wa samani za Ofisi, vifaa vya kompyuta na kulipia huduma muhimu za Wizara kama vile kulipia umeme na maji, huduma za mawasiliano na vifaa vyengine vya kiofisi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa utunzaji wa mali za Wizara, daftari la kuwekea taarifa kuhusu uwekaji na uondoshwaji wa mali limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria.

IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko kwa mwaka 2013/2014, ilitekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

Kukuza Ushindani wa Kibiashara ili kuweka usawa na kuimarisha ustawi wa mtumiaji

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara ilifanya ukaguzi wa vituo vya vipimo na mezani, vituo vya mafuta, maduka maghala na *super market.*

Matokeo ya ukaguzi uliofanyika umefikia wastani wa asilimia 79.3 kama yanaonekana katika Jadweli la hapo chini.

Eneo la Ukaguzi	Lengo 2013/14	Utekelezaji	Asilimia ya utekelezaji
Vituo vya mafuta, *flowmeter*, magari, na matangi	150	121	80.7
Mezani na vipimo	2,500	1,920	76.8
Maduka na *super markets.*	2,506	2,206	88.0
Maghala na bekari	200	143	71.5
Wastani wa utekelezaji wa jumla			**79.3**

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa utafiti wa maduka, taarifa za awali zinaonesha kuwepo kwa maduka yanayozidi 3,000. Aidha, katika kusimamia mwenendo wa bei za vyakula muhimu taarifa zake zimeelezwa katika mapitio ya mwenendo ya bei ya chakula muhimu yaliyoelezwa katika hotuba hii.

Kukuza biashara na masoko ya ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imetekeleza mambo yafuatayo:

- Kushiriki katika maonesho ya 37 ya Biashara ya Kimataifa ya saba saba ambapo wajasiriamali 50 walishiriki;
- Kuandaa Tamasha la Biashara la 2014 ambapo wafanya biashara 200 walishiriki kutoka Zanzibar, Tanzania Bara, Syria, Indonesia, India, Burundi, na Misri;
- Kushiriki katika Maonesho ya Jua Kali yaliyofanyika Nairobi ambapo wajasiriamali 48 walishiriki; na
- Kuandaa Maonesho ya *Idd El Hajj* yaliyofanyika katika Hoteli ya Bwawani, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Ukuzaji Biashara Tanzania (*TANTRADE*) ambapo Washiriki 42 kutoka ndani na nje ya nchi walionesha na kuuza bidhaa zao. Washiriki walitoka nchi za India, Malaysia, Misri na Syria. Maonesho ya *Idd El Hajj* yanatarajiwa kufanyika kila mwaka yakiwa na lengo la kuwezesha wenye viwanda na wafanyabiashara kwa ujumla kupata masoko kwa bidhaa zao katika kipindi cha Sikukuu ya *Idd El Hajj*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kuandaa misafara ya kibiashara na mafunzo ya wajasiriamali nje ya nchi hayakuweza kufanyika kutokana na ugumu wa kifedha.

Kukuza ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya kibiashara ya kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Wizara imeshiriki katika majadiliano yafuatayo:

- Uanzishwaji wa Umoja wa Forodha (*Custom Union*) kwa nchi wanachama wa *SADC* ambayo yapo katika hatua za awali;
- Mkataba wa ufunguaji wa Biashara ya Huduma kwa nchi za *SADC*; na
- Mkataba wa Kimataifa kuhusiana na masuala ya Mezani na Vipimo

Kurasimisha Biashara na mali za wafanyabiashara wadogo wadogo

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imewatambua wafanyabiashara wadogo wadogo 987 katika Wilaya za Kaskazini B (487) na Micheweni (500) chini ya mpango wa Kurasimisha Wafanyabiashara na Mali (*MKURABITA*) na kuwapatia mafunzo wajasiriamali 487. Aidha, asilimia 10 kati ya wajasiriamali hao wameweza kusajiliwa rasmi.

IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UKUZAJI UJASIRIAMALI

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

Sera ya Maendeleo ya Viwanda

Mhe. Mwenyekiti, katika matayarisho ya Sera ya Viwanda, Wizara kupitia Idara hii na kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (*UNIDO*) iliendelea na utayarishaji wa Sera hiyo na hasa utayarishaji wa taarifa ya Kimkakati (*Strategic Paper*) na kuandaa Taarifa ya Ushindani wa Kiviwanda. Kadhalika, hatua za kuimarisha uwezo wa kitaalamu kwa wataalamu wa ndani zilichukuliwa kwa kutoa

mafunzo ya wataalamu kumi (10) ili kujenga uwezo wa ndani wa kutunga, kuchambua na kusimamia utekelezaji wa sera za masuala ya maendeleo ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na kuchukua hatua na kuendelea na utayarishaji wa Sera, kazi nyengine iliyofanywa na Idara hii ni kubainisha aina za viwanda vitakavyopewa umbele katika uekezaji. Jumla ya aina kumi na moja (11) ya viwanda vimeibuliwa kwa ajili hiyo. Utambuzi huo ulitumia vigezo vya soko la bidhaa, nafasi za ajira, upatikanaji wa teknolojia, malighafi na umuhimu wa miradi hiyo kwa sekta nyengine za uchumi. Aina za viwanda vilivyoainishwa katika utambuzi huo ni kama vifuatavyo:

- Viwanda vya kutengeneza samani za mbao;
- Viwanda vya ushoni;
- Viwanda vya kusarifu mazao ya kilimo;
- Viwanda vya usindikaji samaki;
- Viwanda vya kusarifu zao la mwani na karafuu;
- Viwanda vya kuunganisha vipuri vya vyombo vya moto;
- Viwanda vya kusarifu takataka za eletronikia na plastiki;
- Viwanda vya kutengenezea vifaa vya matumizi ya nyumbani (*home appliance*);
- Viwanda vya chakula cha mifugo;
- Viwanda vya kutotolea vifaranga; na
- Viwanda vya kupikia vyakula vya ndani ya ndege (*Catering Industry*).

Mhe. Mwenyekiti, hatua za msingi zinazohitajika kuchukuliwa ili kujenga mazingira mazuri ya kuimarisha uwekezaji katika sekta ya viwanda ni pamoja na kuandaa wataalamu,kutenga maeneo ya uwekezaji viwanda, kuweka miundombinu inayohitajika, kuweka mfumo rahisi wa kutoa vivutio na kuondosha urasimu na baadae kukaribisha wawekezaji. Haya ndiyo masuala muhimu ambayo serikali inayashughulikia hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Wizara imeweza kubainisha maeneo yanayohitaji kupewa umuhimu wa vivutio ili kukuza maendeleo ya viwanda hapa Zanzibar. Maeneo hayo ni pamoja na kuwa na ardhi kwa uwekezaji wa viwanda, miundombinu imara, mfumo unaotabirika wa vivutio vya kikodi pamoja na huduma za bandari.

Mhe. Mwenyekiti, lengo jengine muhimu ambalo Wizara ilijipangia kutekeleza kwa ajili ya kuendeleza viwanda ni uanzishaji wa Kituo cha maendeleo ya viwanda. Lengo hili halikuweza kutekelezwa kutokana na kukosa jengo la kukianzishia. Hata hivyo, Wizara inaendelea na juhudi za kutafuta jengo hilo ili kuendelea na utekelezaji wa lengo hilo.

Kukuza ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya kitaifa, Kikanda na kimataifa kuhusu maendeleo ya viwanda

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imeshiriki mikutano mitatu ya Kitaifa na Kikanda (*EAC-SADC – COMESA*) iliyohusu uendelezaji viwanda kwa nchi wanachama ndani ya Jumuiya. Madhumuni makubwa ya mikutano hiyo ilikuwa ni kujenga misingi mikuu (*Industrial pillars)* ya kuendeleza viwanda katika Jumuiya hizo.

Kukuza ujasiriamali

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imeandaa vigezo maalumu kwa ajili ya uteuzi wa vikundi/miradi ya wajasiriamali vitakavyopewa usaidizi wa Wizara katika kuendeleza miradi. Vigezo vitakavyotumika ni pamoja na muombaji kuwa na usajili rasmi, uzalishaji, idadi ya ajira na ufungaji wa hesabu. Aidha, katika kusaidia wajasiriamali kwenye uandaaji wa maandiko ya miradi (*business write ups*), Wizara imeandaa miradi ya utengezaji sabuni, ukaushaji matunda na utengenezaji wa jamu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kuanzisha mfumo maalum wa vifungashio, Wizara baada ya kuangalia soko na mahitaji ya wajasiriamali imetambua aina mbili za vifungashio (*packaging*) ambavyo vinavyotumiwa zaidi na wajasiriamali wa Zanzibar. Hatua zinazofuata ni kuvinunua vifungashio hivyo na kuviuza kwa wajasiriamali kwa utaratibu utakaowekwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ukaguzi wa miradi ya viwanda, Wizara kupitia Idara hii imekagua miradi ya viwanda na miradi midogo midogo 100. Ukaguzi huo ulikuwa na lengo la kubainisha mafanikio na changamoto zinazowakabili pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu ili kuweza kuendeleza miradi yao. Aidha, Idara

imewajengea uwezo wajasiriamali juu ya uzalishaji wa bidhaa zenye ubora, usarifu wa mazao ya kilimo na ufungashaji. Katika mafunzo hayo vikundi 10 vya wajasiriamali vilishirikishwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuimarisha daftari la miradi midogo midogo ya wajasiriamali, taarifa za miradi mipya 30 ya wajasiriamali zimekusanywa na kuingizwa kwenye daftari (*database*) hilo.

Mhe. Mwenyekiti, moja la jukumu la Wizara ni kuratibu utekeleza wa Sera ya *SMEs* ambayo inatekelezwa na wadau wengi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imeandaa vikao vitatu (3) vya Kamati Tendaji ambavyo vilikuwa na lengo la kubainisha hatua iliyofikiwa ya kuwaendeleza wajasiriamali.

OFISI KUU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO– PEMBA:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi kuu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko Pemba inajukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji wa kazi zote za Wizara katika kusimamia biashara, maendeleo ya viwanda na auendelezaji masoko kwa upande wa Pemba. Shughuli zilizopangwa kufanyika ni ukaguzi wa miradi ya viwanda, ukaguzi wa mezani na vipimo, ukusanyaji wa mapato, usimamizi na uendeshaji wa biashara, na uendeshaji wa Ofisi. Utekelezaji wa kazi hizo umejumuishwa katika ufafanuzi wa utekelezaji wa malengo ya Wizara kwa Idara moja moja hapo juu.

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

Taasisi ya Viwango Zanzibar – *ZBS*:

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Viwango Zanzibar (*Zanzibar Bureau of Standards- ZBS*) katika kipindi cha mwaka 2013/2014, ilitekeleza malengo yake kama ifuatavyo:-

Kuandaa viwango vya bidhaa mbalimbali na kutoa elimu kwa wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Taasisi imefanya mambo yafuatayo:

- Kuunda Kamati 10 za kitaalamu kwa ajili ya kuzingatia mapendekezo ya viwango;
- Kuainisha viwango vya kipaumbele ambavyo ni bidhaa za vinywaji, vyakula, mafuta ya mimea na viungo, umeme na elektroniki, nishati na gesi, sabuni, vifaa vya ujenzi na mazingira;
- Kuzingatia na kupitisha jumla ya Viwango 25 za bidhaa; na
- Kutoa taaluma ya viwango na ubora wa bidhaa kupitia maonesho, vipindi vya redio na ziara kwa wazalishaji na wajasiriamali.

Kuandaa taratibu za upimaji na udhibiti ubora wa bidhaa.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Taasisi imeandaa Kanuni pamoja na taratibu zitakazotumika katika uandaaji wa viwango, ukaguzi, uthibiti wa ubora pamoja na upimaji wa bidhaa katika maabara. Aidha, hatua za uandaaji wa mfumo wa udhibiti na ukaguzi wa bidhaa kwa madhumuni ya kuimarisha ubora na usalama zinaendelea.

Kujenga mahusiano na Taasisi nyengine za viwango.

Mhe. Mwenyekiti, moja ya mambo ya msingi katika masuala ya viwango na ubora wa bidhaa ni kuwa na mahusiano na Taasisi nyengine za Viwango. Katika kutekeleza lengo hili, Taasisi ya Viwango Zanzibar imeanzisha mashirikiano ya kikazi na Shirika la Viwango Tanzania (*TBS*), pamoja na kuanzisha mahusiano mazuri na Taasisi nyengine za Afrika Mashariki kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kushirikiana.

Kujenga uwezo wa kitaalamu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi ya Viwango imeruhusiwa kuajiri wafanyakazi 11 ambapo hatua za uajiri zinaendelea kuchukuliwa. Aidha, wafanyakazi wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi yanayohusu uandaaji wa viwango, uthibiti wa ubora na upimaji. Aidha, kwa upande wa ushiriki wa mikutano, Taasisi imeshiriki katika mikutano mitano (5) ya Kimataifa inayohusu uandaaji wa viwango.

Kuendelea na matengenezo ya majengo.

Mhe. Mwenyekiti, katika Mradi wa kuimarisha Taasisi ya Viwango, Wizara imekamilisha hatua ya uandaji wa michoro na gharama kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi na Maabara unaotarajiwa kujengwa katika eneo la Maruhubi. Aidha, Taasisi imefanya matengenezo makubwa ya majengo ya Ofisi zilizopo Amani.

Mamlaka ya Vipimo na Kamisheni ya Ushindani.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya mamlaka hizi yameainishwa na yanatekelezwa chini ya Sheria za Mizani na Vipimo ya Mwaka 1983 na Sheria ya Kumlinda Mtumiaji ya mwaka 1995. Majukumu hayo yanajumuisha uhakiki wa vipimo, ukaguzi wa mizani, kusimamia mwenendo wa bei na ushindani wa kibiashara ambao kwa sasa yanatekelezwa chini ya Idara ya Biashara na Masoko.

Baraza la Biashara Zanzibar (*ZBC*):

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Biashara la Zanzibar lilitekeleza malengo iliyojipangia kama yafuatayo:-

a. Kuandaa Rasimu ya awali ya Sheria ya Baraza la Biashara ili kulipa nguvu za kisheria Baraza hilo katika kutekeleza majukumu yake;
b. Kuitisha vikao viwili (2) vya mashauriano kati ya sekta binafsi na sekta ya umma na viwili (2) vya Kamati Tendaji;
c. Kukamilisha matayarisho ya mkutano wa nane wa Baraza;
d. Kufuatilia utekelezaji wa maazimio na mapendekezo ya Baraza katika Sekta husika; na
e. Kuandaa mapendekezo ya uundwaji Kamati za Baraza ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*):

Uvunaji na usafirishaji Karafuu

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka fedha wa 2013/14, Shirika lilitarajia kununua jumla ya tani kati ya 4,000 na 4,200 za karafuu zenye thamani ya *TZS* 52.5 bilioni. Hadi kumalizika kwa msimu wa mwaka 2013/2014, jumla ya tani 5,352 zenye thamani ya *TZS* 75.0 bilioni ambazo ni sawa na ongezeko la asilimia 27.4 ya makadirio ya mwaka mzima zimenunuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, msimu mkubwa wa 2013/14 umekuwa na ongezeko la tani 499, sawa na asilimia 10.3 ukilinganishwa na msimu mkubwa wa mwaka 2011/2012 ambao ununuzi ulikuwa tani 4,853.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mauzo ya Karafuu, Shirika limeuza tani 4,997.6 za karafuu zenye thamani ya *US $* 54.9 milioni sawa na *TZS* 88.9 bilioni.

Bei ya kununulia karafuu:

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuanza kwa msimu wa karafuu wa mwaka 2013 -2014, Shirika limenunua karafuu kwa wakulima kwa viwango vifuatavyo**:-**

Daraja la	1	-	14,000
Daraja la	2	-	12,000
Daraja la	3	-	10,000

Mhe. Mwenyekiti, ununuzi wa karafuu kwa viwango hivyo, ulianza mwanzoni wa msimu hadi kufikia mwezi wa Februari, 2014. Katika mwezi wa Machi, 2014, Shirika lilipandisha viwango vya ununuzi ambavyo vilitumika mpaka mwisho wa mwezi wa April 2014. Viwango hivyo ni kama ifuatavyo:-

Daraja la	1	=	15,000
Daraja la	2	=	13,000
Daraja la	3	=	11,000

Mageuzi ya *ZSTC*:

Muundo wa Kitaasisi

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mageuzi ya Shirika, wafanyakazi 67 wamepunguzwa na kulipwa stahiki zao zenye thamani ya *TZS* 3.1 bilioni. Aidha, Shirika limeajiri wafanyakazi wengine wapya 42 wenye fani za masoko, biashara, uhasibu, sheria na ununuzi.

Kuimarisha Masoko

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uimarishaji masoko ya karafuu katika soko la ndani, soko la utalii na masoko ya Kikanda , Shirika limetekeleza hatua zifuatazo:

- Kuandaa ufungashaji kwa ujazo wa gramu 25, 50, 100, 250, 500, na 1000;
- Kufungua maduka matatu ya kuuzia karafuu katika ujazo mdogo; na
- Uuzaji wa karafuu tani 4 za ujazo mdogo katika masoko ya *UAE* na Saudi Arabia.

Mhe. Mwenyekiti, hatua hizo zilizochukuliwa zimeonesha kuwa na tija nzuri ya kibiashara. Kwa uuzaji huo mdogo mdogo katika soko la ndani jumla ya tani 0.5 za karafuu na mafuta ya mimea ziliweza kuuzwa kwa thamani ya *TZS* 20.0 milioni. Mauzo hayo ni makubwa ikilinganishwa na thamani ya uuzaji wa tani moja kwa utaratibu wetu wa kawaida.

Kuimarisha taratibu za ununuzi na huduma kwa wakulima wa karafuu

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa kuimarisha taratibu za ununuzi na huduma kwa wakulima wa karafuu, Shirika lilitekeleza mambo yafuatayo:

- Kufanya matengenezo ya vituo 14 vya ununuzi wa karafuu;
- Ununuzi wa magari saba (7) makubwa na magari matano (5) madogo;
- Kutoa mikopo ya *TZS* 349.2 milioni kwa wakulima 146 wa karafuu, ambapo jumla ya *TZS* 237.4 milioni zimerejeshwa sawa na asilimia 68 hadi mwezi April 2014; na
- Kulipia jumla ys *TZS* 150.0 milioni kwa ajili ya ununuzi wa miche ya mikarafuu kutoka kwa wakulima wenye vitalu binafsi.

Kuimarisha kiwanda cha makonyo

Mhe. Mwenyekiti, Shirika kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*) liliendesha utafiti wenye lengo la kubainisha mahitaji muhimu ya wataalamu, mitambo, malighafi, masoko, kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mafuta ya mimea wenye tija kwa kiwanda hicho. Mapendekezo ya utafiti huo yanaendelea kuzingatiwa na Shirika ikiwa ni pamoja na kuandaa mpango wa utekelezaji wake. Hata hivyo, katika hatua za awali za kuimarisha kiwanda hicho, Shirika lilitekeleza mambo yafuatayo:

- Kununua mashine mpya ya kupimia ubora wa mafuta ya mimea yanayozalishwa na kiwanda (*Gas Chromatography*);
- Kununua mashine ya uwekaji wa mafuta katika ujazo mdogo mdogo (*Semi - Automatic Filling Machine*); na
- Kuingia makubaliano ya awali ya kibiashara kati ya Kampuni ya *Land Co* ya Japan na *ZSTC*. Makubaliano hayo yanahusu uimarishaji wa bidhaa za mafuta ya mimea ili yaweze kuuzika katika soko la Japan.

MALENGO YA WIZARA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuelezea mapitio ya hali ya biashara, viwanda, utekelezaji wa bajeti na malengo ya wizara kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, sasa naomba kuelezea malengo ya Wizara kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyobainisha katika maelezo yangu ya utangulizi kuwa malengo ya Wizara kwa mwaka 2014/2015, yamewekwa kwa kuzingatia majukumu mahsusi ya utekelezaji wa Dira 2020, Mpango

Mkuu wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini (*MKUZA*), Mkakati wa Kusafirisha Bidhaa Nje (*NES*), Maagizo maalum ya Serikali kwa Wizara, Mpango Mkakati wa Wizara na maelekezo ya Serikali. Kadhalika, kutokana na uamuzi wa Serikali wa kuweka mkazo maalum wa kuendeleza sekta ya utalii yapo malengo ya mkakati huo yatakayotekelezwa na Wizara yangu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa kufafanua malengo ya Wizara kwa mwaka 2014/2015 yakihusisha ya utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha sekta ya utalii kwa kila Idara kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, majukumu makuu ya Idara hii ni kufanya tafiti kwa ajili ya kuendeleza sekta ya biashara na viwanda, kuandaa sera, mipango na mikakati ya wizara ili kuendeleza sekta hizo. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza malengo makhususi yafuatayo:

Uandaaji wa Sera ya Kumlinda Mtumiaji na Sera ya Maendeleo ya Viwanda

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kutayarisha mambo muhimu ya kitaalam katika uandaaji sera (kama vile dhana ya sera, hadidu rejea na ratiba ya utayarishaji);
b. Kuteua wataalamu kwa ajili ya maandalizi ya Sera na kusimamia utayarishaji wake;
c. Kuandaa Rasimu za sera zinazokusudiwa na kujadiliwa katika ngazi mbali mbali; na
d. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa sera.

Mapitio ya Sera ya Wafanyabiashara wadogo wadogo (*SMEs*)

Mhe. Mwenyekiti, Sera ya Maendeleo ya Wafanyabiashara wadogo wadogo ilitungwa mwaka 2006. Hivi sasa sera hiyo inahitaji kufanyiwa tathmini ili kupima mafanikio na matatizo ya utekelezaji wake. Katika kutekeleza lengo hili, Idara itafanya kazi zifuatazo:

a. Kuandaa hadidu rejea za mapitio ya utekelezaji sera iliyopo ili kubainisha mafanikio na matatizo yake; na
b. Kuandaa taarifa ya tathmini na kuandika kupendekeza sera mpya na pia kuandaa mpango wa utekelezaji wake.

Sheria ya Maendeleo ya Wafanyabiashara wadogo wadogo (*SMEs*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuendeleza ujasiriamali na wajasiriamali wenyewe na pia wafanyabiashara wadogo wadogo, Serikali inakusudia kuweka mfumo wa kisheria ili kusimamia maendeleo yao kwa utaratibu rasmi. Hivyo, kupitia Idara hii serikali itaandaa mapendekezo ya sheria itakayoshughulikia masuala ya maendeleo ya ujasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo.Kwa mwaka 2014/2015, Idara inakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kufanya maandalizi ya kitaalamu ya uandikaji wa Sheria inayokusudiwa pamoja na ratiba ya utekelezaji;
b. Kukusanya maoni ya wadau na kuandika Rasimu ya sheria; na
c. Kuwasilisha mapendekezo ya Sheria Serikalini na Baraza la Wawakilishi.

Kufanya utafiti wa bidhaa

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kukuza masoko ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini, Idara inakusudia kufanya tafiti za mazao ya nanasi na viazi vitamu. Utafiti huo utahusu kiwango cha uzalishaji na upatikanaji wa soko kwa bidhaa hizo. Katika kutekeleza lengo hili, Idara inakusudia kufanya kazi zifuatazo:

a. Kufanya maandalizi ya kitaalamu ya kufanya utafiti huo (dhana ya utafiti, hadidu rejea na mpango kazi wa utafiti huo);
b. Kukusanya takwimu za uzalishaji na masoko ya bidhaa hizo;
c. Kufanya uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa; na
d. Kuandaa taarifa ya utafiti na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa.

Uratibu wa Utekelezaji wa Mkakati wa Usafirishaji Bidhaa Nje (*National Export Strategy – NES)*

Mhe. Mwenyekiti, huu ni mkakati ulioanzishwa na serikali ili kuiwezesha Zanzibar kusafirisha bidhaa nje ya nchi na hivyo, kupunguza nakisi katika urari wa biashara. Katika utekelezaji wa mkakati huu, Wizara yangu inajukumu la kuratibu utekelezaji wake. Kwa mwaka huu wizara itaendelea na jukumu la kuratibu utekelezaji huo kwa kufanya kazi zifuatazo:

a. Kukusanya takwimu za utekelezaji za kisekta;
b. Kuratibu vikao vya kisekta kwa kila robo mwaka;
c. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Mkakati;
d. Kuwasilisha taarifa kwa sekta husika; na
e. Kuandaa taarifa za utekelezaji za robo mwaka, nusu na mwaka mzima.

Uandaaji wa Bajeti ya Wizara

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii inawajibu wa kufanya mapitio na kuandaa mapendekezo ya bajeti pamoja na taarifa za utekelezaji. Kwa mwaka ujao, Idara itaendelea na kazi zifuatazo:

a. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya 2015/2016;
b. Kuandaa malengo na vipaumbele vya bajeti mpya;
c. Kuandaa mchanganuo wa mapato na matumizi; na
d. Kutayarisha mapendekezo ya bajeti ya wizara.

Ushiriki wa Mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayohusiana na Sera, Sheria na taratibu za kibiashara

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara inakusudia kushiriki katika mikutano ya majadiliano ya Kikanda na Kimataifa kuhusiana na masuala ya kisera, sheria na mifumo ya kibiahara.

Kuratibu Shughuli za Kikosi Kazi

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kudhibiti magendo ya karafuu, Wizara inakusiadia kuendelea na uratibu wa shughuli za Kikosi Kazi kwa kufanya kazi zifuatazo:

a. Kuitisha vikao vya Kikosi Kazi (*Task force*);
b. Kuandaa mtandao wa ulinzi;
c. Kufuatilia uvunaji na ununuzi wa karafuu; na
d. Kuandaa taarifa za utekelezaji.

Utekelezaji wa Masuala Mtambuka (*Cross-Cutting Issues*)

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

a. Kuendelea kutoa elimu kwa wafanyakazi kuhusu masuala ya jinsia na maambukizi ya *HIV*, walemavu, na mazingira;
b. Kuhamasisha wafanyakazi kupima *HIV* kwa hiari ili kupunguza maambukizi mapya; na
c. Kushiriki mikutano na makongamano ya masuala ya UKIMWI, mazingira, athari za rushwa na jinsia.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha *TZS* 278.18 milioni kwa kazi za kawaida.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi, kuendeleza rasilimali watu, kutunza majengo ya Wizara na kutekeleza masuala yanayohusiana na utumishi. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imepangiwa kutekeleza malengo yafuatayo:

Kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi wafanyakazi 17

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuwajengea uwezo wafanyakazi na kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wa kazi, Wizara inakusudia kuwapatia mafunzo wafanyakazi 17 katika fani za biashara, uchumi, masoko, uhasibu, uwekaji wa kumbukumbu, ugavi na ununuzi, ukatibu muhtasi pamoja na kutilia mkazo mafunzo juu ya maadili ya utumishi. Katika kutekeleza lengo hili, Idara inatarajia kufanya kazi zifuatazo:

a. Kuendelea na utekelezaji wa mpango wa mafunzo wa Wizara;
b. Kuteuwa wafanyakazi 10 wa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 7 wa muda mfupi;
c. Kulipia ada za wanafunzi waliopo vyuoni na wapya; na
d. Kufuatilia maendeleo ya wafanyakazi waliopelekwa masomoni.

Kuajiri wafanyakazi wapya

Mhe. Mwenyekiti, ili kuongeza ufanisi wa kazi na tija, Idara inatarajia kufanya uajiri wa wafanyakazi 11 wa fani za mizani na vipimo, sheria, uchumi, biashara na ujasiriamali ambapo Idara itafanya mambo yafuatayo;

a) Kuandaa taratibu za uajiri;
b) Kutoa mafunzo ya awali kwa waajiri wapya; na
c) Kuwapa majukumu yao mapya.

Ukarabati wa majengo matatu na matayarisho ya ujenzi wa ofisi kuu Pemba:

Mhe. Mwenyekiti, katika lengo la kuweka mazingira mazuri ya kufanyia kazi, Idara inakusudia kufanya ukarabati wa majengo yake matatu, pamoja na kutayarisha michoro ya ujenzi ya Ofisi kuu ya Pemba. Katika kufanikisha lengo hili, Idara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

a) Kuandaa makisio ya awali ya gharama za ujenzi;
b) Kuandaa na kutangaza zabuni;
c) Kuteua wakandarasi;
d) Kufanya ukarabati wa majengo mawili ya Ofisi na ghala; na
e) Kutayarisha michoro na gharama kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Wizara Pemba.

Uandaaji wa Mpango wa Manunuzi wa mwaka

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuweka utaratibu mzuri wa matumizi ya rasilimali fedha, Idara itaandaa mpango wa manunuzi kwa mwaka 2014/2015. Katika kutekeleza lengo hili, Idara itaainisha mahitaji ya manunuzi ya vifaa vya Ofisi na huduma na kutekeleza mpango huo kwa mujibu wa sheria ya manunuzi.

Uanzishwaji wa maktaba, uandaaji na utoaji wa taarifa za sekta ya biashara na viwanda

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara inakusudia kufanya kazi zifuatazo:

a) Kuandaa Ofisi ya maktaba ili kuhifadhi nyaraka mbali mbali;
b) Kuandaa vipindi 20 vya redio na 10 vya *TV*. na vijarida vinne, vinavyohusu masuala ya biashara na viwanda; na
c) Kuhifadhi taarifa na utoaji wa huduma za maktaba.

Uratibu wa safari za Viongozi wa Wizara katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuendeleza ushiriki wa Zanzibar katika majadiliano yanayohusu biashara, viwanda na masoko ya bidhaa, Idara itaratibu safari kwa kufuatilia ratiba za mikutano ya majadiliano na kuandaa safari za viongozi wa Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha matumizi ya *TZS* 1,283.32 milioni kwa kazi za kawaida.

IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko inajukumu la kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara, kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji, kukuza na kuendeleza masoko ya bidhaa na huduma, kufanya ukaguzi wa bei na bidhaa na kukusanya mapato ya Wizara. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

Ukaguzi wa mizani 3500, vituo vya mafuta 50, matangi ya mafuta 36 magari ya mafuta 20 na viwanda 10 kwa bidhaa zilizofungashwa na mita 12.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuangalia usahihi wa vipimo, Idara imepanga kufanya ukaguzi wa vipimo hivyo kwa kutekeleza kazi zifuatazo:

a) Kukamilisha mapitio ya Kanuni za vipimo;
b) Kuandaa mpango kazi wa ukaguzi; na
c) Kufanya ukaguzi wa vipimo husika.

Ukaguzi wa maduka 3800, maghala 300 bekari 200 na *supermarket* 6.

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kusimamia mwenendo wa biashara na kumlinda mtumiaji, Idara inafanya ukaguzi wa bidhaa ili kubaini ubora wake pamoja na bei za bidhaa hizo. Katika kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kufanya kazi zifuatazo:

a) Kuandaa utaratibu na mpango kazi wa ukaguzi wa vipimo;
b) Kufanya ukaguzi wa maduka kwa bidhaa zilizopitwa na wakati;
c) Kufuatilia bei za bidhaa; na
d) Kuangamiza bidhaa zitakazogundulika kuwa zimepitwa na wakati.

Kutoa elimu na uelewa kwa jamii kuhusu Sheria Mpya ya Biashara ya mwaka 2013, masuala ya Vipimo na Kumlinda Mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kutoa uelewa kwa jamii juu masuala mbali mbali yanayohusu biashara. Kwa mwaka 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

a) Kuandaa Mpango wa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya Sheria za Biashara;
b) Kutayarisha vipindi vya redio na televisheni;
c) Kuandaa vijarida vya ufafanuzi wa Sheria hizo na masuala ya biashara; na
d) Kuandaa mikutano na taasisi zinazohusika na masuala ya biashara.

i. Tamasha la Biashara:

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuhamasisha biashara na kuwakutanisha wanunuzi na wauzaji bila ya kuwepo mtu wa kati, Idara imepanga kuandaa tamasha moja la biashara. Katika kutekeleza lengo hilo kwa mwaka 2014/15, Idara inakusudia;

a)Kufanya ununuzi wa maturubali na samani maalum (*Pre-fabricated*) ya kuweka mabanda ya tamasha na pia kuimarisha mazingira ya uwanja wa maonesho. b)Kuandaa uwanja wa maonesho kwa kuweka miundombinu muhimu; na
c)Kutoa matangazo ya kualika washiriki wa Maonesho.

ii. Kuandaa maonesho ya Biashara ya ndani na misafara ya kibiashara:

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia suala zima la ukuaji wa masoko ya bidhaa za ndani na kuitangaza Zanzibar kibiashara, Idara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:

a) Kutoa matangazo na uwelewa juu maonesho hayo na vigezo vya ushiriki;
b) Kuteuwa washiriki (waoneshaji);
c) Kufanya uhakiki wa bidhaa zinazooneshwa;

d) Kuratibu ushiriki wenyewe; na
e) Kuandaa ushiriki wa wafanyabiashara katika maonesho ya Jua Kali, maonesho ya Syria, *Eid-el-haji*, Sabasaba na misafara ya kibiashara.

iii. Kuandaa ushiriki wa Zanzibar *Expo Milan*:

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwezi Mei mwaka 2015, kutakuwepo maonesho makubwa ya bidhaa za viungo yatakayofanyika nchini Italia katika mji wa Milan (*Expo Milan*). Zanzibar inakusudia kushiriki katika maonesho hayo na kwamba hivi sasa wizara inaratibu ushiriki huo wa Zanzibar.Katika kutekeleza lengo hili, Idara inakusudia kuandaa "*Documentary*" ya mazao ya viungo (*spices*) na kuratibu ushiriki wa wafanyabiashara.

iv. Kurasimisha wafanyabiashara wadogo wadogo:

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kutekeleza jukumu la kurasimisha biashara na mali za wafanyabiashara wadogo wadogo, Idara imepanga kutekeleza kazi zifuatazo kwa mwaka 2014/2015:

a) Kufanya utambuzi wa wafanyabiashara ndogo ndogo 1000 katika Wilaya ya Kusini Unguja na Mkoani – Pemba;
b) Kutoa mafunzo kwa wafanyabiashara waliotambuliwa; na
c) Kufanya usajili kwa wafanyabiashara.

v. Kuhamasisha matumizi ya Alama za Mistari (*Barcodes*) kwa makampuni na wazalishaji:

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya Alama za mistari kwa bidhaa, Idara imepanga kufanya kazi zifuatazo:

a) Kuainisha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar kwa ajli ya alama za mistari;
b) Kuhamasisha wafanyabiashara juu ya matumizi ya alama za mistari na umuhimu wake katika kukuza biashara; na
c) Kuwasajili wajasiriamali 50 kutumia nembo za mistari.

vi. Kukusanya ada ya *TZS* 100.0 milioni:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, Wizara imepangiwa kukusanya ada ya *TZS* 100.0 milioni zitakazotokana na kazi za ukaguzi wa mizani na vipimo, vituo vya mafuta, ukaguzi wa magari ya mafuta na bidhaa zilizofungashwa katika viwanda(*pre-packed goods*).

vii. Kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato:

Mhe. Mwenyekiti, hapo awali nililiarifu Baraza lako tukufu kuhusu kuanzishwa kwa Mkakati maalum wa kuimarisha sekta ya utalii nchini. Ili kuweza kutekeleza mkakati huo, serikali imezingatia haja ya kuimarisha mazingira ya ufanyaji biashara na mapato ya serikali. Miongoni mwa maeneo yaliyopewa umbele katika utekelezaji wa mkakati huo ni kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya serikali. Moja wapo ya njia za kuimarisha ukusanyaji huo ni kuanzisha mfumo wa utoaji risiti za biashara kwa kutumia vifaa vya ki-elektroniki (*Electronic Fiscal Devices –EFDs).* Jukumu la uwekaji wa mfumo huo limepewa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara imepanga kutekeleza lengo hili kwa kufanya mambo yafuatayo:

i) Kuanzisha mfumo wa kisasa wa utoaji risiti za mauzo ya bidhaa na huduma katika maduka;
ii) Kusajili wafanyabiashara 700 watakaoanza na utaratibu huo;
iii) Kutoa elimu kwa wafanyabiashara na wananchi kuhusu mfumo huo utakavyoendeshwa na kusimamiwa; na
iv) Kununua na kusambaza mashine zinazohusika kwa wafanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko iweze kutekeleza malengo yaliyopangwa, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe *TZS* 327.64 milioni kwa kazi za kawaida kwa mwaka 2014/2015,

IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UKUZAJI UJASIRIAMALI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Viwanda inajukumu la kusimamia sera za kukuza maendeleo ya viwanda, ujasiriamali na kufanya ukaguzi wa miradi ya viwanda na uzalishaji. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inakusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

i. Uandaaji wa miradi minane (8) ya viwanda inayoweza kuwekezwa:

Mhe. Mwenyekiti, kwa lengo la kuongeza uwekezaji katika sekta ya viwanda, Idara inakusudia kuandaa miradi minane ya uwekezaji katika sekta hiyo. Katika kutekeleza lengo hili, Idara inakusudia kutekeleza kazi zifuatazo:

a) Kupitia tafiti za viwanda zilizopo na kufanya uchambuzi wa taarifa mbali mbali za miradi ya viwanda;
b) Kuainisha miradi itakayoekezwa;
c) Kuandaa maandiko ya awali ya miradi mipya (*Project Profiles and Project write Ups);*na
d) Kuhamasisha wawekezaji katika miradi hiyo.

ii. Vivutio vya uwekezaji katika sekta ya viwanda:

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya viwanda, Idara inakusudia kufanya yafuatayo:

a) Kuandaa mapendekezo ya awali ya vivutio kwa mazingatio;
b) Kuanzisha mashauriano na taasisi husika; na
c) Kuandaa taratibu za usimamizi na utekelezaji wake.

iii. Programu ya vifungashio kwa wajasiriamali:

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kufanya kazi zifuatazo:

a) Kuainisha bidhaa zinazohitaji vifungashio;
b) Kuainisha vifungashio vinavyohitajika;
c) Kufanya ununuzi wa vifungashio; na
d) Kuandaa uratatibu wa utowaji wa vifungashio.

iv. Utafiti wa mchango wa sekta ya usarifu bidhaa (*manufacturing*) katika uchumi wa Zanzibar:

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kufanya kazi zifuatazo kwa mwaka 2014/15:

a) Kutayarisha masuala ya kitaalamu katika uendeshaji wa utafiti huo (dodoso, wakusanyaji taarifa, mafunzo na ratiba);
b) Kusimamia uendeshaji wa utafiti wenyewe;
c) Kufanya uchambuzi na tathmini ya taarifa zilizokusanywa;
d) Kufanya mapitio ya taarifa na uchambuzi; na
e) Kuandaa taarifa ya utafiti huo.

v. Ukaguzi wa miradi viwanda na wajasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni ya kutoa usaidizi na ushauri wa kitaalamu, Idara inakusudia kuendeleza na jukumu lake la ukaguzi wa miradi 120 kwa mwaka 2014/15. Katika kutekeleza lengo hili, Idara itafanya yafuatayo:

a) Kufanya utambuzi wa miradi ya viwanda na wajasiriamali 80 Unguja na 40 Pemba itakayokaguliwa;
b) Kuandaa mpango kazi wa ukaguzi;
c) Kufanya ukaguzi wa miradi iliyotambuliwa; na

d) Kuandaa ripoti ya ukaguzi huo.

vi. Usajili wa miradi 120 mipya ya viwanda na wajasiriamali katika daftari *(Industrialdata base):*

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara inakusudia kuingiza katika daftari la usajili la viwanda, miradi 120 itakayokaguliwa. Vile vile, itaandaa utoaji wa Ripoti wa Utekelezaji wa Sera ya *SME*.

vii. Uandaaji wa ripoti ya utekelezaji wa Sera ya *SMEs*:

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kufanya yafuatayo:

a) Kuitisha vikao vya Kamati ya Ushauri kila robo mwaka;
b) Kufanya uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa;
c) Kukusanya taarifa za kila robo mwaka za utekelezaji wa sera; na
d) Kuandaa ripoti ya utekelezaji.

viii. Utoaji wa mafunzo kwa vikundi 17 na usaidizi wa vifaa kwa vikundi 3 vya wajasiriamali:

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kufanya kazi zifuatazo:

a) Kufanya ukaguzi wa vikundi vilivyoomba msaada;
b) Kufanya uchambuzi wa maombi kwa vikundi vilivyoomba msaada kulingana na vigezo vya usaidizi vilivyowekwa na Wizara; na
c) Kuandaa mafunzo kwa wajasiriamali.

ix. Ushiriki wa majadiliano ya Kikanda na Kimataifa yanayohusiana na maendeleo ya viwanda:

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara inakusudia kushiriki mikutano ya Kikanda (*SADC* na *EAC*) na Kimataifa kuhusiana na masuala ya maendeleo ya viwanda.

X. Undaaji wa Taarifa ya Ushindani wa Kiviwanda ya mwaka 2014 *(Industrial Competitiveness Report):*

Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili, Idara imepanga kufanya kazi zifuatazo:

a) kukusanya na kufanya uchambuzi wa taarifa;
b) Kuandaa ripoti ya ushindani; na
c) Kuwasilisha ripoti kwa wadau husika wa maendeleo ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali iweze kutekeleza malengo iliyojiwekea, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha *TZS* 245.04 milioni kwa kazi za kawaida.

OFISI KUU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO– PEMBA:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iliopo Pemba pia ina majukumu ya kusimamia shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba zikiwemo shughuli zote za utawala, kuimarisha mazingira ya kufanya biashara na viwanda kwa upande wa Pemba na kuratibu shughuli za wajasiriamali kisiwani humo. Malengo ya Ofisi ya Pemba ni kama yalivyoelezwa katika malendo ya Idara husika ambayo yatatekelezwa kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ili Ofisi ya Pemba iweze kutekeleza malengo yake, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe *TZS* 352.13 milioni kwa kazi za kawaida.

MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/2015, Wizara inakusudia kutekeleza miradi ifuatayo ambayo itasimamiwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na kutekelezwa na Taasisi husika:

a. Mkakati wa Kuendeleza zao la Karafuu:

- Kuandaa Sera ya Taifa ya Malibunifu na Mkakati wake;
- Kuandaa vigezo na uthibitishaji wa karafuu *(standards and certification);*
- Kuandaa Historia ya karafuu, kuhamasisha umuhimu na matumizi yake *(Inspriration book),* kutafiti sifa za upekee wa karafuu ya Zanzibar ili iweze kulindwa rasmi;
- Kutoa uelewa na mafunzo kuhusu umuhimu wa Tasnia ya Malibunifu kwa maendeleo ya biashara; na
- Kuandaa taratibu za uzinduzi wa *"branding*" kwa karafuu na mazao mengine ya viungo *(spices).*

b. Kujenga uwezo wa kukondoesha biashara Zanzibar:

- Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa Uwanja wa Maonesho ya Kibiashara ya Kimataifa kwa kutayarisha Mpango Mkuu wa Uwanja na kuandaa gharama za mradi.

c. Kuimarisha Taasisi ya Viwango *(ZBS):*

- Kufanya ununuzi wa vifaa vya maabara; na
- Kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya *ZBS* na maabara.

d. Programu ya Mazingira bora ya biashara:

- Kuanzisha sehemu moja ya usajili wa biashara;
- Kutoa elimu juu ya taratibu za uanzishaji biashara;
- Kuimarisha uratibu baina ya taasisi zinazohusiana na masuala ya uwekezaji;
- Kukamilisha utayarishaji wa Mpango wa matumizi ya ardhi;
- Kufanya mapitio ya Sera ya *SMEs* 2006;
- Kufanya mapitio ya Sera ya Uwekezaji ya 2005;
- Kuanzisha sera ya Ujarisiamali; na
- Kuandaa Sheria ya maendeleo ya *SMEs.*

Mhe. Mwenyekiti, ili iweze kutekeleza miradi hiyo kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha *TZS* 2,335.70 milioni kwa kazi za maendeleo.

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA

Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*):

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, Shirika limepanga pamoja na utekelezaji wa mpango wake wa mageuzi, kuendelea na utekelezaji wa shughuli zake za kawaida kama ifuatavyo:

a) Ununuzi wa karafuu kati ya tani 3,400 - 3,600 kwa *TZS* 54 bilioni;
b) Kuajiri wafanyakazi 13 wapya;
c) Kujenga vituo 7 vya ununuzi wa karafuu;
d) Ununuzi wa mezani 30 za kisasa;
e) Ununuzi wa magari makubwa 7 na magari madogo 5;
f) Kujenga eneo tengefu kwa ajili ya tasnia malibunifu ya karafuu hai na mazao mengine ya viungo *(Organic Spices);*
g) Kushiriki katika maonesho ya Kimataifa nchini Uturuki na China;
h) Upandaji wa mimea hekta 40 katika wa Shamba la Mtakata;
i) Ununuzi wa mitambo na ujenzi wa uzio wa Kiwanda cha Makonyo; na
j) Kufanya utafiti wa mchaichai ili kuimarisha uzalishaji;
k) Kufanya utafiti wa karafuu ya Zanzibar ili kubainisha vigezo vya upekee;
l) Uuzaji wa tani mbili (2) za karafuu katika ujazo mdogo kwa soko la ndani na tani kumi (10) katika soko la nje na;

m) Uanzishaji wa Kiwanda kidogo cha majaribio cha uzalishaji wa mafuta ya mimea.

Taasisi ya Viwango Zanzibar – ZBS:

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Viwango Zanzibar ina jukumu la kuandaa viwango na kuvisimamia pamoja na kudhibiti ubora wa bidhaa na huduma hapa Zanzibar. Kwa mwaka 2014/2015 Taasisi ya Viwango imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

a. Kuandaa viwango 80 vya bidhaa;
b. Kufanya ukaguzi *(Inspection)*, uthibiti *(Certification)* na Upimaji *(Testing)* wa bidhaa za vyakula na bidhaa nyenginezo;
c. Kununua wa vifaa vya maabara;
d. Kubadilishana uzoefu na utaalamu kwa kushirikiana na Taasisi za Viwango za Kikanda ;
e. Kutoa usaidizi kwa Wajasiriamali 50 ili kuzalisha bidhaa zenye ubora unaokubalika katika soko;
f. Utoaji wa mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 20;
g. Kuimarisha jengo la ofisi ya Amani; na
h. Kutoa elimu ya matumizi ya viwango na udhibiti wa ubora wa bidhaa kwa kuandaa semina nne (4) na vipindi vinane (8) vya redio.

Mhe. Mwenyekiti, ili Taasisi ya Viwango ya Zanzibar iweze kutekeleza shughuli zake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya TZS 600.0 milioni.

Mamlaka ya Vipimo na Kamisheni ya Ushindani:

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyoeleza hapo awali kuwa Wizara inaendelea na matayarisho ya Sera ya Kumlinda Mtumiaji, hivyo utungaji wa Sheria zitakazoanzisha vyombo hivyo utazingatiwa katika Sera zitakazotungwa.

Kwa kuwa Sheria za Mizani na Vipimo ya Mwaka 1983 na Sheria ya Kumlinda Mtumiaji ya mwaka 1995 bado zinaendelea kutumika, hivyo majukumu yanfuatayo yataendelea kutekelezwa chini ya Sheria hizo:-

i. Kufanya uhakiki wa vipimo;
ii. Kufanya Ununuzi wa vifaa vya mezani;
iii. Utoaji wa Mafunzo kwa wafanyakazi;
iv. Kufanya ukaguzi wa mezani katika maduka na kuhakikisha usahihi wake;
v. Kufanya ukaguzi wa vipimo vya mafuta na matenki ya mafuta;
vi. Kufanya tathmini ya uwekaji wa mezani za elektroniki katika masoko ili kujua idadi ya bidhaa zinazozalishwa;
vii. Kusimamia Ushindani na Kumlinda mtumiaji, Mwenendo wa Biashara na Mwenendo wa bei za bidhaa; na
viii. Kuangamiza bidhaa zilizomalizika muda na zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuwezesha utekelezaji wa masuala ya vipimo na ushindani kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya TZS 50.0 milioni kwa Taasisi ya Ushindani na TZS ruzuku ya 50.0 milioni kwa matumizi ya Taasisi ya Vipimo.

Baraza la Biashara la Zanzibar *(ZBC):*

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Biashara linajukumu la kuandaa jukwaa la majadiliano kwa lengo la kuimarisha mahusiano ya kibiashara kati sekta ya umma na sekta binafsi. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Baraza la Biashara la Zanzibar limepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

a) Utungaji wa Rasimu ya Sheria ya Baraza la Biashara
b) Uandaaji wa mikutano miwili ya Baraza la Biashara;
c) Uandaaji wa vikao vinane vya Kamati Tendaji ya Baraza la Biashara;
d) Uandaaji wa vikao 12 vya Kamati za Baraza la Biashara

Mhe. Mwenyekiti, ili Baraza la Biashara la Zanzibar liweze kutekeleza shughuli zake kwa mwaka huu wa fedha wa 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya TZS 242.3 milioni kwa ajili ya Baraza hilo.

Baraza la Usimamizi wa Utoaji wa Leseni za Biashara:

Mhe. Mwenyekiti, Hivi karibuni Baraza lako Tukufu limepitisha Sheria ya Usimamizi wa Mfumo wa Utoaji wa Leseni *(The Business Licensing Regulatory System Act, No. 13 of 2013).* Moja ya masharti ya Sheria hiyo ni kuanzisha Baraza litakalosimamia mfumo mzima wa utoaji leseni hapa Zanzibar.

Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara itachukua hatua za kuanzisha mamlaka zinazoelekezwa na sheria ili kushughulikia utekelezaji wa masharti ya sheria hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuwezesha uanzishaji wa chombo hicho, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe ruzuku ya TZS 100.0 milioni kwa ajili hiyo na utekelezaji wa mambo mengine yanayohusiana na sheria hiyo.

SHUKRANI:

Mhe. Mwenyekiti, mafanikio ya Wizara niliyoyaeleza katika hotuba yangu ni matokeo ya mashirikiano makubwa niliyoyapata kutoka kwa Wajumbe wa Baraza hili chini ya uongozi wako mahiri. Ninakushukuru wewe binafsi, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza na Wajumbe wote kwa ushauri na michango yao mliyotupa katika kipindi cha utekelezaji wa bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, Sina budi kukiri vile vile kuwa mafanikio ya kiutendaji yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2013/2014 ni matokeo ya ushirikiano mkubwa ambao Wizara yangu iliupata kutoka kwa wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi yetu. Kwa madhumuni ya kutambua mchango mkubwa wa Wadau hao kwa Wizara, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa nchi na taasisi za ndani na nje hususan zifuatazo:-

(i) Jamhuri ya Watu wa China;
(ii) India;
(iii) Serikali ya Marekani;
(iv) Shirika la Kimataifa la Kusimamia Malibunifu *(World Intellectual Property Organisation – WIPO);*
(v) Kituo cha Biashara cha Kimataifa *(International Trade Center – ITC)*
(vi) Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa *(UNDP);*
(vii) Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(UNIDO);*
(viii) Benki ya Dunia (World Bank);
(ix) Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara za Nje Tanzania – *(TanTrade)*
(x) Shirika la Biashara Duniani *(WTO);*
(xi) Sekretarieti ya Jumuiya ya Madola *(Commonwhealth Secretariat);*
(xii) Jumuiya za Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima za Zanzibar na Tanzania Bara;
(xiii) Baraza la Biashara la Tanzania *(TNBC);* na
(xiv) Wafanyabiashara wote wakubwa na wadogo na Wawekezaji wa Viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kwa mara nyengine tena kuwapongeza kwa dhati wafanyakazi wote wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa kazi kubwa yenye ufanisi mzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali. Ni matarajio yangu kwamba wataongeza juhudi zao ili kuzidisha ufanisi kwa kuwahudumia wananchi na kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya Hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawaombea dua njema katika kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii pia kuwashukuru wafanyabiashara wote wakubwa, wakati, wadogo, Juakali na wengine kwa juhudi zao kubwa za kuwahudumia wananchi kwa kuwapatia huduma bidhaa mbali mbali muhimu kama vile nguo, chakula, vyombo vya moto na vifaa vya ujenzi. Nawaomba waendelee kushirikiana na Wizara yangu kwa kufanya kazi pamoja kwa lengo la kuimarisha biashara na kutoa huduma bora kwa wananchi. Nawaomba wafanyabiashara wote kuwahurumia wananchi kwa kuwawekea bei nafuu ili wamudu maisha yao. Aidha, nawaomba wafanyabiashara waelekeze nguvu zao katika uwekezaji wa viwanda na biashara ya viungo *(spices)* kama vile mdalasini, manjano na viungo vyengine ili kunyanyua usafirishaji bidhaa na kuongeza thamani ya bidhaa zetu na biashara. Kadhalika, kwa kutambua mchango mkubwa kwa wawekezaji wa viwanda, naomba pia Mhe. Mwenyekiti, kuchukua nafasi hii kutoa pongezi za dhati kwa:

e. Bakhressa Group of Companies;
f. Kiwanda cha Sukari Mahonda;
g. ZATEPA

h. Allawys Supplies;
i. Zainab Bottlers;
j. Super Pure
k. Zan Bottling
l. Drop of Zanzibar
m. Zenji Sky Cola.

Mhe. Mwenyekiti, juhudi zao za kuimarisha viwanda nchini zinaweka njia kwa wafanyabiashara wengine kuwekeza katika uwekezaji wa viwanda. Aidha, napenda kuwashukuru.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba yangu hii haitokamilika kama sijatoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa Jimbo la Mtoni kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokua mbali nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili, nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya kipekee na ninaithamini sana.

MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015:

Mapato ya Serikali:

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Wizara imepanga kukusanya TZS 100.0 milioni kutokana na ada za huduma za ukaguzi wa mezani na vipimo.

Matumizi:

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi na ili Wizara yangu iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu sasa liidhinishe matumizi ya jumla ya TZS. 5,864.30 milioni. Kati ya fedha hizo TZS. 2,488.4 milioni kwa ajili ya kazi za kawaida, TZS. 2,335.0 milioni kwa kazi za maendeleo, na TZS. 1,042.3 milioni kwa ajili ya ruzuku kwa taasisi mbali mbali zilizo chini ya Wizara. Jadweli Nam. 6 hapa chini linafafanua zaidi maombi hayo ya matumizi ya Wizara.

Jadweli Nam 6:
Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko 2014-2015
(TZS. Milioni):

Vote Nam.	Idara	Kazi za Kawaida	Kazi za Maendeleo	Ruzuku
03:	Afisi Kuu Pemba	352.13	-	-
04:	Mipango, Sera na Utafiti	278.18	2,335.7	-
05:	Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali	245.04	-	-
06:	Biashara na uendelezaji Masoko	327.64	-	-
07:	Utumishi na Uendeshaji	1,283.32	-	-
	Baraza la Biashara	-	-	242.3
	Taasisi ya Ushindani	-	-	50.0
	Taasisi ya Viwango Zanzibar	-	-	600.0
	Taasisi ya Vipimo na mizani	-	-	50.0
	Baraza la Usimamizi wa Utoaji Leseni za Biashara			100.0
	Jumla ndogo:	**2,486.30**	**2,335.7**	**1042.3**
	Jumla Kuu:	**-**	**-**	**5,864.30**

II. HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa mara nyengine tena kukushukuru wewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako wote na wananchi wote kwa jumla kwa kunisikiliza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Kiambatisho Nam. 1

MALENGO YA MWAKA 2013/2014:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

i. **Kukuza ushindani wa kibiashara ili kuweka usawa na kuimarisha ustawi wa mtumiaji**

ii. **Kufanya utafiti wa Bidhaa na masoko:**

a. kuandaa tafiti tatu (3) za bidhaa zinazoweza kuongezewa thamani kwa ajili ya kusafirishwa;
b. kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Usafirishaji wa Bidhaa Nje (*NES*);
c. Kufuatilia makubaliano ya kibiashara yaliyofikiwa ya kitaifa,Kikanda na kimataifa;
d. Kufanya utafiti wa masoko kwa bidhaa zinazozalishwa Zanzibar; na
e. Kufanya utafiti wa uzalishaji, kuongeza thamani na masoko ya mwani.

iii. **Kuandaa Mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji malengo ya Wizara:**

a. Kutayarisha mfumo wa kisekta wa ufuatiliaji na tathmini ya malengo ya Wizara;
b. Kufanya mapitio ya Mpango Mkakati (Strategic Plan) wa Wizara;
c. Kutayarisha Bajeti ya Wizara; na
d. Kuratibu utekelezaji wa mageuzi ya Shirika la Biashara la Taifa.

iv. **Kuratibu utekelezaji wa Masuala Mtambuka:**

a. Kutoa mafunzo ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari;
b. kuzingatia masuala ya jinsia katika kupanga na kutekeleza Sera, Mikakati na Mipango mbalimbali ya kisekta; na
c. Kushirikiana na Idara ya Mazingira na wadau wengine kutekeleza mikakati inayohusu utunzaji wa mazingira pamoja na programu ya utekelezaji wa Sheria ya Mazingira.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

i. **Kuimarisha Rasilimali watu:**

a. Kusomesha wafanyakazi kumi (10) kwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi saba (7) kwa mafunzo ya muda mfupi.
b. Kufanya mapitio ya muundo wa utumishi na mfumo wa urithishaji madaraka (*Succession plan*) kwa madhumuni ya kuimarisha utaalamu na uendeshaji wa Wizara.

ii. **Kuimarisha vitengo vya Manunuzi, ukaguzi wa hesabu za ndani na Habari, Elimu na Mawasiliano:**

a. Kuimarisha vitengo vya Wizara, Idara itanunua vifaa vya mawasiliano, komputa na vifaa vyake; na
b. Kutoa mafunzo maalum kwa wataalamu wa vitengo hivyo.

iii. **Kukuza ushiriki wa Zanzibar katika majadiliano ya kibiashara ya Kimataifa:**

a. Kuratibu safari za kikazi za viongozi wa Wizara na watendaji wa Idara katika mikutano na majadiliano ya Kikanda na Kimataifa.

iv. **Kusimamia masuala ya utumishi na utawala kwa kuimarisha mazingira ya kazi.**

a. Kufanya matengenezo ya majengo yake yaliyopo Unguja na Pemba,
b. Kufanya manunuzi ya vifaa vya Ofisi na thamani, kulipia huduma muhimu za Wizara, na
c. Kuendelea kutunza mali za Wizara.

IDARA YA BIASHARA NA UKUZAJI MASOKO

i. **Kukuza ushindani wa kibiashara ili kuweka usawa na kuimarisha ustawi wa mtumiaji**

a. Kufanya ukaguzi wa mizani na vipimo vya mafuta;
b. ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa;
c. Kufanya utafiti wa kubainisha idadi ya maduka yaliopo Zanzibar; na
d. Kusimamia mwenendo wa bei za vyakula muhimu.

ii. **Kukuza biashara na masoko ya ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa**

a. Kuendelea Kuratibu na Kusimamia Ushiriki katika Maonesho ya biashara ya Kimataifa ya Sabasaba;
b. Kusimamia Ushiriki wa Maonesho ya Kikanda na Kimataifa;
c. Kuandaa Misafara ya Kibiashara (*Trade Missions*);
d. Kuandaa Misafara ya Kimafunzo kwa Wajasiriamali; na
e. Kuendelea na Uwekaji wa misingi ya kuendesha masoko ya Jumapili.

iii. **Kukuza ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya kibiashara ya Kimataifa.**

a. Kushiriki katika majadiliano ya Kikanda na Kimataifa; na
b. Kuendelea kushajihisha ushiriki wa sekta binafsi katika majadiliano ya Kikanda na Kimataifa.

iv. **Kurasimisha Biashara na mali za wafanyabiashara wadogo wadogo.**

a. Kuwatambua wafanyabiashara wadogo wadogo wapatao 1000 na kuwafanyia usajili.

IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UKUZAJI UJASIRIAMALI:

i. **Kukuza Maendeleo ya Viwanda:**

a. Kuendelea na matayarisho ya Sera ya Viwanda;
b. Kufanya utambuzi wa aina za viwanda vitakavyopewa umbele wa kuendelezwa;
c. Kufanya utafiti wa vivutio vinavyohitajika kwa uendelezaji wa miradi ya viwanda;
d. Kuanzisha kituo cha maendeleo ya viwanda; na
e. Kushauri mfumo wa uzalishaji wenye tija kwa baadhi ya viwanda (*Industrial upgrading*).

ii. **Kukuza ushiriki wa Zanzibar katika mikutano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa kuhusu Maendeleo ya Viwanda:**

a. Kushiriki katika majadiliano na mikutano ya Kikanda na kimataifa inayohusiana na maendeleo ya viwanda na ujasiriamali.

iii. **Kukuza Ujasiriamali:**

a. Kuandaa vigezo maalumu kwa ajili ya uteuzi wa vikundi/miradi ya wajasiriamali vitakavyopewa umbele wa kupatiwa usaidizi wa Wizara;
b. Kuanzisha mfuko maalum wa vifungashio kwa ajili ya wazalishaji wadogo wadogo;
c. Kufanya ukaguzi miradi 120 ya viwanda na miradi midogo midogo ili kutambua mafanikio na matatizo yao pamoja na kutoa ushauri;
d. Kuimarisha daftari la miradi midogo midogo ya wajasiriamali;
e. Kuratibu utekelezaji wa Sera ya *SMEs*;
f. Kuendesha mafunzo ya ubora wa bidhaa, usarifu wa mazao ya kilimo na ufungashaji; na
g. Kusaidia wajasiriamali katika uandaaji wa maandiko ya miradi.

OFISI KUU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO– PEMBA:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iliopo Pemba pia ina majukumu ya kusimamia shughuli za Wizara kwa upande wa Pemba zikiwemo shughuli zote za utawala, kuimarisha mazingira ya kufanya biashara kwa upande wa Pemba na kuratibu shughuli za wajasiriamali kisiwani humo.

TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA:

Taasisi ya Viwango Zanzibar – *ZBS*:

a. Kuandaa viwango vya bidhaa mbali mbali hatua kwa hatua na kutoa taaluma juu ya viwango na ubora wa bidhaa kwa wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa hapa nchini;
b. Kujenga mahusiano na taasisi nyengine za viwango nchini, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kutambulika na kubadilishana uzoefu katika utendaji;
c. Kujenga uwezo wa kitaalamu kwa kuajiri wafanyakazi wenye uwezo katika fani husika za kisayansi na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake yakiwemo ya muda mfupi na muda mrefu ndani na nje ya nchi;
d. kuendelea na matengenezo ya majengo; na
e. Kuandaa taratibu za upimaji bidhaa na udhibiti wa ubora wa bidhaa.

Mamlaka ya Vipimo ya Zanzibar na Kamisheni ya Ushindani ya Zanzibar:

a. Kufanya uhakiki wa vipimo;
b. Kufanya Ununuzi wa vifaa vya mezani;
c. Utoaji wa Mafunzo kwa wafanyakazi;
d. Kufanya ukaguzi wa mezani katika maduka na kuhakikisha usahihi wake;
e. Kufanya ukaguzi wa vipimo vya mafuta na matenki ya mafuta;
f. Kufanya tathmini ya uwekeji wa mezani za elektroniki katika masoko ili kujua idadi ya bidhaa zinazozalishwa;
g. Kusimamia Ushindani na Kumlinda mtumiaji, Mwenendo wa Biashara na Mwenendo wa bei za bidhaa; na
h. Kuangamiza bidhaa zilizomalizika muda na zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

Baraza la Biashara Zanzibar (*ZBC*):

a. Kuandaa mikutano miwili ya Baraza la Biashara la Zanzibar;
b. Kuandaa vikao 12 vya Kamati za Baraza;
c. Kuandaa vikao 8 vya Kamati Tendaji *ZBC*;
d. Kuandaa Rasimu ya sheria ya Baraza la Biashara la Zanzibar;
e. Kufanya Tathmini ya maendeleo ya Baraza kwa kipindi cha miaka mitano cha uhai wake;
f. Kuratibu, kusimamia na kufuatilia maazimio ya Baraza la Biashara mapendekezo ya Kamati za Baraza na Kamati Tendaji; na
g. Kuajiri wafanyakazi watatu.

Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*):

a. Kununua karafuu tani 4000-4200 kwa msimu wa mwaka 2013/2014 na kuandaa mikakati ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi huo;
b. Kuendelea na taratibu za kupunguza wafanyakazi kwa mujibu wa Sheria;
c. Kuendelea na uimarishaji wa biashara ya Karafuu katika soko la ndani, soko la utalii na masoko ya Kikanda; na
d. Kuimarisha ufungashaji wa bidhaa za karafuu, makonyo na viungo vyengine.Kiambatanisho Nam. 2.

MUUNDO WA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Mwenyekiti,Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeundwa na Idara nne, mashirika mawili, pamoja na Afisi Kuu – Pemba kama ifuatavyo:

- Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
- Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko;
- Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali;
- Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
- Afisi Kuu – Pemba;
- Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*);
- Taasisi ya Viwango ya Zanzibar; na
- Shirika la Biashara ya Magari (*MTC*).

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo, muundo huo unatarajiwa kubadilika kulingana na mapitio ya sheria zilizopo pamoja na kutekeleza sheria mpya iliyotungwa ambazo zitapelekea uanzishwaji wa taasisi mpya. Taasisi zinazotegemewa kuanzishwa ni:-

i) Kamisheni ya Ushindani;
ii) Taasisi ya Viwango ya Zanzibar; na
iii) Wakala wa Mizani na Vipimo Zanzibar.

MAJUKUMU YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO:

Wizara ina majukumu yafuatayo:-

- Kusimamia kuwepo kwa mazingira mazuri ya biashara;
- Kukuza mashirikiano kati ya sekta banafsi na sekta ya umma;
- Kusimamia kuwepo kwa ushindani halali wa kibiashara ili kumlinda mtumiaji;
- Kuwaimarisha na kuwaendeleza wafanyabiashara ndogo ndogo;
- Kusimamia ubora wa huduma na bidhaa zinazouzwa nchini;
- Kutafuta masoko ndani na nje ya nchi kwa bidhaa za Zanzibar;
- Kuendeleza Viwanda viliopo;
- Kuweka mazingira mazuri yatakayoshajihisha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda;
- Kuimarisha na kukuza viwanda vidogo vidogo;
- Kusimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini;
- Kuratibu na kusimamia shughuli za utafiti na sera zinazohusiana na uimarishaji na uendelezaji wa sekta za biashara na viwanda;
- Kuendeleza mashirikiano ya biashara kinchi, Kikanda na kimataifa; na
- Kuwaendeleza na kuwajengea mazingira mazuri wafanyakazi wa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO



HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA FEDHA, BIASHARA NA KILIMO KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu, kwa kutujalia uzima, siha na nguvu zilizoweza kutufikisha hapa leo za kuijadili Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko (Mhe. Nassor Ahmed Mazrui), Naibu Waziri wa Wizara hii (Mhe. Thuwayba Edington Kisasi), Katibu Mkuu (Ndg, Julian Raphael), pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada wanazozionesha wakati wa kutekeleza majukumu yao na kushirikiana na Kamati bega kwa bega katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii pindi wanapohitajika kufanya hivyo. Tunawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku, hiyo taarifa unayoisoma kuna watu wanaisikiliza ili waweze kuandika *Hansard*. Sasa ikiwa utakuwenda mbio kama hivyo, wale watu ambao wanaandika *Hansard* ndani kule watashindwa kuifanya kazi yao. Naomba uanze mwanzo na uende taratibu ili wale watu ndani weweze kufahamu wanachotakiwa kukifanya. Tuendelee Mhe. Jaku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehema na Mwenye Kurehemu, kwa kutujalia uzima, siha na nguvu zilizoweza kutufikisha hapa leo za kuijadili Bajeti ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, kwa dhati kabisa, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Aidha, napenda kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko (Mhe. Nassor Ahmed Mazrui), Naibu Waziri wa Wizara hii (Mhe. Thuwayba Edington Kisasi), Katibu Mkuu (Ndg, Julian Raphael), pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa jitihada wanazozionesha wakati wa kutekeleza majukumu yao na kushirikiana na Kamati bega kwa bega katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii pindi wanapohitajika kufanya hivyo. Tunawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na hayo sitakuwa ninatenda haki iwapo nitaendelea na hotuba hii bila ya kutoa shukurani za pekee kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, ambao tumeshirikiana kwa pamoja kuyapitia, kuyajadili na kuyachambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Naomba niwatambuwe Wajumbe na Makatibu hao kwa kuwataja kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin- Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija- Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Hamad Masoud Hamad- Mjumbe
4. Mhe. Viwe Khamis Abdalla- Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad- Mjumbe
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub- Mjumbe
7. Mhe. Asha Abdu Haji- Mjumbe
8. Ndg. Haji Khatib Haji- Katibu
9. Ndg. Fatma Omar Ali- Katibu

Mhe. Mwenyekiti, muhtasari wa mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko unaonesha kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara hii iliidhinishiwa jumla ya Tsh 4,990 millioni kwa ajili ya kazi za kawaida, kazi za maendeleo na ruzuku kwa Taasisi zake mbali mbali. Upatikanaji wa fedha kwa wizara hii ni wa wastani tu kwani fedha za matumizi ya kazi za kawaida zilikuwa ni asilimia 64.4, ruzuku ni aslimia 54.7 na fedha kwa ajili ya kazi za maendeleo ni asilimia 20.7 tu ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa ukusanyaji wa mapato, wizara iliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi 90 millioni ambapo hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, wizara imefanikiwa kukusanya shilingi 83.57 milioni sawa

na asilimia 92.86 ya makadirio hayo. Kamati inaona kuwa huo sio mwenendo mbaya wa makusanyo na hivyo tunaipongeza sana Wizara kwa makusanyo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa ufafanuzi na uchambuzi juu ya Idara na Taasisi moja moja ambazo zipo chini ya Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ina majukumu makubwa ya kufanya utafiti katika bidhaa mbali mbali zikiwemo zile zinazoweza kusafirishwa nje ya nchi na ndani ya nchi, pamoja na kufanya utafiti wa masoko ili kuweza kufikia malengo makuu ya wizara. Ni wazi kwamba utekelezaji mzuri wa majukumu ya wizara takribani asilimia 100% unategemea utafiti ulio bora na umakini katika utekelezaji wa kazi zake.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na wizara katika kufanya tafiti za uzalishaji na kuongeza thamani kwa bidhaa mbali mbali zinazozalishwa hapa nchini ikiwemo karafuu, Kamati inaona kuwa bado kuna haja kubwa kwa wizara kuongeza nguvu zaidi katika nyanja hiyo ya utafiti juu ya uzalishaji wa bidhaa na kuongeza thamani kwa bidhaa mbali mbali zinazozalishwa hapa nchini hususan katika mazao ya mwani, mdalasini, pilipili manga, pilipili hoho na hiliki ili kuinua zaidi kipato cha wazalishaji wetu wa ndani hususan wa mazao hayo ambacho kwa muda mrefu sasa kimekuwa duni.

Mhe. Mwenyekiti, taarifa za fedha katika matumizi ya wizara yoyote ni suala muhimu sana iwe matumizi hayo ni ya kazi za kawaida au matumizi ya kazi za maendeleo. Hata hivyo, wizara hii imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya kutofahamika kikamilifu kwa kiwango cha fedha kinachotolewa na Washirika wa Maendeleo katika kazi mbali mbali. Kamati inaona hii ni kasoro kubwa na hivyo, wizara inapaswa kuirekebisha kwa kuweka utaratibu mzuri utakaoiwezesha wizara kupata taarifa kikamilifu za matumizi ya fedha hizo kupitia Idara hii kwani ndiyo inayotakiwa kusimamia kazi za maendeleo ya wizara. Ikumbukwe kuwa Washirika wa Maendeleo wanafanyakazi kwa ajili ya serikali hii ambayo nayo inafanya kazi kwa ajili ya wananchi.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa malengo makuu ya Idara hii katika mwaka wa fedha 2013/2014 yalikuwa ni kuimarisha rasilimali watu kwa kusomesha wafanyakazi wa wizara mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa ajili ya kuimarisha utaalamu na uendeshaji wa wizara. Utekelezaji wa lengo hili unaonesha kuwa ni wafanyakazi saba (7) wamepelekwa masomoni kwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi saba (7) wengine wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na utekelezaji huo, bado taasisi nyingi zilizo chini ya wizara hii zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wataalamu wenye sifa hususan katika Idara ya Maendeleo ya Viwanda pamoja na Kitengo cha Mizani na Vipimo ambapo imekuwa ni vigumu kupata wataalamu wenye viwango vya elimu vinavyoanzia Shahada ya kwanza katika fani ya uhandisi (*Engineering*) ambao ndio hasa wanaohitajika katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona kuwa katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara ilijipangia kuajiri wafanyakazi mbali mbali ambapo wafanyakazi wa wizara, pamoja na taasisi zake ambapo hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, wakati Kamati ilipokuwa ikipitia bajeti ya wizara hii hakukuwa na uajiri wowote mpya uliofanyika. Hivyo, Kamati inaomba wizara na serikali kwa ujumla kuona umuhimu wa kuharakisha ajira za wataalamu, pamoja kufanya juhudi za ziada zitakazosaidia kupatikana kwa wataalamu muhimu wanaohitajika katika wizara hii na taasisi zake, vyenginevyo wizara itaendelea kukabiliana na changamoto mbali mbali zinazotokana na ukosefu wa wataalamu na hivyo, kudhorotesha juhudi za maendeleo katika wizara hii.

IDARA YA BIASHARA NA UENDELEZAJI MASOKO

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Biashara na Uendelezaji Masoko ina jukumu kuu la kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za biashara pamoja na kuzitafuatia masoko endelevu ya ndani na nje ya nchi bidhaa zote zinazozalishwa na kuitangaza nchi yetu ya Zanzibar katika masoko hayo. Vile vile, Miongoni mwa majukumu mengine yanayotekelezwa na Idara hii ni kuhakikisha uendeshaji wa biashara halali na kuimarisha ufuatiliaji wa ubora wa vipimo na mizani.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ndio eneo pekee linalotegemewa na wizara katika kukusanya mapato yake kupitia pamoja na mambo mengine utozaji wa ada za ukaguzi wa mizani na vipimo. Kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, eneo hili lilikadiriwa kukusanya shilingi 90 millioni ambapo kama ilivyoelezwa kuwa hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, jumla ya shilingi 83.57 milioni zimekusanywa, sawa na asilimia 92.86 ya makadirio. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, eneo hili linakadiriwa kukusanya mapato ya shilingi 100 milloni.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na umuhimu huo mkubwa wa Idara hii katika kuingizia mapato serikali, Idara hususan katika kitengo cha mizani na vipimo imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo za uhaba wa nyenzo za kufanyia kazi, uchache wa wakaguzi wa mizani na vipimo pamoja na changamoto ya teknolojia ya kisasa inayotumika katika mashine na vifaa mbali mbali vya kupimia vinavyohitaji kufanyiwa ukaguzi na watendaji wa Idara hii. Hivyo, Kamati inaomba wizara kuchukua juhudi zinazofaa ili kuweza kuzitatua changamoto hizo na kukipa uwezo mkubwa zaidi kitengo cha mizani na vipimo ili hatimae kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi utakaoiongezea mapato wizara hii na serikali kwa ujumla.

IDARA YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UKUZAJI UJASIRIAMALI

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali, ina majukumu ya kusimamia Sera ya Maendeleo ya Viwanda, Sera ya Ukuzaji Ujasiriamali pamoja na kuandaa na kusimamia mikakati ya maendeleo ya viwanda. Vile vile, Idara hii ina jukumu kubwa zaidi la kusimamia kazi za kituo cha Maendeleo ya Viwanda, kusaidia urasimishaji wa vikundi vya uzalishaji na kutoa usaidizi mbadala wa kiufundi na wa kifedha kwa miradi yote midogo midogo ya uzalishaji na ujasiriamali.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii ilikuwa na lengo la kuweka mazingira mazuri kwa wajasiriamali, viwanda na sera zake ambapo pamoja na mambo mengine ilijipangia kutekeleza kazi ya kuanzisha kituo cha maendeleo ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaendelea kusikitishwa sana kuona kuwa, hadi sasa serikali imeshindwa kuikabidhi Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko jengo la Saateni linalodhibitiwa na JKU na hivyo, kuifanya kazi iliyokusudiwa ya kuanzisha kituo cha kufundishia na kuwaendeleza wajasiriamali waliopo hapa nchini kushindwa kufanyika.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala la kutokabidhiwa kwa jengo la Saateni kwa wizara hii, ni jambo lililochukua muda mrefu, Kamati inaitaka serikali kutoa kauli juu ya mustakbali wa jengo hilo kwa wizara hii. Aidha, Kamati inataka kujua ni jambo gani lililopelekea kuwa hadi hii leo jengo hilo bado halijakadhiwa kwa wizara hii na bado linaendelea kudhibitiwa na JKU. Ikumbukwe kuwa jengo hilo linakusudiwa kuanzishwa kituo muhimu cha kuwafunza wajasiriamali wetu na hivyo, basi kushindwa kwa serikali kulikabidhi jengo hilo kwa wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko kunaweza kuchangia kuwadumaza wajasiriamali wetu na Sekta ya Viwanda hapa nchini, mambo ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu na watu wake.

KIWANDA CHA SUKARI, MAHONDA

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imeridhishwa na hatua kubwa ya kimaendeleo iliyofikiwa na kiwanda cha Sukari, Mahonda ambapo sasa Kiwanda hicho kimeanza kuzalisha sukari baada ya kusita kuzalisha bidhaa hiyo kwa miaka mingi sasa. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto kadhaa zinazokikabili Kiwanda hicho zikiwemo za kutokabidhiwa kwa uongozi wa Kiwanda hicho nyumba zisizopungua 150 za kiwanda hicho ambazo zimekuwa zikikaliwa na wananchi. Hadi sasa uongozi wa Kiwanda hicho umefanikiwa kuzipata nyumba 12 tu. Aidha, tatizo la uharibifu katika shamba la miwa unaosadikiwa kufanywa na wananchi wa maeneo hayo bado halijapatiwa ufumbuzi muafaka.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, Kamati inaiomba serikali kukabidhi nyumba zilizobakia za Kiwanda cha Sukari, Mahonda kwa uongozi wa Kiwanda hicho ili waweze kuzitumia kwa ajili ya wafanyakazi wake na kutimiza lengo lililokusudiwa la kujengwa kwa nyumba hizo kwani nyumba hizo zimejengwa kwa ajili ya wafanyakazi wa Kiwanda cha Sukari, Mahonda na wala sio vyenginevyo. Pia, Kamati inatoa wito kwa taasisi zinazohusika pamoja na wananchi kwa ujumla kutoa mashirikiano ya dhati kwa uongozi wa Kiwanda cha Sukari katika kudhibiti vitendo vya kukihujumu Kiwanda hicho vikiwemo uharibifu na wizi wa miwa kwa vile Kiwanda hicho kinatoa manufaa makubwa kwa wananchi ikiwemo upatikanaji wa ajira ambapo wananchi wazalendo wasiopungua 700 hufaidika na ajira hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati pia ilipata taarifa kuwa kuna eneo la shamba la kiwanda hicho lenye ukubwa wa ekari 42 ambalo limezuiliwa na KVZ, baada ya uongozi wa Kiwanda hicho kutaka kupanda miwa katika eneo

hilo ambalo lilielezwa kuwa ni la Kiwanda cha Sukari Mahonda. Pamoja na jitihada za uongozi wa kiwanda hicho kuonana na wahusika mbali mbali, bado eneo hilo limezuiliwa na KVZ. Hivyo, kamati inaiomba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kushirikiana na taasisi husika ili kulipatia ufumbuzi muafaka suala hilo la eneo husika.

TAASISI YA VIWANGO ZANZIBAR (*ZBS*)

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi ya Viwango Zanzibar imeanzishwa kwa Sheria Nam.1 ya mwaka 2011 ikiwa na majukumu mbali mbali yakiwemo kudhibiti na kuhakikisha ubora, pamoja na kutoa vyeti kwa bidhaa na huduma na kukuza uwekaji wa viwango hasa katika viwanda na biashara. Aidha, taasisi hii pia ina jukumu la kuanzisha, kulinda na kuzitambua maabara kwa ajili ya kuweka viwango na kuweza kudhibiti ubora, pamoja na kutoa, kuzuia na kufuta leseni za matumizi ya alama za viwango.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi hii ilikuwa na malengo kadhaa likiwemo lengo la kuandaa taratibu za upimaji bidhaa na udhibiti wa ubora wa bidhaa ambapo jumla ya shilingi 600 milioni ziliidhinishwa na Baraza lako tukufu kama ni ruzuku ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2014 asilimia 80 ya makadirio ilikuwa imeshaingizwa. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, ni asilimia 17.2 tu ya makadirio zilikuwa zimeshaingizwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na wizara hii ikiwemo matayarisho ya michoro kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi na maabara ili taasisi hii iweze kufanya kazi zake kama ilivyokusudiwa. Hata hivyo, Kamati inaiomba kwa dhati serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuiwezesha Taasisi ya Viwango Zanzibar ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hii itasaidia serikali yetu kuweza kusimamia vyema bidhaa za biashara kwa kuzingatia ubora wa bidhaa hizo, pamoja na kuimarisha mfumo wa ushindani wa biashara, pamoja na kuiwezesha sekta binafsi kwenda sambamba na masharti ya viwango vya kimataifa.

SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (*ZSTC*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Shirika la Biashara la Taifa lilikuwa na malengo mengi, pamoja na kuimarisha biashara ya karafuu katika soko la ndani, soko la utalii na masoko ya Kikanda, pamoja na kuimarisha ufungashaji wa bidhaa za karafuu, makonyo na viungo vyengine. Aidha, kwa mwaka huu wa fedha 2014/2015, Shirika hili limelenga pamoja na mambo mengine kununua karafuu kati ya tani 3,400 hadi 3,600.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imesikitishwa sana na kitendo cha baadhi ya wakulima waliokopeshwa fedha na shirika kwa ajili ya kuwasaidia katika shughuli za karafuu na hatimaye wakulima hao kushindwa kuzilipa fedha hizo. Lakusikitisha zaidi kuwa wakulima hao wameuza karafuu zao, lakini wameshindwa kulipa deni hilo. Taarifa zinaonesha kuwa jumla ya shilingi 545 miliioni zilikopeshwa kwa wakulima wa karafuu ambapo asilimia 70 ya deni hilo, ndilo lililokuwa limelipwa. Aidha, kwa mujibu wa utaratibu, deni hilo lilitakiwa kulipwa katika kipindi cha miezi mitatu. Hivyo, Kamati inalitaka shirika kujizatiti kikweli katika kutoa taaluma kwa wananchi juu ya taratibu za shirika hilo pamoja kuwasisitiza wakulima ambao hawajalipa deni hilo kurejesha fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na jitihada mbali mbali zinazofanywa na wizara, pamoja na taasisi husika katika kudhibiti magendo ya karafuu, magendo hayo ya karafuu yanaonekana kuwa bado ni changamoto na yanaathiri upatikanaji wa mapato ya serikali. Hivyo, Kamati inaisisitiza wizara na taasisi husika kuzidisha mashirikiano na wananchi ili kuweza kubaini mbinu mbali mbali mpya zinazotumiwa na wananchi wanaofanya vitendo hivyo haramu vya magendo ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo imeyakubali mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka wa fedha 2014/2015 na pia inawaomba Wajumbe wako waijadili na waichambue kwa kina,watoe mapendekezo yao na hatimae kuipitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa uvumilivu na ustahamilivu wao kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu mkubwa wakati wote wa uwasilishaji wa hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Baada ya hayo, sasa kama Mjumbe nataka kutumia dakika zangu na mimi za kuchangia bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Zanzibar imekuwa na utamaduni kwa muda mrefu wa kutoa msamaha wa kodi katika mwaka wa kipindi cha mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa bidhaa za mchele, unga wa ngano na sukari. Kwanza niipongeze kwa nia njema serikali kwa kuamua katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani ambacho tunakabiliana nacho, lakini naomba maelezo kwa nini bei ile katika soko la rejareja wakati tulitarajia iteremke utakuta hainufaishi mwananchi wa chini, kwa hapa nitahitaji maelezo ya Mhe. Waziri, ananufaika nani ni mnyonge au tajiri?

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba yakumbukwe manufaa ya wananchi na sio kwa misamaha ya kodi, naomba maelezo wafanyabiashara wangapi mwaka jana wamenufaika na misamaha hiyo katika mwezi wa Ramadhani na tani ngapi za mchele na unga wa nganu, pamoja na sukari ziliingizwa katika kipindi hicho. Pia, serikali ilikuwa haikusanye kodi ya kiwango gani katika misamahaa hiyo.Vile vile, inahakakikisha vipi bidhaa zinazopewa msamaha wa kodi zinatumika kwa wananchi…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Wajumbe huku ukiona wanakushangaa wanapiga piga meza, ni kwa sababu wamehisi unasoma, sasa hivi inatakiwa…

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hiyo hakuna tatizo, mimi najiamini kwa hili, sio kama nasoma.

Mhe. Mwenyekiti: Haya *Inshaallah* tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba kuongea eneo jengine kuhusu bidhaa zinazouzwa kwa fungu kama soda tatu kwa shilingi elfu moja (1000), wakati nembo zake hazionekani na soda hiyo ukiikuta dukani inauzwa shilingi elfu moja (1000) kwa kibati kimoja. Kwa hiyo, nitahitaji maelezo hapa, soda tatu kwa fungu la Machinga zinauzwa shilingi elfu tatu (3000) kwa vibati vitatu wakati soda ile dukani inauzwa shilingi elfu moja (1000). Pia, utakuta dawa za mbu hata haziuwi mbu, sasa hivi nembo tu zinachezewa na mbu wenyewe hafi. Kwa hiyo, hapa nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, nije katika eneo la manufaa kwa wananchi wake na taasisi ya kusimamia viwango vya ubora Zanzibar. Wananchi wetu vipato vyao ni vya chini na hii kuharibika kwa vyakula kunasababishwa na wataalamu wanasema ndio tunapata maradhi ya kiharusi kwa bidhaa hizi, hapa vile vile nitahitaji maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo, nije katika suala linalohusu bandari, hivi sasa meli zetu kwa muda mrefu zimekuwa zikifika Mangapwani na nyengine kufika Chumbe kushindwa kufika katika bandari ya Zanzibar kutokana na ufinyu wa bandari ile ilivyo. Tumepiga kelele sana suala lile, lakini naona Mhe. Waziri, kutokana na umakini wako unaweza ukalifikisha pahali ukalizungumza.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba wananchi wanateseka makontena yao sasa hivi yanafika kuwekwa Dar-es-salaam tunawajibika vipi, tunawafanyia haki wananchi hawa.Ushauri wangu kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama, mimi sioni tija yake kwa kweli, Dae-es-salaam wenzetu masaa 24 bandari ile inafanya kazi, kwa sababu gani?

Mhe. Mwenyekiti, leo ufinyu wetu ule tuutumie kwa wakati kufanya kazi masaa 24 bandari ya Zanzibar, lakini ukiwaambia watendaji sijui hawataki kufahamu au wanajua tunakwenda vipi tunavyokwenda, lakini imeshafika wakati bandari ya Zanzibar, hivi sasa kwa ushauri wangu mimi kama Jaku, imeshafika wakati itumie masaa 24 bandari ile, mtu kinachomfaa ni chake, tuangalie wenzetu wa China au Thailand wanalima mchele kwa ghorofa na zao linakuwa kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa bandari ile imekuwa chanzo kikubwa cha mgogoro vitendea kazi bandari ile hamna, makontena hayashushwi kwa wakati, mtu kinachomfaa ni chake. Mhe. Waziri, nikuombe sana hawa watendaji wa Wizara ya Miundombinu tumepigia kelele, lakini hatimae hakuna kinachofanyika. Kwa hiyo, nikushauri Mhe. Waziri, suala hili ulipeleke mbele, Wizara ya Miundombinu bado kuna urasimu mkubwa katika eneo la bandari vitendea kazi havipo, ushushaji wa makontena haupo, bandari yenyewe ikifika saa 12 imeshafungwa, hakuna ufanyaji wa kazi tofauti na wenzetu wa Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo, niunge mkono hoja hii, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe, ambaye umesoma taarifa hii kwa niaba ya Mwenyekiti, lakini kabla sijawakaribisha wachangiaji wengine, kuna tangazo hapa la Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko juu ya ugeni wake ambao umekuja kushirikiana nae katika bajeti hii ambayo ameiwasilisha muda sio mrefu. Wageni ambao wamekuja kwa niaba ya Mhe. Waziri ni; Mhe. Abdalla Abas Omar, Rais ya Jumuiya ya

Wafanyabiashara wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar, pia, amefuatana na ndugu Ali Aboud Makamu wa Rais wa Jumuiya ya Wafanyabiashara na mwisho kabisa wamekuja na mgeni wao anaitwa Attaf Sandrudin Giwan na yeye tunamuomba asimame. Huyu ni Meneja Mkuu wa *Petrol* Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Mohamed Mussa): Mhe. Mwenyekiti, huyu ni Meneja Mkuu wa Petroli Zanzibar. Baada ya maelezo hayo, sasa Mhe. Asha Bakari Makame, tuendelee.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku ya leo kuamka katika hali ya afya na uzima, lakini pia, nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii kuwa mchangiaji wa mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri na watendaji wake wote ambao walimsaidia katika kuandaa kitabu hiki mwanana ambacho kimeelezewa kwa kina na hakikuficha kitu ili kutupa fursa sisi Waheshimiwa Wawakilishi, kuweza kusaidia hapa na pale.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nitakuwa mwinzi wa fadhila kama sikumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa sababu wizara hii ni wizara nyeti na ni wizara ambayo inashughulikia shughuli mbali mbali zinazowagusa moja kwa moja jamii na wananchi wote kwa jumla. Nimpongeze Mhe. Rais jinsi alivyosimamia hasa zao la karafuu kuona kwamba zao hili ni zao ambalo ukiacha sasa hivi tunasema kwamba tunategemea utalii, lakini tukitaka tusitake zao hili ndilo lililoendesha Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar toka enzi mpaka tukaweza kufikia kiwango cha kuweza sasa kujitegemea kwa utalii.

Mhe. Mwenyekiti, nisimpongeze Mhe. Rais tu kwa upande wa karafuu, lakini nimpongeze jinsi anavyoshirikiana na wizara hii kwa sababu anaona ni wizara ambayo inamgusa kila mtu, lakini niseme kwamba tukiwa makini kwa kitabu hiki ambacho amekieleza Mhe. Waziri, basi kwa kweli niwaombe vijana ambao ndio tegemeo la leo na kesho kuwa tujitahidi kujiajiri wenyewe, kwa sababu ajira sio lazima uajiriwe na serikali, ajira ni kujitizama wewe mwenyewe ukoje na kuhakikisha kwamba umejifunza baadhi ya mambo ambayo yatakuwezesha wewe kukuletea maisha yako ya baadae.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo, niseme tu nimpongeze sana Mhe. Waziri, jinsi anavyoshirikiana na naibu wake, sisemi wengine hawashirikiani, lakini mimi ni mtu mchunguzi, nachunguza na nimeona Mhe. Waziri na Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kweli wana mashirikiano makubwa sana kiutendaji katika kazi na inatudhihirishia dhahiri jinsi Naibu Waziri anapoulizwa maswali na jinsi anavyojibu maswali yake, hii yote ni kuonesha kwamba yuko sambamba, si kwamba anakaa tu, anajitahidi na ufuatiliaji wa shughuli zote za wizara hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo, nije katika ukurasa wa 80 na 81. Ukurasa huu unaeleza kwa kuwa kutakuwa na matayarisho ya sera ya viwanda. Nimuombe sana Mhe. Waziri, kwamba kitu chochote kama huna mpango kwa sababu sera ni mpango unaambatana pamoja na sheria.Nimuombe sana Mhe Waziri, sera za nyuma zimeshapitwa na wakati na sasa hivi kwa kweli tuna mambo mengi ya utandawazi, namuomba Mhe. Waziri, ahakikishe kwamba sera hii anaisimamia ili kuipitisha kunakohusika na kuweza kutunga sheria ambazo zitaweza kutusaidia, lakini hapo hapo niseme kwamba ukurasa wa 81 unaeleza kukuza maendeleo ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, sote ni mashahidi tulikuwa na viwanda vyetu mbali mbali hapa Zanzibar ambapo viwanda hivi vilikuwa vinazalisha na sio kuzalisha tu, lakini hata ile thamani ya ule uzalishaji ulikuwa na matokeo mazuri. Tulikuwa na viwanda vya viatu, sigara, soda, viwanda ambavyo hasa cha viatu kilikuwa kinaitwa mwendo. Kiwanda cha Mwendo ni mwendo kweli, maana mguu utamalizika, lakini kiatu bado hakijamalizika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimuombe Mhe. Waziri, kama kuna mabadiliko ya kuhakikisha, tunataka kufungua viwanda japo vidogo vidogo, kwa kweli kuna haja sasa hivi ya kurudi tena katika ufunguaji wa viwanda, pamoja na kwamba nchi yetu ni ndogo, lakini kuna viwanda vidogo vidogo. Hivyo, tunaweza na hasa ninavyomjua Mhe. Waziri, kwamba yeye ni mtu ambaye ameshatembea nchi nyingi na anaelewa kitu gani viwanda, sio yale maviwanda makubwa. Sasa hivi kwa karne hii ya 21 kuna viwanda ambavyo tunaweza kuvifungua wala visichukue nafasi kubwa ya ardhi. Nimuombe Mhe. Waziri, alifuatilie hili ili tuweze na sisi kwenda sambamba na teknolojia ya sasa.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nizungumze la mwisho. Huko nyuma katika zao letu la karafuu tulikuwa na vifaa maalum ambavyo ni vya kuanikia karafuu, tulikuwa tuna majamvi, hata hivi sasa naona yapo, lakini kwa nini utamaduni huu umekufa? Kwa sababu majamvi yalikuwa yana haiba yake na ile karafuu yenyewe ni kwamba haiharibiki, lakini nitamuomba Mhe. Waziri, kupitia vyombo vyetu vya habari ikiwa ni televisheni au redio atoe

taaluma maalum kwa wananchi kwamba kwa kweli haiwezekani sasa hivi sisi tukaanika karafuu barabarani. Kwa sababu ukienda huko Pemba na ukija hapa Unguja karafuu kwa wingi utaziona kando kando ya barabara, tunauwa karafuu *graide* yake, nitamuomba Mhe. Waziri, atoe taaluma hiyo ili wananchi wetu waweze kuanika karafuu kwenye majamvi. Wananchi wetu wanaelewa, lakini sijui ni kitu gani ambacho kinawafanya sasa hivi zile karafuu kuzianika barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa nimuombe Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema atupe afya na uzima tuweze kufunga Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani ambao uko mbele yetu na niwaombe Waisilamu wenzangu na hasa wale wafanyabiashara. Kwa sababu wafanyabiashara wanaona kama mwezi huu ndio mwezi wa kuchuma, lakini mwezi huu ni mwezi wa toba. Sasa niwaombe sana wafanyabiashara tusifanye Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa kuchuma, tufanye Mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa toba na ni mwezi mtukufu. Kwa hivyo, niwaombe bei ziwe nafuu za vyakula ambavyo wanatumia Waisilamu wote kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Baada ya kusema hayo, tutakiane mema katika mwezi huu unaokuja wa Ramadhani na *Inshaallah* tuonane tena kwa salama na amani. *Amin. (Makofi)*

Mhe Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, nikupe kwanza shukurani zako za dhati, kabla sijaanza, nikushukuru sana na wewe asubuhi hii ya leo kuweza kunipa muda huu na kwa kuwa Wajumbe wetu wengi hawapo ningeomba unisaidie muda, ili niweze kupata muda mkubwa na kuweza kuchangia vizuri. Naomba hilo tuweke Kanuni kando unisaidia muda, unipatie dakika zangu 30 hakuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia kitabu hiki, kuna masikitiko makubwa sana nje, masikitiko haya kuhusu wafanyabiashara wetu kwa kuzuiliwa makontena yao Dar-es-Salaam na hata kupata ugumu wa kuyatolea mpaka ikabidi yapate *escort* kuja Zanzibar kwa kuweza kuja kupekuliwa. Kwa kweli hili suala ni zito na linatia unyonge, naomba Mhe. Waziri, kwa ninavyomuamini na katibu wake na watendaji suala hili leo au kesho atapokuja kutupa majibu anipe jibu kuwa kafanikisha na hizo fedha ambazo zinatakiwa tufanyiwe hesabu zirejeshwe Dar-es-Salaam zimebaki hapa hapa bila ya tatizo lolote. Naamini hivyo anaweza tena anaweza sana. Kwanza nianze kupeleka ujumbe, halafu tena niingie katika hicho kitabu chenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, alikuwa ni mfanyabiashara kwa miaka mingi sana ana *experience* nzuri sana, ndio maana Mhe. Rais wa Zanzibar akamuona hakubakisha wala hakumchagua usiku, kamchagua mchana na kwa kuona jina lake. Kwa sababu ukichagua usiku hata jina unaweza ukasahau badala ya kumwita Nassor Ahmed Mazrui, unaweza kumwita Makame Mshimba kwa kuwa umechagua usiku, lakini yeye kamchagua mchana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi katika ukurasa huu wa 75 hii ni Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kama sijakosea, ni wizara ambayo nusu ya roho ya Zanzibar kwa utendaji wake, leo shilingi bilioni tano na shilingi milioni mia nane haikidhi haja kwa wizara hii kupewa. Ni masikitiko makubwa sana, kwa mimi mtaalamu na nina cheti cha uchumi kinanisikitisha sana kuona leo wizara hii ambayo tulitegemea kutupatia kodi kubwa sana katika nchi hii, Wizara ya Fedha kuweza kumpa shilingi bilioni tano, tuangalie pesa hizo ni sawa sawa na kwenda kununua kiatu kwa Suma umemaliza kazi. Kwa kweli inasikitisha sana. Usinione hivi ninatoka machozi ya kuhurumia wizara hii kwa kupewa shilingi bilioni tano haikidhi haja.

Mhe. Mwenyekiti, mama yangu Bi Asha Bakari Makame, alisema hapa ndio vijana pa kuweza kujiajiri na kuanzisha viwanda vidogo vidogo. Mama Asha Bakari tusidanganyane, Mhe. Waziri, hana uwezo huo wa kufanya hivyo, kwa sababu pesa yake haikidhi haja kabisa kutokana na hali halisi. Nimesema baada ya siku tatu nilipata *short course* ya mafunzo ya kuja kuichambua jinsi gani wanapoanza kukaa kitako mawizara na wakapeleka bajeti zao katika Wizara ya Fedha na mpaka kutiliwa kila kitu chao, hiyo nimesema baadae nitakuja kuiona kutokana na hali halisi ilivyokuwa haikidhi haja. Sasa siku hiyo mtashangaa nimejua wapi mtakuja kuona.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa saba Mhe. Waziri, hapa amesema kuwa, mwenendo wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara kwa mwaka 2013 wameainisha ongezeko la usafiri. Nakubaliana na Mheshimiwa, lakini aendelee kufanya takwimu vizuri, biashara zinakwenda, lakini usumbufu upo mkubwa bado hatujabadilika.

Mhe. Mwenyekiti, katika waziri niseme Baraza hili wala sitaona haya, wala hajanilishia chochote na wala hatujuani; yeye CUF na mimi CCM, lakini kwa heshima yake lazima niseme Mhe. Waziri, ambaye yuko *straight* na sheria kutuletea Barazani ni yeye nambari *one*. Hili lazima niliseme, mtu haki yake mpeni, hata akivaa tai nzuri msifu kutokana na hali ya utekelezaji wa hali halisi, ulivyo. Mhe. Waziri hongera sana nilikuwa nikwambie kwa neno la Kiingereza lakini kidogo miwani yangu haitizami mbali, lakini hata hivyo, nakwambia *congratulation* ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea wafanyabiashara wetu wadogo wanasumbuliwa tu kule kwa biashara ndogo kama mafriji, wakati friji tushalipia hapa na yeye yule kanunua kwa mfanyabiashara mkubwa wa hapa, lakini kwa kuwa kapata *price* ya kuweza kuwa na yeye akapate tonge, basi bado anasumbuliwa, jamani naomba usilifumbie macho hili suala. Nakuomba usione tabu, wapo kina Mhe. Mbarouk Wadi Mussa wachukue pale bandarini wakakusaidie, maana tukisema hivyo, watu hawafahamu kwenda kusaidia, sio kutetea serikali au kutaka serikali ngapi kutetea biashara ziende. Mimi naomba watu watufahamu vile tunavyozungumza, naamini akienda Mhe. Mbarouk Wadi Mussa pale hakubali upuuzi huo, mimi naomba sana Mhe. Waziri, hiki unda tume yako ndogo wala usione tabu, wapeleke Waheshimiwa wakusaidie ili watu wetu waweze kunufaika na biashara hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 10 upandaji wa bei. Mimi inanisikitisha sana na niliwahi kusema siku moja bora wafanyakazi wasipandishiwe mishahara, lakini bei za biashara zishuke chini na kodi zipunguke, lakini serikali inaona ikipunguza kodi inakula hasara nikiwauliza hasara iko wapi hawaeleweki.Kwa sababu sioni kama inawekeza, sioni kama nao wananunua, sisi ndio tunawapangia humu sheria, tunakwenda kuwapa wao na wao ndio wanaowauzia wafanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nashangaa sana sheria tunazitunga sisi kwa nia nzuri baadae tunawapa wao na wao wanazitoa kwa kuwaelekeza wafanyabiashara, lakini kule hali halisi ilivyo mpaka sasa hivi hazisimamiwi kwa mujibu wa utaratibu ulivyo, kuna mambo tutumie siasa, nadhani na sheria ndani yake. Kwa sababu leo mtu unapomwambia bidhaa fulani tunakupunguzia bei, basi isimame ile ile, lakini wafanyabiashara hawa wanakuwa mara mbili zaidi, wewe ushampunguzia bei anakwenda kuongeza zaidi, haileti tija kwa wafanyabiashara na hasa huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhani Mhe. Waziri, hamaki sana nataka nikwambie hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu hapa ndipo watu wanapofanya mambo, watu tunatakiwa tusali sio kwenda kuuza biashara nyingi, hapa ndipo tunapotakiwa tuchume kwa kusali na kukesha misikitini, lakini wafanyabiashara hapa ndipo wanapofanya biashara za kuchuma tunakwenda wapi. Mhe. Waziri, namuomba sana asimamie awatizamie na *price* ya kodi ili Mwezi huu Mtukufu watu wafunge vizuri, masikini waweze kumiliki na wao.

Mhe. Mwenyekiti, inatia aibu ndugu zetu wa kimasikini wanashindwa kununua njugu mawe, wanashindwa kununua matunda kwa sababu uwezo wao ni mdogo. Sasa kwa kuwa nimemuamini nataka nione wala asione tabu kutembea madukani mara kwa mara, atembee achukue wanasheria wake anayeleta ubishi afunge biashara, hakuna tatizo, wako wengine wataleta na wako wengine wanazaliwa watakuja na biashara, namuomba hilo wala asizubae kabisa wa kufumbia macho hakuna kumuogopa mtu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika hali ya viwanda vyetu. Mhe. Waziri, aliwasifu sana wafanyabiashara na alimtaja Said Salim Bakhresa, Kiwanda cha Sukari, aliwataja na watu wa *Zanzibar Bottlers* na watu wengine, hizo ndizo sifa, ungekuwa wewe mlango umeufunga, basi usingewapata hawa, lakini sifa moja uliyoipata ya kuwa njooni, hukujali Katiba wala Kanuni, ila umejali maslahi ya Wazanzibari kupata ajira. Sasa ajira hii isimamiwe wapate wale wale Wazanzibari, sio *foreigners*, tumechoka na *foreigners,* sasa hivi ukweli tuseme, *foreigners* mkubali aliyekuwa na jipya kuja kutuletea hapa Zanzibar, huyo akubaliane nae sina tatizo. Lakini sio *foreigner* anakuja kufanya akaunti. Hawa watoto waliosoma hapa Chuo cha Chwaka kule wana kazi gani. Mhe. Waziri hili nakuomba sana usikubali kitu kama hicho. Tumechoka na *foreigner* bwana, wanachukua kazi za Wazanzibari maskini ya Mungu wana uwezo nazo. Halafu la pili wanawaambia Wazanzibari ukiwaweka wezi! Sio wezi kwa sababu wewe humlipi kama yule *foreigner,* utamkandamiza kwa kuwa Mzanzibari asikuibie, atakuibia tu. Lakini wewe mlipe sawasawa na yule ambae mwenye cheti kama kile, hapo ndio utakuwa na usahihi. Tusiwasingizie tu Wazanzibari wakipewa nafasi wanakimbilia kuiba, mazingira mnayowafanyia sivyo na kweli haki yao mnawaonea.

Leo unamtoa mtu nje gari unamlipia wewe, maji unamlipia wewe, ndugu yako wa hapa hapa unashindwa kumtengenezea mazingira mazuri, halafu unasema wanakuibieni hapana tusiwe na utashi huo. Hao *foreigners* wengine wezi. Mimi nawajua wengi wameshawaibia watu wamebakia wanakwenda zao na mapesa chungu nzima. Wewe unacheka kwa kuwa nini kakuibia *foreigner*, lakini Mzanzibari unachukia. Tunafanya nini Mhe. Mwenyekiti, tunasema wazawa sasa hivi mimi nimeshika bango nipo *serious* na suala hili, sikubaliani hata kidogo na nitahakikisha katika kipindi changu cha lala salama hichi nione Wazanzibari wangapi sasa hivi wamekamata zile *post* za *foreigner*. Hiki kitu mimi sikubaliani nacho. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana viwanda hivi tunavikubali asilimia 99, mimi sina tatizo navyo.

Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru Kamati Mwenyekiti ameeleza suala la Kiwanda cha Sukari. Ni kweli tunawafuja, tunawaharibia tatizo, lakini tuwape elimu sasa hivi wananchi wetu. Tatizo kubwa linakuja kutokana

na kukosa mabonde ya ukulima. Waziri kutana na Waziri mwenzako wa Kilimo na Maliasili, washajiisheni wale wananchi watafutieni mabonde mengine ya kulima. Lakini tuna tabia ya kuwa tunawafukuza wananchi sehemu ya kujipatia kula hatuwapi sehemu nyengine na hili ndio tatizo.

Wazanzibari ni watu wasikivu, ni watu laini wanaelewa, lakini wewe unamuudhi kwa makusudi kutokumpa *position* nyengine. Mhe. Waziri fanya hili kwa makusudi kwa sababu tatizo kule la Kiwanda cha Sukari wananchi kuchoma miwa, wananchi kuvuruga na kuvuruga sababu yao tumewatelekeza hatukuwaita tukawapanga sehemu nyengine, kwa kutafuta *income* yao na wao kwa njia ya kulima. Wazanzibari ni watu karimu, mimi nafikiri mkenda mkawaweka chini wale, au mkawa-*organize* mkawaingiza kwenye viwanda fitna imekwisha. Nasema imekwisha kwa sababu wanatafuta nini kuganga njaa.

Sasa mkiwaita humo mimi nafikiri itakuwa ni suala la busara. Tuwaelezee wananchi wasifanye uharibifu, ile ni mali yao. Nawaomba sana wananchi wangu wa maeneo yale wote wa ukanda na nawasihi sana. Hata sasa hivi ukija Pangeni, Upenja wameacha yale mabonde kwa kutaka iendelezwe kupandwa miwa kwa wingi na hakuna hitilafu mpaka sasa hivi na *inshaallah* Mwenyezi Mungu ajaalie wasichome miwa wala wasivune kiholela. Hizo nyumba wengine kuna maskini muangalie. Wale waliokuwa hali duni nawaomba sana waachieni, kuna wale wengine wameziweka nyumba kwa mambo ya ufuska tu wanyang'anyeni, hata kama kuna mkubwa mnyang'anyeni msimuache. Lakini hawa watu waliokuwa maskini ya Mungu ninaomba sana wale wapeni *tahfif* ili kuweza kuwasaidia waendeshe maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, kiwanda cha maziwa cha Bakhressa nasikia tayari kimeanza kazi. Nashukuru sana mpaka sasa hivi asilimia kubwa ya Wazanzibari wanaelekea huko kuweza kupata kazi. Ninaomba Mhe. Waziri uhakikishe hilo tunamshukuru sana mwekezaji huyo.

Pia kuna wengine *J. K. Enterprise* karibu na wao wataweka chelezo cha kutengeneza maboti na tunatarajia Wazanzibari 300 kuweza kufanya kazi pale Mangapwani, hivi karibuni tu na wao wataanza kuwaajiri watu. Hivi ndivo tunavyotaka ili kuweza kutusaidia kuwapatia ajira Wazanzibari. Mhe. Mwenyekiti, baada ya miaka michache kwa kusimamia kazi vizuri hapa tutakuwa Wazanzibari *Alhamdulillah* kila mtu ana *pocket money* wakati wote. Sio sasa hivi Wazanzibari nusu ndio wenye fedha.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Kiwanda cha *Coca-Cola* hebu Mhe. Waziri anifafanulie kuna maneno mengi hapa. Unajua mimi sijapata *in deep* na wala sitaki nieleweke ku-*crush* sana hapa, isipokuwa naomba hebu aniambie hapa vipi. Wengine wanasema kimefungwa kwa utashi tu kuwa kuna mtu amekinunua kiujanja apate kuuza soda zake. Kuna wengine wanasema kuwa wanasingizia soko la Zanzibar sasa hivi hakuna. Naomba sana Mhe. Waziri hili suala uje kunisaidia kwa kina kabisa. Uje kunieleza sababu gani ambazo mpaka sasa hivi kiwanda hiki cha Zanzibar hakifanyi kazi; kinafanya kazi kiujanja ujanja. Wewe utaona *crate* tele zinaletwa lakini kumbe zile zinaletwa kwa njia iliyokuwa si nzuri; haileti neema.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji wa Rasilimali. Mhe. Mwenyekiti, kuna kipindi fulani kulikuwa kuna mradi wa Wachina. Hapa mimi naomba sana nimshukuru Mhe.Waziri kaangalia vizuri viwanda vidogo vidogo kama wale watu wa pale Gulioni. Mhe. Mwenyekiti, hebu wale vijana twende tukawape vifaa kazi *model* ya kisasa, vipo vitu vya kutengenezea vinavyotumia *energy power*.

Mashine zile zipo India na sehemu nyengine. Hebu twende Mhe. Waziri tukawa-*organize*, kwa kweli ni watu ambao wanastahili sifa, wanastahili kupewa vianzio kwa sababu wameji-*organize* wenyewe bila ya Serikali kutia mkono wake. Kama imetia mkono wake utanieleza, kama hakuna mkono naomba Mhe. Waziri nenda kwa makusudi tuwaelekeze wale vijana wanatumia nguvu kazi za nyundo. Lakini tuwarahisishie mashine zipo za kukata, za kunyoosha, za kutoa umbile la kile kitu unachokitaka. Naomba sana Mhe. Waziri tuwapelekee pale wafadhili, ili waweze kusaidia kwa wakati huu tuliokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika hili Shirika la Biashara la Taifa *(ZSTC).* Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba tuwe na sheria. Sasa hivi watu wetu wengi sana wanaanguka kwenye mikarafuu. Wewe ukusanyiwe bilioni tano huna uwezo wa kuweza kuwalipa. Kwa kungoja Serikalini pesa zilipwe tunakawia sana. Hebu tafuta sheria, sheria hiyo waweze kupata bima anapoanguka mtu aweze kumlipa bima. Mhe. Mwenyekiti, hapo tutapata kazi nzuri, hawatojirusha kwa makusudi watu lakini itakuwa angalau anajua mimi nakifuata kikonyo kilipo nikianguka bima ipo kwa mujibu wa utaratibu. Kwa sababu ile bima itakubalika lakini itakuwa na muundo wake wa sheria.

Sasa nakuomba sana Mhe. Waziri nayo hii weka jina lako katika Wizara hii kuwatafutia sheria kuwawekea haya. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wanaanguka na mpaka leo sidhani kama kuna ambao wameshalipwa pesa zao. Hilo mimi siamini kabisa, ninaamini mpaka leo watu hawajalipwa na wanahangaika,

hasa katika Jimbo letu la Kitope wapo watu kibao kule mpaka Fujoni hawajalipwa mapesa yao walioanguka. Mhe. Mwenyekiti, sheria hii kama Mhe. Waziri ataifuatilia vizuri tutafanikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia suala la karafuu mpaka sasa hivi na hasa hii *branding* tuliyoikusudia itatusaidia sana kwa sababu sasa hivi mikarafuu nchi nyingi wanaotesha. Lakini sisi Zanzibar hapa ukiweka na ile hata mimi niliyekuwa sina macho nitasema ile kuwa Zanzibar kumbe Malaysia. Sasa mimi naomba kwa huu muundo ambao unataka kufanya hiki chombo cha kuweza kuitambua ile karafuu yetu *quality* yake. Hasa kwa sababu najua *quality* kuliko nyengine ni ya Zanzibar. Hasa unapokusudia Mhe. Waziri kuwa pesa hizi umetoa tamko rasmi na ndio umeamua kuwa na zao rasmi. Ndio maana nikakuongezea sheria kuwa Zanzibar sasa hivi unakusudia karafuu.

Sasa hivi Mhe. Mwenyekiti, watu matajiri nikwambie ukweli. *Alhamdulillah* siku hizi Mhe. Mwenyekiti, mpeta huukuti chini. Watu wamekuwa waangalifu tofauti na zamani. Mikarafuu haikatwi ovyo ovyo kwa sababu mtu akiikata anajua anaingia umaskini. Mwenye shamba anakuwa yumo katika utaratibu mzuri wa kusimamia. Mhe. Waziri nakwambia Mwenyezi Mungu atakupa fungu lako pamoja na Naibu wako na Katibu wako. Mumesifiwa hapa na mama yangu Mhe. Asha Bakari Makame na hiyo ni kweli sio siri. Katika mawizara niseme muna *sample* nyingi, Katibu wako unasikilizana nae, Naibu Waziri wako unasikilizana nae na Wakurugenzi. Lakini wizara nyengine Katibu anapita kushoto, Waziri anapita kulia. Tunakwenda wapi hizi kazi? Wanakuja kutambuana kwenye bajeti tu hapa. Lakini nyinyi wakati wote mko pamoja, kwa kweli nimefurahishwa kwa suala kama hilo.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho si vibaya na Wawakilishi wako hao ukawapeleka nchi za nje kwa kwenda kuangalia jinsi gani *modality* ya karafuu na sisi tukaweza kuagiza. Na katika safari hiyo ukiamua Mhe. Waziri *inshaallah* ukianzia mwanzo tu unione mimi hapa.

Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia, sina pingamizi nayo. Ahsante sana.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kwa dhati kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutupa pumzi hizi tulizokuwanazo kwa muda huu na muda unaokuja.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa dhati kabisa kwa kuweza kunipa nafasi hii ya kuwa mmoja wa wachangiaji katika Baraza lako hili tukufu la Wawakilishi Zanzibar, ambapo tumekuja hapa kuwatumikia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, leo nina fahari kusema kwamba bajeti hii imenigusa ndipo kwa sababu ndio fani yangu, ndio kazi yangu na *Alhamdulillah* nimefika wakati huo sasa kazi kubwa ni kuendelea kuwasaidia hii Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, nitoe pongezi za dhati kabisa kuishukuru wizara nzima kwa hekima zao, busara zao, usikivu wao kuanzia Mhe. Waziri, Naibu wake, Katibu, Manaibu Katibu, wizara nzima kwa jumla. Ni matumaini yangu kwamba kama ilivyo wizara hii naamini leo kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tutaiga mfano wetu kama mwaka jana; tunateremka tu kilima kwa kumsaidia huyu mwenzetu ili bajeti hii iweze kupita.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasaha zangu tu kwa Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti, namheshimu sana Mhe. Waziri, ni miongoni mwa watu ambao niliotoka nao mbali katika nchi yetu hii ya Zanzibar. Sasa kazi yetu kubwa mimi na Mhe. Waziri na wafanyabiashara wengine ni kuwatizama watu waliokuwa chini yetu sisi ambako ndio tunakotoka huko. Ninachomuomba Mhe. Waziri kwa heshima zote na namheshimu sana pamoja na uongozi wake mzima, anapopata masuala baadae akija kufanya *wind up* namuomba sana kaka yangu Mhe. Nassor Ahmed Mazrui pamoja na wasaidizi wake ikiwa jambo halijui aseme halijui, jambo amelikosea aseme naomba radhi, na kama wamelikoroga watendaji wake aseme hili limekorogwa na watendaji wangu.

Kwa hivyo, mimi ninachopenda kwamba akiambiwa ghala yake *ZSTC* inaweka karafuu, lakini banda hilo hata mbuzi huwezi kumuweka basi asiropoke. Kama kuna banda la *ZSTC* linavuja hata mbuzi huwezi kumuweka alifanyie kazi. Asije hapa sehemu hajafika akawa anaropokwa. Namuomba sana tena namheshimu.

Kwa hivyo, ninachoomba kila anapokuwa anakuja na suala hapa alifanyie kazi, hakuweza atuandikie alijibu jambo analolijua. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, humu ndani hatupo skuli, tumekuja huku kwa masuala ya kiutu uzima, Baraza hili ni la wananchi. Mimi naringia na *people's power* hii ya Uzini ndio niliyojia hapa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri awe msikivu, yale anayoyajua ayajibu, kama amekosea namuomba basi aoneshe mfano aombe radhi, mimi bwana hili jambo nimelikosea nawaomba radhi Wawakilishi. Huu ndio uungwana, huu ndio Uzanzibari. Kama mtendaji wake amekoroga aseme.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimkumbushe Mhe. Waziri. Wakati tulipokuwa tunafanya kazi pamoja siku moja tuliitwa Ikulu na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati huo alikuwa ni Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma. Mimi na yeye tuliitwa na nakumbuka Komandoo Rais alitwambia kwenye meza wanangu Raza na Sheikh Nassor Mazrui mnapopewa majukumu na wenzenu basi watumikieni wananchi ili mkimaliza wananchi wakukumbukeni na Serikali ikukumbukeni.

Sasa namwambia Mhe. Waziri dhamana aliyopewa na Rais akamteua Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ni dhamana kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu. Ni imani yangu dhamana ile aliyopewa na Mhe. Rais, dhamana aliyopewa na wananchi ndio atakayokuja kuitumikia, ili heshima yake iendelee kuwekwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nataka nimuulize Mhe. Waziri kwa ufasaha kabisa na utulivu. *Zanzibar Bureau of Standard* nataka aje atwambie mpaka sasa hivi imefikia hatua gani. Je, imeshajiunga na nchi za Afrika Mashariki na Kati, *East Africa, SADC* na Mataifa mengine. Kumbukumbu nilizozikuta hapa hii *Zanzibar Bureau of Standard (ZBS)* ilikuwa imeshapitishwa na Baraza lako tukufu mwaka 2011. Kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu ametujaalia Mhe. Rais wetu, mpendwa wetu, Rais Alhaj Dkt. Ali Mohamed Shein akasaini baada ya kupitia kwenye Baraza la Wawakilishi. Sasa nataka kumuomba Mhe. Waziri atakapokuja atwambie kwamba hii imefikia hatua gani katika kujiunga.

Mhe. Mwenyekiti, nikimalizia hapa nakuja na suala la pili la *COMESA*. Hili Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati lilimfika Mhe. Waziri. Nataka atwambie Zanzibar tupo katika hatua gani ya kujikwamua katika mazingira haya ya biashara na uchumi wetu.

Pia Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri mambo ya biashara hayamo ndani ya Muungano. Na haya masuala ninayomuuliza wala hatuna haja ya kusubiri Bunge la Katiba kwa sababu Muungano wa Biashara ndani ya Jamhuri yetu ya Muungano haupo. Nchi huru mbili zimeungana, Marais wawili, hakuna Rais mkubwa wala mdogo. Kuna taratibu tu tumewekeana. Kwa hivyo, tumeungana nchi mbili huru kuipata Tanzania, hapo kambla zikiitwa Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Tanganyika. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachoomba kwamba hazi ni dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nimuulize Mhe. Waziri suala zima hili la Afrika Mashariki na Kati, juu ya biashara. Kwa sababu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko haimo ndani ya Muungano. Sasa nataka kujua nini hatua tuliyofika sisi Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara, tulichofaidika na tunachoelezwa katika mambo ya Afrika Mashariki na Kati.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba suala la Afrika Mashariki na Kati toka hapo mwanzo Zanzibar tuna nyaraka. Tulisema tuingie kama Zanzibar kwa sababu kuna mambo ya biashara, michezo, kilimo, miundombinu, mifugo, kuna mambo ambayo haya yote hayamo ndani ya Muungano.

Sasa nataka aje aseme Mhe. Waziri hatua waliyofikia na hatua tuliyofikia sisi. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri sasa hivi watu wanazungumza hili suala la Muungano wa Fedha ya Pamoja. Sasa Mhe. Mwenyekiti, ninachotaka Mhe. Waziri asije akatafuna maneno, aje atwambie sisi Wawakilishi na wananchi, hivi vituo vyote tumefikia hatua gani na Zanzibar ipo kwenye *position* gani, na *what is next* ili tupate kuisaidia wizara na serikali kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa isitoshe suala la biashara nilimuuliza mwaka jana Mhe. Waziri, suala la matairi, kuna *spares* za *Isuzu*, vitu vya *Toyota* na mambo mengine. Sasa ninataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba *ling long* ambayo yanapakia kokoto na mchanga. Kwa bahati nilikuwa sikufuata utaratibu, nilikuja na *sample* Mhe. Mwenyekiti, lakini ilikuwa ule utaratibu sijakamilisha ningeliweza kuja kukuonesha. Unajua Mhe. Mwenyekiti, hii kuwasaidia Waheshimiwa Wawakilishi, hii ndio fani yangu ya biashara.

Sasa hii *ling long* ndio inayopakia gari za michanga. Mpaka sasa hivi imekuwa huwezi kuleta *ling long* ukenda China anakwambia *agent* Tanzania, wakati ni *agent* Bara. Sasa vitu vyote hivi sasa inabidi tuvipitishie njia ya Dubai kutoka China, ikitoka Dubai ndio ije Zanzibar.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, gharama zinakuwa mara mbili. Kwa hivyo, gharama zile magari yale au matairi yale sisi hatuyapanti, sasa utakuta wananchi wetu wengi wanapenda kwenda kwenye majumba lakini kuna gharama

ambazo zingeliweza kupungua kama serikali au Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko ingelikaa na kuona jinsi ya utaratibu mzima.

Mhe. Spika, sasa ninataka Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kwa ufasaha hatua aliyofikia katika hilo. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna haja wizara hii kama nilivyosema na sisi wafanyabiashara ambapo Mwenyezi Mungu ametuleta hapa tulipofika, kazi yetu kubwa Mhe. Mwenyekiti, sasa ni kwenda kutizama huko chini wenzetu walivyo, ndio kubwa sana.

Sasa jambo ambalo Mhe. Mwenyekiti, nililokuwa ninasema hili suala la misamaha. Mimi ninamshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza, ninaishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa imetoa msamaha kwa walengwa. Mchele hivi sasa hauna ushuru, tende hulipii, sukari ni *ten percent*.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, na mwaka jana nilizungumza, ninataka nimuombe Mhe. Waziri kwamba hivi vitu tunachotaka sisi wafanyabiashara wote wafaidike. Lakini utakuta meli ipo Chumbe msahama unatoka kesho, wanaofaidika ni watu wawili watatu akina Mohamedraza. Nilizungumza kwa nini fursa hii wasipewe wafanyabiashara wote, wakapewa miezi mitatu serikali inajua inakuja kusamehe mchele, tende, sukari kupunguza makali ya wananchi walio chini hasa mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini matokeo yake mimi Mohamedraza nimeshaweka meli yangu pale nitakwenda, kwa hivyo hata wafanyabiashara wengine wale ambao wana fursa wanalipa ushuru, leseni, *Tin number*. Matokeo yake hata ukenda kuagiza baada ya miezi mitatu. Sasa mimi ninafikiri Mhe. Waziri asaidie sana, kufanya kosa sio kosa ila kosa ni kurejea kosa. Nilizungumza mwaka jana, imekuwa lengo la wafanyabiashara wote walete ile sukari, mchele, matokeo yake fursa ile wameshindwa na wananung'unika na sisi tuna jukumu la Mwenyezi Mungu.

Mimi Mohamedraza nipo kila kitu kwenye faida tu. Sasa ningeliomba Mhe. Waziri kwamba hivi vitu kwa kodi zake, hivi visaidiwe wananchi na mimi nikitaka kutoa wito kwa wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti, hasa kwa mwezi huu. Ningeliomba kwa kuanza mimi Mohamedraza tutoe *subsidize* kwa sababu hivi vitu tulivyovileta vitakaa, si kila anayepepesuka ni mlevi, si kwamba watu wote ni sawa. Vitakaa wengine watavieka *stock*, ikisha Ramadhani vitakuja kuuzwa mara mbili, mtu kishapata msamaha. Kwa hivyo, ninachotoa wito kwa wafanyabiashara tuwakumbuke watu wanakotoka na hali ya maisha ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo nikitaka Mhe. Waziri hili alitazame vizuri kusaidia wale walengwa. Kama walengwa hawakupata afueni hii, wizara ninaomba kwa sababu Mhe. Waziri ni msikivu sana. Wafanyabiashara wengi tunamuheshimu sana na tunaithamini wizara yake, lakini tutafute njia ya kuitana kwa sababu si vizuri ikawa samaki mmoja kaoza wakawa samaki wote wameoza, aah! *la hasha*. Kuna wengine wana nia nzuri, wengine wana-*subsidize*. Lakini yule anayeuza mchele - anaeleta, yule mtu wa pili wa dukani anauza mara mbili.

Sasa hili ni lazima tuliweke sawa ili manung'uniko haya na lengo la serikali yawafikie walengwa waliokuwepo kwa mchele, tende na sukari. Tukiacha hivyo mtu atakwenda kuchukua *stock* yote kwa Mohamedraza, kaleta meli anakwenda kuleta kuweka kwenye ghala yake, mchele unapungua. Mwezi wa Ramadhani ikimaliza anakwenda kuuza mara mbili, wakati ule Mohamedraza kauza mchele kutokana na afueni aliyepata ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, matokeo yake mutakuja kuwaandama wale wafanyabiashara wakubwa ambao wameitikia wito, lakini kuna wa pili yake na wa tatu yake ndio wakorofi. Kwa hivyo, mimi ninachoomba Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ikatazame maghala, ikatazame watu waliopewa msamaha wafuatwe wale waliopewa msamaha, bwana eeh! Bwana wewe umepewa msamaha uko wapi mchele, huu hapa, nani uliyemuuzia, huyu hapa. Ili yule ambae ameuziwa mtu wa pili asiende akazifungia asubiri Ramadhani imekwisha mchele urejee mara mbili. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Mwenyekiti, tuna dhima kwa Mwenyezi Mungu na nikasema kwa sababu ili masuala ya biashara, ujanja wa biashara tunauelewa, mimi ninauelewa, Mhe. Waziri anauelewa, wafanyabiashara wanaelewa. Kwa hivyo ni lazima tuisaidie serikali katika hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika 5.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ningeliomba hali halisi ya Mhe. Waziri kwa kumalizia kwamba aje na muongozo huu nilioutoa. Majibu yangu niliyoyasema kwa uwazi kabisa lakini vile vile nichukue nafasi hii kuwaomba Wawakilishi wenzangu kwa heshima zote, ninawaomba kwamba wizara hii ni ya usikivu. Mimi kwa niaba yangu kwa wananchi wa Jimbo la Uzini, sina haja ya kutoa shilingi. Ninamuamini ninamuachia yeye Mwenyezi Mungu. Ninaiunga mkono zaidi ya asilimia mia, kuanzia mimi na wananchi wa Jimbo la Uzini na wala sina haja kupiga buti.

Amejibu anafahamu yeye lakini ninachomuomba kwamba aje na maneno ya ufasaha. Kuna mwenzangu atasimama akilisema banda haliingii mbuzi akalitizame, alifikirie asije akaropoka hapa. Kwa hivyo, ninachomuomba heshima yake huyu Mhe. Waziri Mhe. Mwenyekiti, aendelee kwa sababu tumekuja humu ndani kuwatumikia wananchi, bila ya kujali rangi, kabila, dini au chama.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache ninashukuru na ninaiunga mkono sana wizara hii kwangu mimi na wananchi wa Jimbo la Uzini na ninaomba Wawakilishi, huyu kijana ni mwenzetu, mkweli tumpe nguvu ya wizara nzima ili atusaiie.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali. Sasa ni nafasi ya Mhe. Raya Suleiman Hamad na baadae Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Mimi ni mjumbe wa kamati lakini nina maulizo tu kidogo.

Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataallah* mwenye kutupa uhai na uzima na tukaweza kuhudhuria hapa leo. Vile vile ninakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi ya kuzungumza na pia ninaipongeza serikali na ninampongeza Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sisi Wapemba kule zao letu kubwa na sikukuu yetu ni zao la karafuu. Mheshimiwa alipoingia madarakani na akaweza kulinyanyua zao hili la karafuu. Mimi ninapongeza sana. Halafu ninawapongeza watu wa mawizara. Ninampongeza Mhe. Waziri na wafanyakazi wake wote isipokuwa mimi nitamuulizia kidogo tu, kwa sababu siku nyingi kwenye kamati nilikuwa sipo lakini mwaka 2011 nilikuwepo na nikatembelea kidogo, nina mambo kidogo tu ninataka nimuulize.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza hii Ofisi Kuu Pemba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Kule kwenye viwanda Pemba niliwahi kutembelea na tukaviona viwanda pale Wawi havina ubora. Mhe. Mwenyekiti, tuliweza kutoa maelekezo yetu. Ninataka nijue tu kwamba viwanda vile viko hali gani ili kuweza kufanyiwa matengenezo na kuweza kuboreshwa. Kwa sababu pale tulisema hata ile mitambo yenyewe ikitaka ifanyiwe matengenezo tupate mtambo wa kisasa, kwa sababu pale wana mambo mengi wanayoyafanya ya kuweza kuzalisha mafuta ya makonyo na mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, tulikwenda kukagua vikundi vile vya yale majungu wanayoita mafuta ya mkaratusi, tulikwenda kwenye yale mashamba kwenda kukagua. Pia navyo tukaviona. Vile vile aje anipe majibu vimefikia au havipo tena na hapa tujue huu ukarabati wa viwanda vyetu uliofanyiwa.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nitauliza neno moja tu, kuna ile ofisi yetu iliopo Dar es Salaam kule. Ofisi ile ilikuwa ipo katika hali mbaya sana. Kila tukenda ile afisi ipo kwenye hali mbaya sana na tulipokwenda katika lile jengo mara moja, hapo nilipomalizia mimi walisema wana nia ya kuwa liuzwe wapate pengine au waweze kupata sehemu nyengine ya kukaa. Vile vile aje anijibu Mhe. Waziri limefikia wapi jengo lile la *ZSTC* kule Dar es Salaam. Kwa sababu sehemu yao iliyokuwa ni mbaya na katika zile bidhaa zao wanazoweka hata ile nafasi Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa ndani hamna.

Mhe. Mwenyekiti, halafu vile vile nikija bandarini pale Dar es Salaam tulikwenda kutembelea pale, tukakuta watendaji wetu. Lakini kilio chao kikuwa walichotupa pale walikuwa wao hawana ile kazi hasa ya kufanya. Mizigo ikija hata ikiwa imehusu Zanzibar lakini walio pale ndio wanaosimamia mizigo ile, wao walikuwa wapo tu katika ile ofisi, walikuwa hawana matumaini yote. Hata maposho yao ilikuwa mpaka yatoke huku na pengine wakikaa miezi kadhaa hawajapata pesa pale. Tulikwenda ofisini pao pale kwenda kuwakagua.

Mhe. Mwenyekiti, halafu mimi ninataka nimuulize tena Mhe. Waziri ana mpango gani wa kudhibiti wahalifu wa mikarafuu. Kwa sababu mikarafuu Mhe. Mwenyekiti, inazaa lakini itakapozaa mikarafuu wewe mwenyewe

una gamu. Kwanza huthubutu ikiwa upo mbali mkarafuu kwenda kuukagua wewe peke yako, lazima uende na mwenzako, unaweza ukauliwa wewe na ule mkarafuu wakakata wakachukua. Atueleze amedhibiti vipi watu hawa wanaokata mikarafuu kwa wingi, kwa sababu mimi nina mtoto wangu ana mikarafuu hii ya kunyanyukia nyanyukia pale Chanjamjawiri.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana alipata hasara kubwa ya mikarafuu yake kukatwa na ule mkarafuu hujui unakwenda kupelekwa wapi. Hata ukiutafuta huoni wewe utakuta shina tu pale kwa sababu ile mikarafuu ni midogo. Kwa hivyo, watu wanakata halafu wanaibeba.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nikiondoka hapo mimi ninauliza katika Shirika la *ZSTC*, tulikuwa na mpango wa wale wachumaji wa karafuu kuwakopesha majamvi. Kwa sababu tukiziona karafuu zetu barabarani zinaanikwa chini mabarabarani, ukenda hapa uwanja wa Gombani watu ndio wanapofanya pakuanikia karafuu. Tunazitoa thamani kwa sababu hasa zinaanikwa kwenye majamvi, karafuu zikianikwa chini zinapungua ubora kwa sababu zinaingia mavumbi na ile hadhi yake ya mmerometo unaondoka.
Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Waziri aje atwambie wamefikia wapi huko ukopeshaji ule wa majamvi na umemalizikia wapi mpaka karafuu tukipita barabarani, zinakanyagwa na magari na zikawa hazina ubora. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tujue hawa watu wa ukulima wa mikarafuu katika *ZSTC*, tujue ni wangapi waliowezeshwa kupewa fedha za kuweza kujiendesha katika kuboresha mashamba yao na tujue wangapi waliokuwa hawakupata mikopo. Wakikopa tujue, je, pesa hizi wanazirejesha au ndio basi.

Mhe. Mwenyekiti, pale Mkoani tulikwenda mara moja vile vile kukagua mezani. Namuomba Mhe. Waziri aje anieleze matatizo yale ya mezani wameyatatua vipi ili kupata mezani za kisasa kuwaondolea hofu wananchi katika upimaji wao wa karafuu, wasione kuwa wamenyang'anywa.

Mhe. Mwenyekiti, zao la karafuu na biashara kwa jumla, kwa kweli Zanzibar ndio tegemeo letu. Awe makini sana Mhe. Waziri katika zao hili. Vile vile kwanza ninapongeza vikosi vyetu kuweza kutulindia na karafuu zikaweza kupatikana kwa wingi, ikawa zimepungua kidogo ule mpunguzo wa kuweza kutukimbia karafuu zetu wakati bei yetu ni nzuri. Tuweze kusimamia kwa umakini na tuweze kupata maboresho.

Vile vile ninasema tena kuwawezesha wafanyakazi wetu ndio watakapoweza kufanya kazi zaidi na tukaweza kupata kipato chetu kikakidhi haja. Ukiwazembea wafanyakazi lazima na wewe watakuzembea katika kazi yako, wapate maposho yao kwa wakati, na wapate mishahara yao kwa wakati. Kwa sababu hawa wanafanya kazi masaa 24. Sisi tuliopo Pemba tunaona ile jitihada kwa sababu kule ndio kwenye zao hili la karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nina mambo kidogo tu hayo ya kumuuliza Mhe. Waziri. Kwa hivyo ninaiunga mkono hoja yake asilimia mia kwa mia na ninawaomba wenzangu tuweze kumpa msaada mkubwa ili aweze kufanikisha malengo haya.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Raya Suleiman Hamad. Sasa ni nafasi ya Mhe. Mahmoud Thabit Kombo na baadae Mhe. Nassor Salim Ali.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Mhe. Mwenyekiti, ninakushuru sana na naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataallah* kutujaalia sote tukiwa hapa hai na wazima na leo kuchangia katika wizara hii muhimu ambayo inagusa maisha takriban ya wananchi wote wa Zanzibar, ambao huwa wanaungana na sisi mara nyingi kusikiliza haya yanayoendelea humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia mchango wangu, kwanza naomba sana nimpongeze Sheikh Nassor Ahmed Mazrui - Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa kuwasaidia wananchi kiuchumi. (*Makofi*)

Naomba pia kumpongeza sana Hajati Thuwayba Edington Kissasi - Naibu Waziri wa wizara hii pamoja na watendaji wote wakiongozwa na ndugu yetu Mr. Julian Raphael. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa katika mchango wangu naomba niseme kwamba Zanzibar *historical* ni *trade port*, yaani biashara nyingi sana wakati huo zilikuwa zinafanyika Zanzibar. Wakati huo Zanzibar ilikuwa kuliko hiyo Dubai. Wakati huo Zanzibar ilikuwa kuliko masoko mengine ya Singapore huko ulimwenguni ambapo katika Afrika hapa ndio palikuwa panafanyika *trading*.

Kwa sababu gani palikuwa panafanyika *trading*, yaani biashara? Kwa sababu ardhi yetu ya kilimo ni ndogo. Maisha ya watu wa Zanzibar kiasili ni biashara na ni makutano ya kuleta bidhaa mbali mbali ambazo hata minada mikubwa ilikuwa ikifanyika hapa.

Historia inatwambia hivyo na ndio maana kuna masoko mbali mbali ambayo yamejengwa hapa. Lakini sasa mambo hayo hayapo tena lakini biashara bado ipo na imeendelea kubakia katika *commodities* mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika mchango wangu wa leo, naomba sana kwanza kumpongeza Mhe. Waziri lakini pili naomba Mhe. Waziri akija pale kujibu, ajue kwamba Wawakilishi wanafanya *research*, wanaangalia haya mambo, wanazungumza na wananchi na la mwisho kabisa wananchi wetu wana akili tena wana akili sana, maana michango wanayotupa wengine sisi wenyewe huku hatujui, wanajua kila kinachoendelea na wana mategemeo mwakubwa sana kwa serikali yao.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja kujumuisha basi aje na majibu, maana tunakuwa na mtindo wakati mwengine huingia *virus* humu. Ikawa waziri umeshazungumza naye kila kitu vizuri, umemuuliza lakini akishafika pale kwenye meza kuna *virus*, naomba Mwenyezi Mungu amjaalie *virus* hao wasimuingie yeye Mhe. Nassor Mazrui, *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amuepushe yeye pamoja na Mhe. Thuwaybah Edington Risasi Naibu Waziri wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa biashara sasa hivi inachangia kwa asilimia 10 tu ya kipato cha Zanzibar, viwanda naamini viko chini ya hapo naomba kumlaumu sana Mhe. Waziri katika kitabu chake angetuwekea majedwali, lakini hakuna majedwali Mhe. Waziri kwenye kitabu na haya majedwali huwa ndio yanatupa mara nyingi takwimu mbali mbali. Nadhani katika vitabu vyote tulivyosoma vya wizara zote, basi kitabu hiki ndio chenye majedwali machache kuliko kitabu chengine chochote.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri ukija katika majumuisho, mimi nitakupa takwimu ambazo nimefanyia *research*, lakini ukija katika majumuisho kama utaweza kutoa jedwali mbali na hii jedwali moja tu ulilokuwanalo la matumizi na mapato ya wizara yako, basi itakuwa ni vizuri sana. Jedwal lako liko moja tu hapa nimeliona katika ukurasa wa 6, hilo la kwanza na la pili liko huku mwishoni.

Mhe. Mwenyekiti, kuna jambo moja muhimu sana biashara inachangia asilimia 10 ya kipato cha Zanzibar, viwanda imo kwenye asilimia 6 au 7, utalii iko zaidi ya 40, sasa ukichanganya na bahati mbaya utalii haiko kwanye wizara yake yeye, lakini ingekuwa kachanganyishiwa na utalii basi yeye angekuwa na zaidi ya asilimia 55 ya uchumi wa Zanzibar, pamoja na wizara yake ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, nitarudi katika hizi takwimu ambazo tunazo. Katika nchi yoyote tutazame nchi zenye chumi ndogo ndogo kama visiwa. Tutazame Singapore, tutazame Mauritius, tutazame Seychelles, tutazame nchi zote za visiwa zenye serikali zenye uchumi mdogo, utakuta kitu kikubwa kinachochangia katika uchumi wa nchi ile, Mhe. Waziri naomba nimuambie ni *Lower Interest Rate* za Banki. Sisi hapa Zanzibar tuna za *Highest Interest Rate* zetu za benki, haiwezekani wala huwezi kukuza uchumi. Uchumi wetu *bank base rate* ni kuanzia asilimia 17 ndio unaanza kukopeshwa, wawakilishi wengi wamekopa humu benki watakuwa wanajua.

Mhe. Mwenyekiti, Singapore leo ukenda au ukenda Mauritius hapo jirani, ukenda Seychelles basi benki zao ni kati ya asilimia 2 na 4. Kwa hivyo, inakuwa haingii kwenye mankiti kwamba kama ile serikali inakuchukulia dhamana au serikali kama haiwezi kukuchukulia dhamana wewe mwananchi wake ikaweza kumchukulia mtu wa nje haiwezekani.

Tuna wizara ya uwezeshaji ambao wanatoa uwezeshaji kwa wananchi. Tunaambiwa kuna *fund* ya bilioni 2 kule, juzi Mhe. Zainab Mohammed alisoma bajeti yake, ambayo ile *fund* hai-*charge interest*. Sasa kule anakopeshwa mfanyabiashara mdogo au mwenye kikundi, nadhani mwisho ni milioni 5. Lakini wakati huo huo benki, hususan benki yetu *PBZ* imejaa mafedha sasa hivi kwa sababu watu hawana uwezo wa kukopa katika benki.

Mhe. Mwenyekiti, benki inakopesha kwa asilimia 17, ina maana mfanyabiashara anatakiwa apate faida zaidi ya asilimia 30 ili aweze kulipa mkopo wake na riba ya asilimia 17. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi biashara zote *average* ya faida ni baina ya asilimia 20 na 25, baada ya kulipa vitu vyote hivyo, *VAT* na *tax* nyengine ni humu humo asilimia 20, wengine hushuka katika faida yao mpaka asilimia 15.

Kwa hivyo, kama tunataka mfanyabiashara akuwe basi kama yule mfanyabiashara anapata asilimia 15 atawezaje leo kukopa benki kwa faida ya asilimia 17. Sasa hapo Mhe. Waziri anaweza kuja kunijibu kwamba

mabenki haya yanakuwa *regulated* na *BOT*, ndio *regulator*. Ninachotaka kusema mimi ni kwamba kama mfuko wa uwezeshaji unaweza kumkopesha mwananchi wake wa kawaida bila faida, basi benki hizi zetu, kwa hapa Zanzibar zinaweza kuwa na *sub-regulations* ili kumkopesha mfanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii Mhe. Waziri akitaka *server* ya wizara hii basi ni *small and medium enterprises*. Mfanyabiashara mkubwa kabisa hapa Zanzibar tunamzungumzia Mhe. Raza maana kazungumza sana. Mhe. Raza ana biashara na kajitolea yeye mwenyewe mfano.

Mimi nilibahatika siku moja kutembelea kwenye ile *godown* yake, nikakuta vespa nyingi sana, nilikuta karibu vespa 1,000. Nikauliza swali pale, kwa nini jamani hamumshauri Mhe. Raza afunge *assembling plant* ili vespa hizi tuwe tunazifungia hapa hapa Zanzibar? Kwa sababu kuleta *finishing goods* au *finishing products* yaani bidhaa ambayo imeshamalizwa kutengenezwa basi ni tofauti na ukiwa una-*create* ajira na watu wanafanyia biashara hapa hapa kwa kupata ajira kwa kufanya *assembling* na wakati huo huo Mhe. Raza ataweza kuleta makontena mengi zaidi ya *spare parts* ambazo atachajiwa kama *spare parts* ili afunguwe *assembling plant* ya kufunga zile vespa pale. Naamini mimi ikifanyika hivyo basi vespa hizi hazitouzwa kwenye soko la Zanzibar tu, lakini itaweza kuwa *exported* katika *SADEC* nzima, ambapo sisi tuna ushuru nafuu katika hili eneo la *SADEC*.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri akija kidogo atowe ufafanuzi je, anachukua jitihada gani katika eneo hili la kuhakikisha *lowering of interests rate*, ili mfanyabiashara wa Zanzibar apate kukua, apate kujiweza, apate kujikimu na biashara yake itanuke. Leo wafanyabiashara wa Zanzibar wanaaminiwa na mabenki ya nje zaidi kuliko benki zetu za Zanzibar. Wako wafanyabiashara wa Zanzibar ambao wamekopa katika benki za nje, wamepata *interest rate* ndogo zaidi na biashara ile inafanyika hapa. Sasa faida ile inakuwa sio yetu, inakuwa ni kwa benki za nje wakati benki zetu zinaendelea kujaza *reserve* ambayo inakuwa haifanyiwi kazi.

Mhe. Mwenyekiti, faida ya benki ni ku-*lower interest rate*, kupata mzunguko wa fedha mkubwa ndipo mishahara yao wataweza kujilipa. Kwa sababu ku-*store* pesa nyingi pia nayo ni hasara, kwa sababu unahitaji ulinzi wa hali ya juu, unahitaji *facilities* nyingi kuweka fedha zile.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Rais kwa kubuni lile tamasha la biashara wakati wa sherehe za Mapinduzi. Mimi nilibahatika kutembelea na nilifanya mahojiano mengi sana pale na vyombo vya habari pia. Naweza kusema maonesho kama yale ndio *exposure* kwa nchi, maonesho kama yale yasisubiriwe sherehe mpaka miaka 50 au 60 au miaka 100 mingine ndio yafanyike tena. Maonesho yale ikiwezekana Mhe. Mwenyekiti, yafanyike kila mwezi. Kwa sababu pale ndio mwananchi wa kawaida au mfanyabiashara wa kawaida anapata ku- *showcase products* zake.

Mhe. Mwenyekiti, hapa palikuwa na *Sunday Market* sijui imekufa wapi. Mhe. Waziri ningependa sana atowe ufafanuzi, hizi *Sunday Markets* zimekufia wapi. Kule Ulaya mpaka leo wana jina lake wanaita *Pat cot Market*, ambayo hili soko la Jumapili huria huwa linafanywa kila Jumapili, hivi ni vitu ambavyo wananchi vitaweza kuwafaidisha ku-*show case products* zao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa kufanya ziara katika hivi vikundi mbali mbali vya ujasiriamali na uzalishaji. Mhe. Waziri kwa bahati nzuri katembelea Jimbo la Kiembesamaki hivi karibuni, kama sijakosea alitembelea vikundi vitatu. Hebu Mhe. Waziri ukitembelea vikundi hivi basi fuatana pia na viongozi ambao wanawawakilisha wale wananchi, mtafute Mwakilishi wa Kiembesamaki uende nae, mtafute diwani uende nae. Ukijenga utamaduni huu basi hata yale mafanikio yako ya kutembelea vile vikundi yatakuwa ni makubwa zaidi. Mimi nakupongeza sana kwa kufanya hivyo, lakini hebu watafute hawa viongozi uwe unakwenda nao.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, vikundi hivi huwa vinakwenda kule Saba Saba; namshukuru Mhe. Waziri yeye ndie ana wa-*facilitate* kuwatayarishia mazingira mazuri kule Saba Saba, ili *products* zao zionekane. Kwa hivyo, Mhe. Waziri nakuomba sana vikundi hivi wanapofika kule muwasaidie zaidi na muwashajihishe viongozi wengine wa kule wa kwenu ambao wapo, ili wawapokee na kuwa nao karibu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika tano.

Mhe. Mahamoud Thabiti Kombo: Mhe. Mwenyekiti, niongeze dakika nina vitu vingi kidogo, lakini nitajitahidi.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kiwanda cha maziwa cha Bakharesa. Mhe. Mwenyekiti, mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri wawekezaji kama hawa na wengine kina Raza na wengineo basi angekuwa kila mwezi

anafanyakazi ya kukaa nao, ili kuwashajihisha waongeze zaidi uwekezaji wao, kwa sababu hawa ndio wanaotengeneza ajira.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitatoa takwimu chache tu ambazo Mhe. Waziri hajatoa, hebu namuomba akija hapa anitolee takwimu zaidi juu ya kiwanda cha maziwa. Mimi ninavyojua kiwanda kina mitambo ya kisasa. Nilibahatika kufanya ziara kidogo pale, hiyo ziara ilifanyika kwengine lakini na mimi nilibahatika kuwemo na nilifanya ushawishi mkubwa sana kuuliza. Kiwanda kile Mhe. Mwenyekiti, kina mitambo ya kisasa, tulipo kwenda kule walisema kwamba watakuwa na uwezo wa kuzalisha tani laki moja na nusu kwa siku ya maziwa.

Mhe. Mwenyekiti, hizo karafuu zake Mhe. Waziri anazojidai nazo, karafuu zote hizo mwaka mzima tani 4,200 tu. Lakini kiwanda hiki kitakuwa na uwezo wa ku-*export* maziwa sio Tanzania peke yake, ni Afrika Mashariki nzima kitakapokuwa katika *full capacity* yake. Mhe. Mwenyekiti, kiwanda hiki kinatarajiwa kulipa serikalini karibu bilioni moja, katika *tax* tu. Hiyo bilioni moja imepita wizara nyingi hapa kwa mwezi katika bajeti zao. Kwa hivyo, kiwanda hiki kina matarajio hayo.

Pia wamenunua meli ambayo baada ya yale maziwa kuzalisha basi yatakuwa yanatolewa kutoka Zanzibar na kupelekwa Bara. Sisi Mhe. Mwenyekiti, tutakuwa tunatumia asilimia 5 hadi 10 *maximum capacity* ya kiwanda kile tutakuwa tunatumia sisi wenyewe Zanzibar.

Kwa hivyo, wawekezaji kama wale Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri anatakiwa kama sio kila mwezi kukutana nao basi kila siku awe anapata nao *breakfast* ili kuhakikisha kwamba uwekezaji kama ule unaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda wangu ni mchache naomba nimalizie la mwisho kuhusu habari ya mambo ya karafuu *ZSTC* kidogo tu. Hawa *ZSTC* humu kuna mpango umeandikwa wa kutaka kuwapunguza wafanyakazi, imo humu kwenye kitabu imeandikwa. Nadhani wamewapunguza wengine na wamewalipa mafao yao, kwa sababu tunawajua wafanyakazi wengine wa *ZSTC* kwa ukaribu wao. Lakini wakati huo huo *ZSTC* hiyo hiyo inataka kuajiri tena. Kwa hivyo, ningeomba ufafanuzi hapa wale waliopunguzwa vipi, kama walikuwa tayari wameshafikia umri wa kustaafu au wamepitiliza na wao wanaongezwa ni vijana wabichi *fresh graduates* kutoka *Universities* zetu, na kiasi gani kitatumika huko.

Pili *ZSTC* Mhe. Mwenyekiti, wameshika kwenye karafuu tu, wataalamu wote wanaekeza kwenye karafuu, pesa zote zinaelekezwa kwenye karafuu. Karafuu hazifiki hata 40, ni 30 *million* US *dollas*. Kuna biashara hapa hapa Zanzibar Mhe. Mwenyekiti, biashara moja inalipa zaidi ya *million* 30 katika ushuru tu kwa mwaka, tunazijua hizo biashara. Juzi *ZAT* ilitajwa hapa na pesa zake iliyolipa nyingi. Lakini sisi tuko kwenye karafuu tu, wataalamu wote, nguvu zote, maghala yote, *resources* zote na pesa zote.

Mhe. Mwenyekiti, hebu aangalie na hii biashara ya mwani. Biashara ya mwani ni shilingi 17,000 kwa kilo na milioni 17 kwa tani, biashara ya mwani inashindana na karafuu. Lakini katika jambo ambalo hamna kitu chochote, hakuna utaalamu, hakuna *storage capacity* na kadhalika. Wale baada ya kuvuna zao la karafuu ambalo ni miezi miwili *maximum.* Mimi nakumbuka wakati tulipokuwa shule tulikuwa tunapakiwa kwenye meli, kwenda kuvuna karafuu ilikuwa ni programu maalum wakati huo. Lakini baada ya miaka miwili wale watu wote wanakaa chini wanafunga mikono. Kwa hivyo, *resources* zote za serikali, pesa zote zinatumika kwa miezi kumi inayobakia hakuna kitu, kwa sababu ile *season* ya karafuu ya miezi miwili inakuwa imeshakwisha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini Mhe. Waziri *capacity* ile, fedha zile, bajeti zile usitumie kwenye uzalishaji mwengine, kama mwani, *spices* na mambo yanayoibukia hapa Zanzibar, ili nayo yakaweza kuchangia katika *contribution* ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya Mhe. Waziri kunipa mambo yote hayo niliyosema na mengine sijatosheka nitamuandikia kwa maandishi, basi mimi nitakuwa maridhawa kabisa katika kuunga mkono hoja. Lakini akija kujibu kama wenzake wanavyojibu basi hapo tutakwenda katika ile *policy* yetu. Nashukuru sana Mhe. Mwenyekit.

Mhe. Mwenyekiti: Nashukuru sana Mhe. Mahmoud Thabiti Kombo. Sasa ni nafasi ya Mhe. Nassor Salim Ali, baadae Mhe. Mohammed Haji Khalid ajiweke tayari.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia kidogo hotuba hii ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Nassor Ahmed Mazrui, somo yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote katika kuandaa hotuba hii nzuri na ambayo ina maneno mazuri kwa maslahi ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze pia kwa kumpongeza Mfanyabiashara maarufu na mkubwa Tanzania ndugu yetu bwana Said Salim Bakhresa, kwa kuweza kuwekeza katika kiwanda kile cha maziwa ambacho kimeweza kuwaajiri wananchi wetu katika nchi yetu hii ya Zanzibar na Tanzania kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, nimuomba Mhe. Waziri na najua kwamba ana uelewano mzuri na mfanyabiashara huyu bwana Said Salim Bakhresa, kwa kuweza kukaa naye na kuzungumza nae. Ninaimani kwamba ndugu yetu huyu ni muelewa na ana imani na nchi yake, ana imani na ndugu zake, kwa sababu niliwahi kukutana nae tukiwa mimi na wewe Mhe. Waziri na alitueleza msuguano, ugumu wa kupata kuendesha katika kiwanda hiki, pamoja na ujenzi ule wa pale bandarini.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri baada ya kukutana nae siku ile nadhani anakumbuka, aliyachukua yale maoni yake na mapendekezo yake au maelezo yake na akaenda kumueleza Mhe. Rais na matunda yake leo tunayaona; bandari imejengwa, kiwanda kimejengwa na tayari kinaanza kufanyakazi kwa maslahi ya wananchi na serikali kwa ujumla.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri aweze kumshawishi mfanyabiashara huyu, kuweza kuekeza kule kisiwani Pemba, ili na wananchi wa Pemba na wao wapate fursa hii ya mfanyabiashara huyu.

Baada ya kutoka hapo Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye Idara ya Biashara na Ukuzaji wa Masoko. Mhe. Waziri katika kitabu chake ametueleza kwenye ukurasa wa 29 kifungu cha 57 naomba ninukuu Mhe. Mwenyekiti.

Ukurasa wa 29 kifungu cha 57 kinaeleza hivi:-

> “Kwa upande wa utafiti wa maduka, taarifa za awali zinaonesha kuwepo kwa maduka yanayozidi 3,000. Aidha, katika kusimamia mwenendo wa bei za vyakula muhimu taarifa zake zimeelezwa katika mapitio ya mwenendo wa bei ya chakula muhimu iliyoelezwa katika hotuba hii”.

Mhe. Mwenyekiti, maduka ambayo yapo Zanzibar ni takribani 3,000, ambapo wenye maduka haya wanakuwa wanalipa kodi, wanaingizia pato serikali. Lakini jambo la kusikitisha na ambao sio utaratibu mzuri kwamba utakuta wafanyabiashara wa Juakali kuweza kufanya biashara zao nje ya maduka kwa kuuza biashara barabarani na kuikosesha serikali mapato ingawa na wao wanakuwa wanafanya hivyo, kwa ajili ya kujikwamua kimaisha, lakini kiutaratibu si vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jambo baya zaidi ni kwamba wamekuwa wakiuza biashara hata hao wafanyabiashara ambao wanawauzia wanakuwa wanawauzia biashara ambazo zimekwisha muda wake. Kwa hivyo, utaona wananchi wananunua biashara zile kwa sababu wanaona ni rahisi, lakini kiafya sio nzuri.

Naomba wizara kwa kushirikiana na taasisi nyengine ambazo zinahusiana na masuala haya, kuhakikisha kwamba zinawaangalia wale wafanyabiashara wanaofanya biashara barabarani, ili kuacha kununua biashara au bidhaa ambazo zinaweza kuleta athari kwa afya zao. Kwa kweli biashara nyingi ambazo zinauzwa barabarani ni zile zilizokwisha muda wake au zinakaribia kumaliza muda wa matumizi. Sasa si vyema kuliachia suala hili na wananchi wetu kuendelea kupata athari kutokana na biashara au bidhaa hizi.

Hivi sasa tunaelekea katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mwezi huu kwa kweli matumizi ya biashara au bidhaa yanakuwa ni mengi, sasa si vyema kwa mwananchi kwenda kununua bidhaa ambazo zimemaliza muda wake wa matumizi. Hali hii inawapelekea wananchi kufuatilia kununua biashara au bidhaa zile kwa sababu ni rahisi, kutokana na kwamba wananchi wetu wengi ni masikini.

Kwa hivyo, katika kipindi hichi ambacho tunaelekea katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, namuomba sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kuhakikisha kwamba kwa kushirikiana na taasisi husika biashara zile ambazo zinauzwa katika mji wetu huu, angalau kuwapa maelekezo wale wafanyabiashara ambao wanauza biashara au bidhaa ambazo ziko kwenye kiwango kizuri na sio zile ambazo zimemaliza muda wake wa matumizi.

Nikiendelea na mchango wangu naomba nimuunge mkono Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kuhusiana na Maonesho ya Biashara kwa Wafanyabiashara. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli Maonesho ya Wafanyabiashara ni maonesho ambayo yanakuwa yanaleta faida kubwa kwa wafanyabiashara na wananchi kwa jumla. *(Makofi)*

Sasa katika kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu kulifanyika maonesho hayo. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba kila wakati wa sherehe za Mapinduzi Matukufu, maonesho haya yawe yanafanyika na tumekuwa tukiona kwamba wenzetu Tanzania Bara wanayo siku maalum ya kuonesha maonesho ya wafanyabiashara. Kwa hiyo, ni vyema na sisi hapa tukawa na siku au mwezi ambayo ni maalum kila mwaka kuhakikisha kuwa yanafanyika maonesho ya biashara. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji. Katika idara hii naomba nizungumzie kuhusu mradi wa mkakati wa kuendeleza zao la karafuu. Mhe. Waziri ametueleza hapa katika mikakati na mipango mbali mbali katika kukuza zao la biashara ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na zao la karafuu kwa upande wa mazao mengine na ametueleza hapa kwamba kuna mikakati ya kuhakikisha kuwa kuna uboreshaji pamoja na uzalishaji wa bidhaa mbali mbali. Kwa mfano, mazao ya viungo yakiwemo mdalasini, pilipili hoho, pilipili manga na bidhaa nyengine kama vile hiliki pamoja na mambo mengine.

Kwa kweli bidhaa hizi zinakubalika mahala popote ulimwenguni. Kwa mfano, ukienda katika nchi tofauti hususan katika nchi za visiwa kama Zanzibar ikiwemo Madagascar, Mauritius, Seychelles ni watumiaji wakubwa wa bidhaa kama hizi. Kwa bahati nzuri nimewahi kufika katika visiwa hivyo na nimeona utumiaji mkubwa wa bidhaa hizi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri katika kukuza mazao haya pamoja na zao la karafuu, lakini utumiaji wa bidhaa au viungo hivi ni mkubwa sana katika nchi hizi ambazo nimezitaja. Sasa wakati atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho naomba kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anieleze kwamba amefanya mipango gani kuzitembelea nchi hizo na kuwasaidia wafanyabiashara kwenda kuuza biashara zao hizi, ili kukuza uchumi wa nchi yetu katika kutumia viungo hivi ambavyo nimevitaja tukiachia zao la karafuu.

Mazao haya ambayo huwa yanazalishwa katika visiwa vyote viwili vya Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, imani yangu ni kwamba serikali kupitia wizara husika na waziri wenyewe, kama kweli watafanya bidii, maarifa pamoja na mipango kwa ajili ya kuweza kutafuta soko la bidhaa au viungo hivi, wananchi wetu wataweza kufaidika sana na kuweza kuingiza pato kwa serikali katika kuendesha uchumi wa nchi yetu na kwa maslahi ya wananchi wetu.

Nadhani si vibaya Mhe. Waziri wakati atakapofanya ziara zake katika nchi au visiwa hivyo, tukaambatana naye kwa ajili ya kwenda kutafuta soko hilo.

Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba ya Mhe. Waziri ametueleza kwamba kuna wale ambao wameshindwa kulipa fedha kupitia katika viwanda mbali mbali katika kusaidia kukuza uchumi wa nchi yetu. Hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba kuna watu ambao wanashindwa kulipa kodi ama fedha katika kuendeleza viwanda vyao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba watu hawa au viwanda hivi ambavyo vimeshindwa kulipa kodi mbali mbali, aje atueleze ni viwanda gani.

Vile vile nimuombe Mhe. Waziri kwamba kuna suala la ekari 42 la KVZ na Kiwanda cha Sukari cha Mahonda. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, atueleze kwamba lile limefikia wapi, kwa sababu suala la Mahonda ilikuwa ni kauli ya serikali na kuhusu jengo la Kiwanda cha JKU Saateni, nadhani Mhe. Waziri analifahamu na sijui limefikia wapi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja kufanya atusaidie.

Katika kutekeleza Sera au Ilani ya Chama cha Mapinduzi, naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwamba amekuwa akitekeleza vyema ilani ya chama kwa kushirikiana na Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ambayo yanahitajika kupewa kipaumbele au msukumo ni suala zima la ndugu zetu wafanyabiashara wa makotena, ambao wanakuwa wanafanya biashara zao na kuleta makontena mbali mbali ambapo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk amelizungumzia hili sio vyema kuwaona wafanyabiashara wanapata matatizo na Mhe. Waziri amenyamaza kimya.

Kutokana na hali hiyo, nimuombe Mhe. Waziri kwamba haya matatizo yanayowakumba wafanyabiashara wetu ni matatizo ambayo pia yanawakumba wananchi wetu, kwa sababu makontena yale yanapokwama wananchi

wetu wanapata matatizo. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba tatizo hilo ambalo limejitokeza analitatua na kama limekwama alikwamue kwa mslahi ya wafanyabiashara hawa ambao.

Kwa kweli hawa ni wafanyabiashara wazalendo, wazanzibari na wajibu wake Mhe. Waziri kuwasaidia na kuhakikisha kuwa kama kunatokezea mabadiliko ya ulipaji wa kodi ni vyema kuelimishwa wafanyabiashara hawa, ili kuelewa na kuliko kushtukiza na kuweza kupata matatizo kama haya ambayo yamejitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende kwenye Kiwanda cha Soda cha *Cocacola*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, unazo dakika nne.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na maelezo ambayo ametupatia Mhe. Waziri. Kufungwa kwa kiwanda kile wananchi wetu wengi wamekosa ajira katika kiwanda kile na wananchi walikuwa wanapata ajira kwa kuendesha maisha yao, kusomesha watoto wao, lakini kufungwa kwa kiwanda kile imekuwa ni hasara kwa wananchi wetu. Sasa kumekuwa ingawa wamaeleza katika taarifa yao kwamba kufungwa kwa kiwanda kile pia kumesababishwa na wafanyabiashara ambao wanaleta soda za vikopo kutoka nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri afanye kazi ya ziada na imani yangu ni kwamba uwezo huo anao kuhakikisha kwamba kiwanda kile kinarudi, ili wananchi wetu wapate ajira, kwa sababu tatizo la ajira katika nchi yetu ni kubwa, sasa tunawalilia wafanyabiashara akina Said Salim Bakhresa.

Sasa viwanda hivi ambavyo tayari vimeshaanza na vimewapa ajira wananchi kuweza kufungwa ni tatizo na nimuombe sana Mhe. Waziri kuhakikisha kuwa kiwanda kile kinarudi, ili wananchi wetu wanapata ajira kwa ajili ya kuipunguzia mzigo serikali yetu katika kupata ajira wananchi wake.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Mwenyekiti kwa sababu muda umekwisha, nasema naunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na niwaombe wenzangu kwamba tuipitishe bajeti hii, ili Mhe. Waziri aweze kuendelea na majukumu yake katika kuiletea maendeleo Zanzibar na wanzanzibari kwa jumla. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kupata nafasi ya kuweza kutoa yangu machache kuhusu Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Kwanza naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha asubuhi hii kuwepo hapa kwa ajili ya kuendelea na kazi zetu za kawaida za Baraza.

Pili nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na kunipa nafasi hii.

Aidha, nimpongeze Mhe. Waziri na Mhe. Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoendelea kufanya katika Wizara hii ya Biashara, Viwanda na Masoko, lakini uwezo wao huu wote umesababishwa na watendaji wao wote wakiongozwa na Katibu Mkuu ambao ndio wanaowasaidia katika harakati za kuendesha hii Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kuhusu hali ya biashara ya Zanzibar na pato la taifa kwa sekta hii ya biashara. Kwa mwaka huu uliomalizika, inaonesha kuwa pato la taifa kupitia sekta hii limeanguka kidogo kuliko lilivyo kuwa mwaka 2012/2013. Hali hii wameieleza pengine kutokana na upungufu wa uwagiziaji wa bidhaa kama vile mitambo.

Kwa upande mwengine kwenye usafirishaji na uwagiziaji, umepanda kidogo na hali hii imesababishwa na kusafirisha karafuu, mwani na mazao mengine kwa wingi. Kwa hivyo, kwa hili nawapongeza kuwa wameweza kusafirisha bidhaa kwa wingi ukilinganisha na mwaka uliopita.

Kwa upande mmoja kuna upungufu wa uwagiziaji na huu unatokana na kupungua kwa kuagizia hizo bidhaa kubwa kama vile za mitambo hasa ya uwekaji wa umeme, lakini bidhaa za vyakula, vifaa vya ujenzi na magari bado viko pale pale. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa biashara ya vyakula haikupungua na vilivyopungua ni zile zana nzito au vifaa vyengine tunavyoagizia.

Kwa kweli vifaa vya ujenzi hatuna uwezo navyo kuzalisha ndani ya nchi yetu kwa sababu bado hatuna viwanda vya saruji wala vyuma na mengineyo, tutalazimika tuagizie kwa hali yoyote, kwa sababu tunaendelea. Sasa

bidhaa za vyakula ikiwemo mchele, sukari, unga na vyenginevyo, vyakula vya makopo inaonesha bado uagizaji huu haujapungua.

Hali hii ina maana nchi yetu bado haijaweza kwa kiwango kujitosheleza kwa vyakula ndani ya nchi, ingawaje uzalishaji wa vyakula si kazi yao, lakini kuna mambo yanakwenda katika *chain process*, hivyo lazima kuwepo na ushurikiano baina ya wizara moja na nyengine, ili hii *system* ikamilike na mwelekeo wetu uwe mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, wao si wazalishaji wa vyakula, lakini ni waagiziaji na kuna wengine ni wazalishaji lakini si waagiziaji. Sasa ili hali ya kuagiza vyakula ipungue, lazima hawa wanaozalisha waongeze uzalishaji, kwa ajili ya kupunguza fedha zetu kutoka ndani kwenda nje na tuongeze idadi ya fedha kutoka nje kuingia ndani ili kudhibiti hali ya uchumi. Sijui watakuwa na ushirikiano gani na Wizara ya Kilimo na Maliasili ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, nitazame kidogo kwenye ukurasa wa 12 uliozungumzia mwenendo wa bei ya karafuu na mwani. Karafuu ni moja katika mazao ya biashara ya nchi yetu na ndio zao pekee ambalo serikali haikubali kwa hali yoyote kulitoa, bidhaa nyengine zote wame-*surrender* waache wafanyabiashara binafsi waendeleze na hatimae wao kukusanya kodi tu, lakini karafuu serikali kwanini hawataki kuziachia.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani kama serikali ingeachia biashara hii na wao wakadhibiti yale mapato yao tu kama ilivyo biashara nyengine yoyote. Utalii tunaufanya kuwa unaingiza pesa kwa wingi lakini si serikali inaouendesha, serikali inadhibiti na kukusanya kodi tu za kitalii na kuwa utalii unachukua sehemu kubwa ya uchumi wa nchi, pamoja na kuwa serikali sio inayodhibiti lakini imewaachia sekta binafsi, wawekezaji wa ndani na nje wanaendesha na hatimae serikali inakusanya kodi. Inasemekana kama ingelikuwa serikali inakusanya kodi barabara hii sehemu ya utalii basi ingeliweza kuzalisha fedha nyingi zaidi kuliko inavyozalisha, lakini bado kuna mianya ya hapa na pale inayoachiwa.

Kwa hivyo, imani yangu mimi kama wanaamini zao hili ndio pekee lililobakia kuwa serikali hawataki kuliachia hebu wajaribu waliachie na waweke masharti kwa wafanyabiashara binafsi kuliendesha hili tuone. Mimi nadhani kama tulivyoweza kupata fedha nyingi kutokana na sekta ya utalii pia serikali inaweza kupata fedha nyingi kwa biashara hii pale ambapo wataiacha kwa wafanyabiashara binafsi waiendeshe.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine niseme kwenye hali ya viwanda. Nyuma kidogo kulikuwa na viwanda kadhaa hapa Zanzibar na nyuma sana kulikuwa na viwanda vichache tu kama Kiwanda cha Usumba, Viwanda vya Mafuta ya Nazi na Viwanda vya Soda. Kwa kipindi hicho ilikuwa viwanda hivi vinakwenda vizuri, lakini hatimae viwanda hivi kwa sababu moja au nyengine vilikufa fofofo, havipo tena. Sasa ni sababu zipi hasa za msingi zilizosababisha viwanda hivi kama cha Mafuta ya Nazi na Sabuni, Kiwanda cha Usumba kuwa vife?

Vile vile katika miaka ya 1960 - 1970 tulianzisha viwanda kadhaa vikiwemo Kiwanda cha Viatu, Kiwanda cha Sigara na vyenginevyo, navyo hatimae vilipotea. Sijui ni sababu zipi zilizotufanya tuanzishe, sababu zipi zilizotufanya baadae viwanda hivi tuviachie vife, na leo tunazungumzia tena juu ya ukuaji wa viwanda. Mimi nadhani hapa Zanzibar tunapoanzisha viwanda bado wafanyabiashara au serikali haijatoa taaluma juu ya mambo ya msingi ya kuanzisha kiwanda. Kiwanda ili kiwepo kuna mambo matatu ya msingi lazima yapatikane; kwanza kuwepo kwa wafanyakazi rahisi *cheap labors,* Zanzibar hili si tatizo kwa sababu wapo vijana wanaotafuta kazi.

Jengine ni vile vitu ambavyo vitatumika katika kutengeneza hicho ambacho tunataka tukitengeneze kwa mfano tulikuwa tuna kiwanda cha viatu, *row material* yake ilikuwa ni ngozi, je, tulifanya utafiti tukaona kwamba hatuna ngozi za kutosha za kiwanda hiki ili kiweze kuendelea kama hatuna ndio hatunayo unakuta tunaanza kitu baadae tunakosa mali ghafi na kiwanda kile kinapotea. Jengine ni njia ya usafiri; kusafirisha bidhaa kwenda kiwandani kupeleka katika masoko je, ile bidhaa tunayozalisha inasoko la hapa ndani na nje, au la hapa ndani tu?

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada Mhe. Mohammed.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mie naona dakika ishirini hazijatimia Mheshimiwa, je, tunayo masoko ya zile bidhaa ambazo tunazizalisha kwa sababu kama utazalisha bidhaa na hatimae ikawa haina soko biashara itakuwa haiendi na kiwanda hatimae kitakufa. Niiulize Wizara je, katika uanzishaji viwanda kuna utafiti wowote tunaofanya kuonesha kuwa hizi *conditions* za kuweka viwanda zipo *cheap labor, row material, transport na market* au tunaanzisha tu kwa kuwa tuna pesa zetu na watu wana pesa zao bila ya kufanya utafiti.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mageuzi ya Shirika la *ZSTC;* niipongeze Wizara kwa kutumia mageuzi hayo na inshaallah Shirika pengine litakwenda vizuri lakini shirika hili linashughulikia na ununuzi na usafirishaji wa karafuu, lakini hizi karafuu ili wao waweze kuzinunua kuna watu ambao wanazihudumia ndio hatimae zikawafikia wao. Kwanza ni mchumaji, mwengine ni tajiri mwenye hii mikarafuu, je, hawa wawili Shirika hili linawaangalia vipi, linawatunzaje ili waweze kuzitunza hizi karafuu na hatimae ziweze kuwafikia wao. Mimi huyu mchumaji naona bado hajatunzwa vyema pamoja na kuwa nadhani mchumaji analipwa shilingi elfu mbili kwa pishi anayoichuma ya karafuu lakini kulingana na ukuwaji wa mahitaji ya kila siku na matumizi ya nchi yalivyo na bei ya karafuu ilivyo bado huyu mchumaji kabwanwa kidogo.

Ningeiomba Serikali iwashawishi matajiri kwa kuwa bei wanayouza ni nzuri na huyo anayezitoa mpaka zikamfikia yeye tajiri na yeye aangaliwe zaidi badala ya elfu mbili aongezewe japo kidogo, ili na yeye aongeze juhudi ya kuzitafuta hizo karafuu katika mkarafuu. Lakini na pale ambapo atapata ajali Serikali imuangalie kama ilivyokuwa ikiangalia nyuma hapo kati kati, nadhani serikali ilikatisha kwa sababu karafuu haziuzwi nchini; hawatompa mtu fidia wakati unaambiwa Serikali haikupata faida, sasa Serikali inapata kwa hivyo ule utamaduni wa kuhudumia wale waliopata ajali ningeomba urejeshwe.

Mhe. Mwenyekiti, bidhaa tunazoagiza nyingine zinakosa viwango; bidhaa zetu nyingi wanazoleta ni zile *used* mafriji na mambo mengine hatimae yanakuwa ni majumba ya mende. Ningeomba Mhe. Mwenyekiti, serikali haiwezi kufanya utaratibu wa kuona kuwa mfanyabiasharara fulani anaingiza hivi vitu vya *used* kabla havijaingia nchini vikafanyiwa ukaguzi kuliko kuingia ikawa havifai sasa ikawa inatafutwa njia ya kuviangamiza. Yule mfanya biashara anapata hasara na lakini kama ingelikuwa tunadhibiti mapema kabla hajaviingiza akaambiwa shehe hivi usiingize nadhani ingelitusaidia.

Halafu naiomba Serikali keshokutwa tunaingia kwenye mfungo wa Ramadhani; tusaidie kuzungumza na wafanyabiashara pale ambapo kama hawatokuwa na hasara wapunguze kidogo faida ili watu wengi waweze kumudu hizi biashara zao, kununua kwa unafuu zaidi kuliko wanavyonunua hivi sasa. Lakini pale ambapo itakuwa hawapati hasara kwa sababu biashara lengo kubwa ni kupata faida kupata hasara ni bahati mbaya tu na aghalabu bidhaa kama hizi wafanyabiashara hawapati hasara *unless* ziharibike kwa sababu una-*calculate* ulivyonunua na unajua nikiuza hivi mimi nitapata faida. Kukosa faida ni pale biashara yako ambapo haitonunuliwa au kuambiwa kwamba imeharibika itakapoangamizwa. Lakini kwa njia nyengine yoyote mfanyabiashara hana mzigo, ni huyu mtu wa mwisho kwa lugha yenu mnamwita mlaji, kwa sababu mlaji ananunua kulingana na bei ambayo mfanyabiashara kaiweka; bei ambayo yeye hatopata hasara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nadhani dakika tano hazijamaliza niingie kidogo kwenye Idara ya Mipango Sera na Utafiti ukurasa wa 20, kuna jambo dogo tu nimegusiwa hapa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mohammed muda wako umekwisha na umeshazidishiwa dakika za ziada malizia.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Hapa pamegusia chumvi; chumvi huko nyuma ilikuwa na mzozo baina ya kilimo na mifugo na uvuvi, kilimo waliichukua kwa roho mbaya, lakini katika kitabu chao haikutajwa popote ni Waziri tu kaona haina baba wala haina mama yeye akajifanya awe ni mlezi wa chumvi, lakini kwa sababu Mhe. Waziri wa Biashara kaitaja nasema Mhe. Waziri wa Biashara chumvi ni yake, kwa sababu wote wawili wale chumvi hawakuitaja yeye ndio peke yake aliyeitaja kwa hivyo hii chumvi iwekwe kwenye wizara ya biashara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo machache nami naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa vile muda uliobakia ni mdogo mno hautoshi kwa watu kuendelea kuchangia jioni basi tutakapofika tunayo orodha ya watu sita ambao wanataka kuchangia, bado na wale ambao wanahitaji kuchangia tunaomba baadae waendelee kuleta majina. Kwa hivyo nitawataja majina ili waweze kufika mapema zaidi kuendelea na michangio yao. Wa kwanza ni Mhe. Panya Ali Abdala, akifuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Wanu Hafidh Ameir na Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa.

Baada ya maelekezo hayo sasa nasitisha shughuli za baraza hili hadi jioni saa 11.00.

(Saa 7.00 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: (Mhe. Mgeni Hassan Juma) Waheshimiwa Wajumbe msinione kimya isipokuwa nimepigwa na butwaa kidogo kwa sababu bado idadi yetu ni ndogo sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote sina budi na mimi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kutujaalia uhai tukaweza kukutana hapa jioni hii kuendelea na majukumu yetu. Pia nikushukuru wewe Mwenyekiti, kwa kunipa na mimi fursa niweze kusema machache katika hotuba hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri na Naibu Waziri na watendaji wao wote wa Wizara hii kwa ushirikiano wao ambao umeweza kutuletea hotuba hii ya mapato na matumizi ya mwaka huu wa fedha 2013/2014/2015. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli niseme sina mchango mkubwa leo isipokuwa mchango wangu ni kuunga mkono kwa asilimia mia moja Wizara hii. Kwa hivyo niseme machache yale ambayo niliyonayo nayo nitakwenda katika ukurasa wa 1987 ambao kuna majukumu ya Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa katika kitabu majukumu ya Wizara ni kusimamia kuwepo kwa mazingira mazuri ya biashara. Ninakubaliana na wao lakini waelewe Mheshimiwa mazingira mazuri ni pamoja na kuwa na maeneo ya kuwaweka wafanyabiashara wetu. Mhe. Mwenyekiti kwa kweli wafanyabiashara wetu wanajitahidi katika kuitikia wito wa serikali kwamba wajiajiri kwa sababu ya ukosefu wa ajira na jambo hili tuwashukuru wananchi na tuwapongeze wanalifanya. Lakini mazingira ya kufanya biashara yao kwa kweli hilo ni tatizo.

Tuseme wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanapika chapati, maandazi, yaani utawakuta wanapouzia biashara zao ni barabarani pengine mavumbi ya magari yaani hata yale mazingira ya yule mlaji basi hayaonekani kama ni mazuri. Kwa hivyo mimi niiombe serikali kwa kuwa wananchi wetu wanaitikia wito basi na sisi tujaribu kutafuta angalau sehemu nzuri za kuwaweka ili ile biashara yao basi iendane na yale mazingira hata yule mlaji asisite site kununua.

Pia serikali inapoamua labda kuwaondosha wafanyabiashara katika eneo lile ambalo wanafanyia biashara, serikali inapolihitaji ningeomba sana ingeweza pia kuwatafutia kwanza eneo jengine halafu ikawaweka wafanyabiashara wale, ili kuondosha ule usumbufu ambao unakuja kujitokeza katika serikali na wafanyabiashara. Tukiwafanyaia hivyo wanajiingizia wao wenyewe kipato lakini pia serikali nayo inakuza uchumi wake itakapokuwa na wafanyabiashara ambao wanafanya biashara zao kwa kutulia.

Mhe. Mwenyekiti, pia mimi mchango wangu niuelekeze katika ule ukuzaji wa wajasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli serikali ikijiandaa hasa na ikaweza kweli kutekeleza majukumu haya basi wajasiriamali hawa wanaweza wakafikia mahala pazuri. Mimi niseme basi serikali iwape elimu ya usarifu wa biashara zile, ili na biashara hizo zikiwemo mwani na dagaa kavu kwa sababu wafanyabiashara wanajitahidi, wapo waanikaji wa madagaa lakini wapo ambao wanashughulika na kilimo hiki cha mwani.

Sasa tukiweza kuwapatia elimu ile ya usarifu wakaweza kusarifu mwani ule wanaweza wakauza kwa bei itakayokuwa nzuri zaidi. Kwa sababu ndani ya mwani humo ninasikia kunapatikana vitu vya aina nyingi ambavyo wanaweza kuvitengeza. Kwa hivyo mimi niiombe tu serikali izidishe elimu hiyo kwa wafanyabiashara wetu hawa, ili waweze kupata mafanikio.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea katika majukumu ya Wizara pia Wizara inasema itasimamia ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini. Hili ni jambo muhimu sana na nalipongeza sana kwani tunaweza tukaona tunajitahidi kufanya biashara na pengine tukaona labda hazitoki au faida yetu ndogo lakini kumbe tumekosa ule ubora wenyewe wa biashara. Kwa hivyo serikali itakapolisimamia jambo hili tunaweza tukaona tuna wafanyabiashara wazuri ambao wanaweza wakanufaika katika biashara zao.

Pia Wizara inaeleza kwamba kutafuta masoko ndani na nje ya nchi. Hili hata sisi wajumbe tumekuwa tukiishauri serikali mara kwa mara, kwa sababu wafanyabiashara wanapofanya biashara wakawa hawana soko la kuuza pia wanaweza wakavunjika moyo. Lakini kama serikali itaweza kulisimamia jambo hili basi ninaamini wafanyabiashara hicho ndio kilio chao kikubwa.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika kukuza ujasiriamali ambapo mumeeleza mengi wenyewe hapa katika kitabu, sasa niombe mtakapowakuzisha hawa wajasiriamali basi ule mpango ambao mumesema kuandaa vigezo maalum kwa ajili ya uteuzi wa vikundi na miradi ya wajasiriamali vitakavyopewa kipaumbele basi Mheshimiwa niiombe sana serikali iwe makini kwa kuona tunavisaidia vikundi ambavyo vimetimiza vigezo na sio kuvipa tu vikundi kwa upendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika zao la karafuu. Nasema naipongeza sana serikali kwa kuunda kikosi kazi yaani *Task Force*. Mheshimiwa jambo hili limeweza sana kusaidia upunguzaji wa magendo ya karafuu. Kwa hivyo niiombe sana serikali iendelee na kubuni mbinu mbali mbali ambazo zitasaidia kulibakisha zao letu hili liendelee kuwapatia manufaa wananchi wake. Mheshimiwa juhudi ambazo imechukua *task force* imeonekana kwa hakika tumeweza kufuzu kidogo. Kwa hivyo bado muendeleze nguvu zenu.

Pia wenzangu wengi wameeleza kwamba wavunaji wetu wa karafuu kwamba karafuu hawazitendei haki kwa kuzianika mwahala chini labda au kwenye barabara, kweli hili si jambo zuri, elimu hii ni lazima tuwape wakulima kwa sababu tujuwe wanapozianika karafuu chini wao wenyewe wanajipunguzia soko kwa kuanguka *grade* ya karafuu yao, lakini hiyo serikali ambayo tunategemea tukapeleke zao hili nje ya nchi ambako kuna ushindani wa kibiashara basi pia waelewe inaweza ikawa tunaiangusha *grade* karafuu yetu. Kwa hivyo wajitahidi kuanika karafuu katika vifaa ambavyo vitakuwa vinakubalika ili kuiweka karafuu katika ubora wake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema niunge mkono tu hii hotuba kwa asilimia mia moja lakini mchango wangu ulikuwa ni mdogo sana, na ninawashukuru na ninawapongeza, ninawatakia kila la kheri yale ambayo mumeandaa humu ambayo yatatuongoza katika njia za kheri basi waweze kufanikiwa, ili na sisi tufaidike katika biashara zetu. Ahsante.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa furasa ya kuweza kuchangia mawili matatu katika bajeti hii ya Wizara yetu muhimu; Wizara ya biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichukuwe fursa hii baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nikushuru na wewe pia kwa kunipa fursa hii kwa kuzungumza. Pia niwapongeze Mhe. Waziri, Wizara ya biashara, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu wao kaka Julian Raphael pale.

Mhe. Waziri baada ya hapo niwapongeze wajumbe wenzangu pamoja na viongozi wa Chama cha Wananchi CUF ambao leo wako katika mkutano wao huko *inshaalla* wafanye mkutano wao kwa salama na watuletee viongozi wazuri sio kwa mazoea. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hatua hiyo sasa naomba kutamka rasmi kwamba bajeti Wizara hii naiunga mkono kwa asilimia 50, nabakisha asilimia 50 mpaka pale Mheshimiwa Waziri atakaponitosheleza kwa majibu ya kina hususan kwa kadhia ya wafanyabiashara wetu wa Zanzibar, ambao wanaendelea na shughuli zao za kibiashara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kwa kusema naona haya, naona aibu, naona fedheha hususan baada ya kuona kwamba kumekuwa na kuna utaratibu ambao si wa kisheria ni matakwa tu ya watu fulani kuamua kufanya vitu kwa maslahi yao lakini kwa kudhalilisha nchi na wafanyabiashara kwa ujumla, pasina kuwepo na sababu za msingi.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nilipo nina barua; barua hii Mhe. Mwenyekiti, amepelekewa Waziri wa Fedha na Uchumi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, juu ya kadhia ya wafanyabiashara wa Zanzibar ambao makontena yao yalikuwa yamezuiwa bandari ya Dar es Salaam. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa katika majumuisho yake anisaidie hawa wafanyabiashara wa Zanzibar wamekosa nini katika sheria zetu, wamekosa nini katika Katiba yetu na wamekosa nini katika utaratibu wa shughuli zetu hata ikabidi wanageuzwa kama watoto wa kambu waliokuwa hawana wazee wa kuweza kuwasaidia na kuwahakikishia kwamba usalama wa mambo yao na shughuli zao unakwenda katika utaratibu ambao unafaa.

Mhe. Mwenyekiti, makontena haya yamefika Zanzibar sasa hivi baada ya harakati kubwa ya serikali pamoja na viongozi mbali mbali, lakini kinachonisikitisha Mhe. Mwenyekiti, kontena hizi zimefika Zanzibar na *escort* ya watu ambo wamekuja kuhakiki nini kilichomo ndani ya kontena hizi. Ni jambo la kushangaza sana wakati Tanzania yetu tunafanya kazi ndani ya mfumo wa TRA mmoja, lakini tuna Naibu Kamishna ambae yuko Zanzibar akiwa na mamlaka kamili, akiwa na watendaji ambapo baadhi wametokea huko huko upande wa pili wa TRA. Lakini sasa wapo Zanzibar wanaendelea shughuli hizi, kwa sababu kitendo cha kuvuka maji kuja Zanzibar imekuwa sasa hawaaminiki TRA wa Zanzibar ndio waje na watu kutoka Bara ili kuja kusaidia kadhia hii. Mhe. Mwenyekiti, hili sikubaliani nalo, sikubaliani nalo kwa sababu ni kitendo ambacho kinamdhalilisha Naibu Kamishna wetu Ndugu Mcha.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba atakapokuja hapa Mhe. Waziri kwanza atoe *kalma* ya wale watu ambao wamekuja kutoka TRA kwa shughuli za biashara Zanzibar, wasiwe na jukumu la kufanya juu ya hilo. Wale ma-*officer* ambao wako hapa ndio wakamilishe taratibu hizi na wakamilishe mambo haya na kila kitu kiweze kutolewa taarifa zake na baadae ziende katika utaratibu tuliojiwekea. Sio kama mpaka atokezee mtu kutoka Bara ndipo aje kuhakiki vitu ambavyo viko pahala ambapo pana sheria zake, kuna na watendaji wake na kila kitu chake.

Mhe. Mwenyekiti, nitamuomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa mimi suala hili nitakuja kulizungumzia zaidi na kutaka ufafanuzi wake wa kisheria tutakapokuja kuzungumzia katika bajeti ya Wizara ya Fedha. Kwa sababu hii ndio Wizara ya Biashara na inashughulika na masuala ya biashara na walioadhibiwa ni wafanyabiashara, nitaomba Waziri wa Biashara niweze kujua yeye ameshiriki vipi, amesaidia vipi, kuhakikisha kwamba vijana wetu hawa na wafanyabiashara wetu wa Zanzibar wanaondokana na kadhia hii ambayo imejitokeza katika visiwa vyetu vya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia watu hawa wanakwenda kinyume mpaka na matakwa ya Katiba yetu. Katiba yetu kifungu cha 9(2)(a) kinazungumzia juu ya mamlaka ya kuendesha nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa serikali kufuatana na Katiba utatoka kwa wananchi wenyewe. Lakini kama hiyo haitoshi kifungu cha 10 sasa Mhe. Mwenyekiti, naomba kukariri pia;

“Kwa madhumuni ya kuendeleza umoja na maendeleo ya watu na ustawi wa jamii katika nchi itakuwa ni wajibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoa huduma za kutosha kwa ajili ya kuendeleza watu katika njia za mtu kuwa huru kwenda atakapo na kutoa huduma kwa watu wote na kutoa haki zote za kuishi kwa Mzanzibari sehemu zote za Zanzibar”.

(b) “Kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa cheo dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka”.

(c) “Kusimamia maendeleo ya uchumi wa nchi kufuatana na misingi na madhumuni yaliyowekwa na Katiba kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora, kuratibu na kusimamia uendeshaji wa raslimali muhimu za nchi”.

Sasa Mhe. Mwenyekiti mimi nashangaa hapa hawa wenzetu wanachokitaka ni nini? Wanataka hawa wafanyabiashara wasilete biashara zao hapa Zanzibar? Kama ambavyo wamekuwa wanawafuata baadhi ya wafanyabiashara na kuwaambia, kwa sababu wako wafanyabiashara wa Zanzibar ambao wanakwenda kufuatwa na hawa hawa maafisa wa TRA kuwaambia kwamba wasilete mzigo Zanzibar washushe mzigo upande wa pili wa muungano na waendeleze shughuli zao kule, hili si jambo zuri, wala si jambo jema.

Kwa sababu kwa mujibu wa makubaliano yetu mzigo wowote ambao unakwenda pahala pale ambapo itakuwa ni *final destination* unatakiwa ulipwe pale na baadae kuna taratibu za kuwekwa takwimu zinafuatwa. Mizigo hii ya wafanyabiashara *final destination* ni Zanzibar. Sasa leo kimezidi nini hata ikabidi lazima walipe bara, wakati ni *transit* tu pale na wameruhusu kwamba mzigo huu uje Zanzibar halafu tumeletewa maafisa 7 waje kuhakikisha, mambo haya ndio vipi! Kweli tunatumia ile nafasi na kweli tunatumia maana halisi ya muungano wetu. Kwa sababu muungano wetu katika mambo ya msingi moja ilikuwa ni kutumia soko la Tanzania Bara.

Sasa leo tukiwa tunafikia hali kama hii tutakuwa tunawasaidia wafanyabiashara wetu, wao wende wapi zaidi ya hapa kwao walipo. Kila kitu kiwe kinatokea mpaka aingilie Waziri wa Fedha, mpaka waingilie baadhi ya Watendaji Wakuu Zanzibar ndio mambo yatendeke, ndio maana yake nini! Wakati nchi ina sheria zake, ina Katiba zake na kuna kanuni zake.

Naomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe maelekezo ya kina juu ya kadhia hii ambayo inaendelea juu ya biashara na wafanyabiashara wetu wa Zanzibar, juu ya makontena 100 ambayo yamefika hapa.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, ninakuja katika suala la MTC. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa sababu suala hili ni la muda mrefu, leo kama sikupata majibu ambayo yatanitosheleza nitapunguza shilingi moja katika bajeti hii kwa ajili ya kutaka mustakbali na maamuzi juu ya suala la wale watendaji wa Shirika la Magari la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyakazi wale sasa hivi wamekuwa kama ni watu ambao wamefungwa pingu za mikono lakini hapo hapo wakatakiwa wende mbio, sasa watakwenda vipi mbio wakati wao tayari mumewafunga. Kama ilikuwa ni suala kwamba shirika limeshindwa kujiendesha na tukaona kuwa tayari imefikia pahala lile shirika

lifungwe sasa hivi ni mwaka wa nne watu wanatononeka hawawezi wao kujisaidia wala serikali haiwasaidii, matokezeo yake wanapata matatizo; maisha ni magumu, naomba kupata ufafanuzi katika suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, jengine vile vile hapa nilitaka kumuomba Mhe. Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ilikuwa na kazi yakuwasaidia watu wetu hususan akina mama kujishughulisha katika mambo ya ujasiriamali na kufanya biashara zao, ili waweze kupata rizki na wajisaidie katika maisha. Lakini Wizara ya Biashara sasa ndio yenye jukumu lakusimamia hususan suala zima la soko lile la Jumapili, ili wajasiriamali na wengineo waweze kuuza biashara zao na waweze kujisaidia kwa kujiongezea vipato vyao.

Sasa kulikoni hata lile soko la Jumapili tumeanza nalo kwa vishindo lakini sasa hivi limekuwa linasinzia sinzia. Mhe. Waziri kwa sababu sekta ya biashara ni yako nitaomba utakapokuja hapa unisaidie maelezo ya kina, ili niweze kufahamu ni kwa nini biashara ile ya Jumapili imeshindwa kwenda vizuri katika maeneo ya Kisonge.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa niende katika vifungu lakini kwa leo kutokana na kazi nzito ya hawa wafanyabiashara wenye makontena yao, naomba kuishia hapa hadi pale Mhe. Waziri atakaponipa neno ambalo litanitosheleza mimi na wafanyabiashara wa Zanzibar, juu ya kadhia hii ya kila siku kunyanyaswa kama watoto wa kambu wakati utaratibu huu unafanywa na utashi wa watu tu, si kwa sababu ya suala la Muungano, si kwa sababu ya sheria wala si kwa sababu ya Katiba ni utashi wa watu tu wanaamua kufanya hivi.

Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe jawabu lakini suala hili hili litaendelea tena katika Wizara ya Fedha na Uchumi. Baada ya maelekezo hayo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya wizara hii kwa asilimia 50 na asilimia 50 nasubiri majibu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi pia nimshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kuwa sote tupo katika hali ya uzima na afya njema. Pia nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuchangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwa mwaka 2014/2015.

Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi yake kubwa, jitihada kubwa anayoionesha katika wizara hii na niwapongeze watendaji wake wote kwa kazi yao hii wanaoifanya na kama tunavyojua wizara hii inagusa moja kwa moja jamii katika kazi zao za kila siku kwa kujipatia rizki zao.

Vile vile niwapongeze wajumbe wote wa kamati kwa kazi yao nzuri na kubwa kwenye ripoti yao waliotusomea hapa, nawapongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie kwenye ukurasa wa 14 kifungu Nam. 26 katika sekta ya viwanda bado inaendelea kuchangia chini ya asilimia 10 katika pato la taifa kupata ajira kwa wananchi wetu. Mhe. Mwenyekiti, sekta hii ya viwanda ni sekta muhimu na sekta nyeti kabisa ambayo inawapatia vijana wetu ajira ili waweze kupata rizki zao. Lakini kabla ya yote nimpongeze sana ndugu Said Salim Bakhresa kwa kazi yake kubwa na uwezo aliounesha kwa kipindi kifupi juzi juzi kuanzisha kiwanda cha maziwa hapa njia ya Fumba. Kwa kweli kiwanda hicho Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipata bahati yakwenda kuangalia, barabara pale kwenye kiwanda hicho alijenga kwa pesa zake. Kwa hivyo, mimi nampongeza sana kwa uwezo wake mkubwa na imani aliyoionesha kwa nchi yetu hii ili vijana wetu wapate ajira.

Mhe. Mwenyekiti, hii kazi ya viwanda ni kazi kubwa na pia kuna wafanyabiashara wengi wameanzisha viwanda hapa nao niwapongeze sana na wao kwa juhudi zao kubwa kama hiki Kiwanda cha *Cool* kinazalisha maji *director* wake ni Mhe. Turky, *Zainab Bottlers* nampongeza sana kwa juhudi zake kubwa kwa kuwapatia vijana wetu ajira, pia Kiwanda cha *Drop* nawapongeza sana kwa jitihada yao kubwa, na kiwanda cha soda.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme hawa wawekezaji wanakuja lakini kuna mazingira mengine serikali isaidie sana kuchangia hawa wawekezaji wapate nafuu. Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano mdogo suala la miundombinu. Mhe. Mwenyekiti, mfadhili huyu amejenga mwenyewe ile barabara kutoka pale kwenye kiwanda chake mpaka barabarani, ni fedha nyingi sana sijui hata milioni ngapi. Sasa wafadhili wengine Mhe. Mwenyekiti, wanakuwa hawawezi kujenga miundombinu kama hii, masuala ya umeme, maji safi na salama naiomba sana serikali kupitia Waziri wa Miundombinu hii iimarishwe kabla ya mwekezaji hajafika, itasaidia sana wawekezaji wetu kuweza kuekeza katika kisiwa hiki cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano mzuri sana kwa wajasiriamali wetu; juzi juzi hapa Mhe. Mussa Ali Hassan Mwakilishi wa Koani wananchi wake walitengeneza pilipili, achari kwa kazi zao walizofundishwa na serikali,

kwa kweli walikuwa wanafanya kazi nzuri na Mhe. Mussa kanambia hebu angalia hivi vitu, hebu nunua ujaribu. Mhe. Mwenyekiti, nikanunua vile vitu yaani vitu ni vizuri sana, nampongeza sana Mwakilishi wa Jimbo la Koani kuwatafutia soko. Mimi mwenyewe nimenunua na sasa hivi nimo kutafuta soko kwa watu wengine kuwaonesha wanunue vitu hivi, ili wananchi wetu wapate ajira na hili soko lao liweze kukua.

Kwa hiyo, naiomba wizara iweze kuwasaidia sana hawa wajasiriamali hawa wadogo wadogo kuwasaidia mitaji, tatizo kubwa ni soko vitu wameshatengeneza lakini soko la kuuzia hawana. Mfano mzuri nimekupa wananchi hawa wa Koani kupitia mwakilishi wao anawatafutia soko kwa waheshimiwa na wananchi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze serikali sana kwa kuondosha ushuru wa bidhaa za chakula kwani juhudi hii waliochukua ni kubwa ya kuwaondoshea watu hali ngumu ya maisha, kuweza kupata chakula chao cha kila siku hasa katika mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nisikitike sana niseme kuwa huu udhibiti wa vyakula Mhe. Waziri hebu uangalie vizuri, kwa sababu hawa wafanyabiashara unaweza leo ukenda dukani na pesa zako lakini unakuta bei imepanda ukimuuliza anakwambia hali ngumu, mambo yako hivi. Kwa hivyo, naomba hili soko Mhe. Waziri hebu liangalie hawa wafanyabiashara wasijiamulie tu kujipandishia bei; baadhi ya vitu maana yake ukiwauliza wanakwambia bahari sasa hivi imekuwa hivi, hali ngumu, mbatata bei juu, tungule bei juu, mboga mboga bei juu, soko linakuwa halipo vile kama kuna serikali yakudhibiti vyombo hivi bei zisipandishwe tu holehola Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia suala hili kama zamani tulikuwa na Shirika la Bizanje linauza mchele, sukari, na unga. Hata kama hawa wafanyabiashara wanaamua kupandisha bei lakini inakuwa haiwezekani kutokana na serikali kuwa na vyakula wameweka akiba wao wanauza kwa bei yao nzuri. Kwa hiyo, naiomba wizara iangalie sana suala hili kurejesha tena Shirika la Bizanje au shirika lolote lakini liwe la serikali, ili liweze kulimiliki hili soko hasa la vyakula lisiweze kupandishwa kiholehola, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye zao la karafuu katika ukurasa wa 12 kifungu Nam. 23. Mhe. Mwenyekiti, kwa wastani mwenendo wa bei ya mazao makuu yanayozalishwa Zanzibar na kuuzwa katika masoko ya dunia moja wapo ni zao la karafuu. Mhe. Mwenyekiti, niishukuru serikali kwa kuuza karafuu kwa kilo moja dola 11.5 kwa wananchi hasa wananchi wa Pemba wanafaidika kwa zao hili. Nikitizama asilimia 80 zinakwenda kwenye mfuko wa mwananchi, serikali inabakishwa na asilimia 20. Kwa hiyo, inakuwa serikali pato lake ni dogo.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana mpaka sasa hivi zao la karafuu duniani bado lipo na linaendelea vizuri, lakini tukitizama hili zao la karafuu ni la msimu sio zao la kila siku au kwa muda wa miezi ni mwaka mara moja, naweza kusema mwananchi anafaidika na zao hili au mara mbili, hivyo haliwezi kumtimizia mahitaji yake na serikali pia haiwezi kuingiza pato kwa asilimia 20 likasaidia kwenye nchi hii, inakuwa tabu na biashara itakuwa iko nusu nusu sio suala la kulitegemea sana zao hili. Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia takwimu uzalishaji wetu wa karafuu kwa mwaka tani ni 4200; kiwango kidogo sana ukitizama na hali zetu za maisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema serikali haitoweza kupunguza umasikini kwa kutegemea zao la karafuu, kwa sababu ukitizama faida yake ni ndogo kabisa na mkulima hafaidiki.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 12 kifungu Nam. 24 biashara naweza kusema ni uti wa mgongo wa wananchi wa Zanzibar hasa kwa sasa hivi, pato kubwa sana wananchi wanafaidika na biashara ndogo ndogo na biashara kubwa. Katika ukurasa huo Mhe. Waziri kuhusu ongezeko la biashara uingizaji na utoaji wa makontena katika bandari ya Malindi Zanzibar, naishukuru kwanza serikali na naipongeza sana kwa juhudi kubwa wanajitahidi kujaribu biashara iongezeke sana Zanzibar ili wananchi wapate kufaidika. Lakini nina masikitiko makubwa Mhe. Mwenyekiti na Mhe. Waziri uliangalie hili, ukitizama bandari yetu kwanza kuna ufinyu wa nafasi, vifaa vyenyewe haviko sawa na vyakutosha na ukitizama msongomano mkubwa wa makontena bandarini hata kuleta Bwawani na kurejesha wale wafanyakazi wanapata tabu sana kuweza kuhimili vishindo hivi. Mhe. Mwenyekiti, ukitizama hata hali yao ya ufanyaji wa kazi unakuwa unachelewa na unachukua muda mrefu kabisa.

Kwa hiyo, mimi naomba sana Mhe. Waziri kupitia serikali uangalie yale mabanda yaliyokuwa pale bandarini yavunjwe yale ili makontena yaweze kukaa kwa haraka na yaweze kuondoka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kipindi cha nyuma nilikuwa Dubai nilipakia kontena yangu nikaambiwa ukitaka kupeleka Zanzibar kontena utalipa dola 2200, ukitaka kupeleka Dar es Salaam kontena hilo hilo utalipa dola 1700 na ukitizama unauliza Zanzibar kontena itafika muda gani, unaambiwa itafika muda wa wiki tatu mpaka nne, lakini

Dar es Salaam unaambiwa siku kumi tu kontena hili litafika. Kwa hivyo, hii inachangia sana kutoleta biashara Zanzibar na wananchi wanapata matatizo makubwa kama alivyoelezea mwenyekiti wangu matatizo ya wafanyabiashara wetu, wanahangaika sana.

Mhe. Mwenyekiti, makontena haya yanayokuja Zanzibar ni makontena muhimu ambayo yanaleta vifaa vya ujenzi, chakula, vifaa vya umeme na bidhaa mbali mbali ambazo ni muhimu sana zinatakiwa zifike kwa haraka katika nchi hii, na wafanyabiashara wengi wanafanya biashara hizi. Niseme serikali ina nia njema nakubali hilo, na nina imani hivyo kipindi sio kirefu sana kuna mpango wa kujenga gati ya Mpigaduri. Lakini bado nasema gati ile haitojengwa leo na kesho na tukiangalia bandari yetu hii tutapoteza mwelekeo, tutapoteza wafanyabiashara wetu kwa ajili ya kucheleweshwa makontena yao Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hiyo, Mhe. Waziri naomba uangalie sana kabla ya kujenga bandari hii kwanza tuboreshe bandari yetu ile na biashara yetu iende vizuri na wafanyabiashara wafaidike na makontena yao yafike kwa haraka kabisa, tukisubiri gati ya Mpigaduri kila siku tutapoteza mwelekeo wa biashara.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema hivi ukitizama takwimu karibu vijana 100,000 wanaohitimu masomo katika vyuo mbali mbali wanahitaji ajira na uwezo wa serikali haupo, wataajiriwa sana vijana 5,000, 6000 lakini hawawezi kuajiri vijana 100,000 sasa vijana hao wengi wanajishughulisha na biashara. Mhe. Mwenyekiti, mfano mzuri wafanyabiashara wetu Darajani pale wanauza tende, halua ukitizama wale masikini ya Mungu wanahangaika sana Mhe. Waziri na ukitizama kipato chao ni kidogo na ukitizama saa nyengine wanaondoshwa kwa mabunduki, hivyo wanatia imani sana.

Mhe. Waziri naomba uwaangalie sana vijana hawa kwa sababu ndio ajira zao ziko pale, sasa hivi utakuta wanafanyabiashara vizuri lakini kuna muda unakuja wanaondoshwa wote. Sasa naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Waziri wale ni wadau wako, uwaangalie kwa jicho la huruma kabisa, ujue utawaweka wapi pahala ambapo wataweza kufanya biashara zao. Mhe. Mwenyekiti, ukisema uwapeleke Saateni kule biashara inakuwa ndogo na wateja wanakuwa hawapati kwenda kule vizuri kwenda kununua bidhaa zao.

Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri uliangalie sana suala hili wale wafanyabiashara wadogo wadogo wajengewe mazingira mazuri ama pale pajengwe *moll* moja kubwa *shopping center*, wawekwe pale wafanyabiashara wadogo wadogo wasaidiwe kupitia Serikali yao ya Mapinduzi. Mhe. Waziri naomba hilo uliangalie sana kwa wafanyabiashara wale.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitoe mfano mmoja mzuri nakuamini kabisa Mhe. Waziri na watendaji wako na unaujua na unafahamu vizuri biashara ya Zanzibar inavyokwenda. Mimi katika miaka ya 1996 nakumbuka nilikuwa nahitaji *certificate* ya *Zanzibar Chamber of Commerce* nikenda kwenye sekta hii nikamkuta Mhe. Waziri yeye ndie mwenyekiti na mimi nikaomba uanachama ule, ili niweze kupata *visa* yakwenda Marekani kufanyabiashara. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Waziri alinisaidia nikapata *certificate* ile na mpaka imenisaidia kufikia hapa, Mheshimiwa nashukuru sana yeye alinisaidia na ameniamini kama naweza kufanya biashara. Kwa hiyo, naamini yeye ni mdau mkubwa na anajua tatizo kubwa la biashara Zanzibar; kwa nini imeshuka na vipi ipande yeye Mhe. Waziri anajua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niseme kitu kimoja katika suala hili la kutizama biashara vipi imepanda na vipi imeshuka. Suala hili mimi niseme vizuri kabisa linachangiwa sana na bidhaa zetu zinavyokuja hapa Zanzibar halafu inakuwa lile soko kulipata ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, mfano mzuri nikupe hawa wafanyabiashara wetu utakuta wanafanya biashara lakini wanakula hasara, hasara vipi wanakula? Huwa wanaagiza bidhaa kutoka nje zinakuja hapa wanalipa ushuru pale wakishakulipa ushuru pale *TRA* wanachukua ule mzigo wakitoa bidhaa ile kupeleka Dar es Salaam wanalipishwa tena ushuru bandarini pale.

Sasa Mhe. Waziri mimi nilikuwa nakuomba sana wewe ni mdau mkubwa wa biashara Zanzibar kama nilivyotoa mfano. Kwa hiyo, naomba usaidie suala hili, wasilipishwe ushuru tena mara ya pili kama kulipa walipe hapa hapa, kwani hapa kuna ushuru Mhe. Mwenyekiti, kuna ushuru wa *ZRB*, kuna ushuru wa *TRA*. *TRA* bandarini wanalipa wakienda Dar es Salaam wanalipishwa tena unaambiwa kule ushuru wenu ni mdogo. Kwa hiyo, naomba Mhe. Waziri umsaidie Waziri wa Fedha, tusaidiane suala hili muweze kuondosha hii kero hizi za Muungano nilizosema.

Mhe. Mwenyekiti, mfanyabiashara ukitizama asilimia ngapi atapata faida ameshaagiza mzigo, duka amekodi, umeme analipa, alipe wafanyakazi, alipe gharama mbali mbali za dukani kwake kwa kweli hata akipata faida basi anapata faida asilimia 20 katika hiyo biashara yake.

Mhe. Waziri nitoe mfano mwengine mzuri kabisa, nilikopa pesa katika Benki ya *FBME* milioni 80 katika miaka ya 2008, lakini nikaja mpaka kwenye mwaka 2011 mkopo ule nimeurejesha kwa hiari yangu kwa sababu niliogopa nisije nikapata hasara nikaja kuuza vitu vyangu kwa ajili ya mkopo ule. Nikawarejeshea pesa zao kule benki zote kwa sababu biashara imeshuka na kweli Mhe. Waziri unafahamu biashara imeshuka Zanzibar kipindi hiki tunachokwenda, bidhaa zipo lakini wateja wa kuja kununua hawapatikani. Wakitoka hapa huenda Bara kwenda kuuza, ukitizama mikopo uliyokopa ukitaka ulipe faida kwanza ulipe riba ya benki, hivyo haiwezi kulipa wafanyabiashara, watafilisika tu akitaka asitake hasa biashara hizi kama za nguo zimekufa sana. Utakuta bidhaa ziko bei juu ukienda China bidhaa ziko chini sana, ukija hapa bidhaa ziko juu.Kwa hiyo, haziwezi kukidhi hawa wafnayabiashara wetu kurejesha pesa zao kwa faida nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, tuseme ukichukua bidhaa ukitoka nazo hapa mfanyabiashara mdogo aende akauze Tanzania Bara. Mimi mwenyewe binafsi nimeona suala hilo bandarini pale anakuja mfanyabiashara kutoka Zanzibar analipishwa friji moja 70,000 tena *used*, analipishwa *TV* elfu 15, 000, unafkiri itamlipa?

Mhe. Waziri, naomba hili uliangalie sana haya masuala ya gari hawa wafanyabiashara wetu wanaotoka hapa kwenda kuuza kule hawapati faida yoyote, nakuomba kwani wewe ni mdau mkubwa unaweza kulitetea suala ili kutafuta ufumbuzi mzuri.

Mhe. Mwenyekiti, niseme hizi zote ni kero za Muungano tunajua haya mambo yanatatulika tunaweza kukaa pamoja tukayatatua lakini mimi niseme kwa nia njema kabisa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete, kwa nia njema ameanzisha Bunge la Katiba ili hizi kero zote za Muungano tuzimalize hapa, lakini kwa masikitiko makubwa hawa wenzetu Mhe. Waziri pia na wewe umo mumeondoka kwenye Bunge la Katiba, na pale ilikuwa ni sehemu nzuri ya kutetea wananchi wetu na kufungua hii milango yao tuweze kuyamaliza haya matatizo yetu.

Mumeondoka mumetuachia peke yetu, sasa haya matatizo tutaweza vipi kumaliza peke yetu, tena tuna nia njema sote kwa Zanzibar, lakini na nyinyi muwepo, na sisi tuwepo tuweze kutatua haya matatizo yetu yote kwa nia njema kwa ajili ya wananchi wetu kupata vipato vyao vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimalizie kwa ukurasa wa 57 wizara imepata kukusanya shilingi milioni 100 kutokana na kazi za ukaguzi wa mizani, upimaji na hasa vituo vya mafuta.

Mimi nataka niipongeze sana wizara kwa kukusanya shilingi milioni 100 kutokana na vianzio mbali mbali vya mapato, lakini pia niwapongeze wafanyabiashara wakubwa hasa vituo vya petroli kama hawa *GAPCO*, *United Petroleum* na *Zanzibar Petroleum*. Hawa ni wafanyabiashara wakubwa na wanaingiza pato kubwa, tukiongeza wafanyabiashara kama hawa watatusaidia sana katika kuwapa ajira vijana wetu na kuweza kupata vipato vyao vya kila siku ili kukidhi maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja lakini ninachomuomba Mhe. Waziri yeye ni mdau mkubwa, na anafahamu nini tatizo la wafanyabiashara wetu wanalolalamikia, kila siku wanashuka chini badala ya kupanda katika kipato chao.

Kwa hiyo, naomba suala hili alifuatilie kwa umakini, mimi sina matatizo na bajeti yake, najua yeye ni makini kabisa, masuala ya biashara anayafahamu. Kwa hivyo, naomba masuala niliyouliza ayafuatilie kwa kina, ili tuweze kuwaondoshea matatizo wananchi wetu, hasa hawa wafanyabiashara. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.
Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe sasa nimwite Mhe. Fatma Mbarouk Said na atafuatiwa na Mhe. Wanu Hafidh Ameir.

Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Wanu Hafidh Ameir ni mchangiaji wa mwisho katika *list* yangu, kwa hiyo, ningeomba kama kutakuwa na mwengine yeyote anataka kuchangia alete maombi yake hapa au kama hakuna itabidi tuakhirishe kikao baada ya hapo na kumuachia Waziri aende akafanye majumuisho tutarudi kesho. Ahsanteni.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii nikachangia machache katika hotuba hii ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli wizara hii ni wizara muhimu na ni wizara yenye majukumu mazito kwamba ni wizara ambayo inaendesha na kusimamia biashara, usafirishaji wa bidhaa pamoja na uagiziaji. Vile vile kuna sekta mbali mbali katika kitabu hiki Mhe. Waziri ametuwasilishia, lakini kama kawaida ya Wajumbe wako humu ndani ni kazi yetu kujadili na kupitisha bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi sitakuwa na mengi ya kuchangia kwenye kitabu hiki ni kusema kwamba, kabla ya yote naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja kama wenzangu walivyosema. Ingawaje jana kwenye semina tuliambiwa kwamba kwenye miswada ni lazima tuifikishe kwa wenyewe wananchi, ili kujadili nao pamoja na isiwe tunasema tu kwa niaba ya watu wangu naunga mkono kwa asilimia fulani wakati hata hatujakaa nao.

Kwa hivyo, tujenge utamaduni huo wa kukaa pamoja na wenzetu ambao wametuchagua na waweze kutoa maoni yao, ingawaje ni tatizo kwa sababu unaweza kumwambia mtu jambo la kisheria yeye mwenyewe sheria haijui, sijui atakwambia nini, kwa hivyo, hilo ni jambo la msingi kabisa ambalo sasa tunakwenda kwenye mabadiliko hayo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa nne (4) wa hotuba hii ya bajeti ambako kuna mwenendo wa biashara. Mhe. Waziri ametwambia katika hotuba yake hii kwamba kwa mwaka 2013/2014 aliliarifu Baraza hili kuendelea kuyumba kwa uchumi wa biashara duniani kutokana na sababu mbali mbali; zikiwemo kudorora kwa uchumi wa nchi za magharibi na migogoro ya kisiasa.

Hali ya mwenendo wa uchumi wa dunia na biashara bado haijatengamaa, kwa kweli hili ni tatizo ambalo tunalo kwamba uchumi wetu unategemeana na hasa hayo mambo yote ya kibiashara na wenzetu ulimwenguni, namna gani wako katika hali ya kuendeleza hizi biashara.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na usafirishaji wa bidhaa Mhe. Waziri ametwambia hapa kwamba kiwango cha usafirishaji wa bidhaa duniani kilifikia US$ 18,794 bilioni kwa mwaka 2013 kutoka US$ 17,849 bilioni ikilinganishwa na mwaka 2012, ni ongezeko la asilimia 5.3.

Kwa upande wa usafirishaji wa huduma ulifikia US$ 4,625 bilioni. Niseme kwamba kidogo inaonekana usafirishaji wa bidhaa pia nao umeshuka si mzuri wa kusema kwamba tumepata mafanikio.

Vile vile nikienda kwenye ukurasa wa sita (6) anasema hali ya biashara Zanzibar, kwamba pia mchango wa sekta ya biashara katika pato la taifa ulikuwa ni asilimia 9.3 kutoka asilimia 9.5 na ukuaji wa sekta hiyo ya biashara mchango wake umepungua kutoka asilimia 10.2. Nataka nimuulize Mhe. Waziri ni sababu gani ambazo asilimia hizo zilifikia kiasi hicho?

Pia Mhe. Mwenyekiti, nikienda kwenye ukurasa wa 31 Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji wa Wajasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, ujasiriamali ni jambo la kuwasaidia hawa wajasiriamali wenyewe, kwa sababu tunawaona wajasiriamali wengi lakini uwezo wao ni mdogo. Kwa hivyo, ni lazima wizara hii iweze kuwatafuta na kuwakusanya pamoja au kuwawezesha ili waweze kujiendesha wao wenyewe na kuwahamasisha pamoja na kuwapa elimu.

Vile vile nimeona niunge mkono hii kamati kwamba kuna mambo mengi ambayo wameyaona kama kamati na wametoa mapendekezo. Kwanza ni kwenye hii Idara ya Mipango na Sera fedha za washirika kutopatikana mahesabu yake.

Kwa kweli fedha hizi za washirika ambazo wanatusaidia kutokupatikana mahesabu yake inakuwa ni tatizo kubwa. Vile vile kuna uhaba wa wataalamu kamati imesema, nafikiri kama tutakuwa tunataka kufanya kazi za kweli na mafanikio basi lazima tuwe na utaalamu. Kwa hivyo, hapa Mhe. Waziri kama nafasi anayo ya kuajiri wataalamu, na ni lazima wataalamu wawepo basi hili ni tatizo, pahala panapotaka kutumika utaalamu ni lazima patumike utaalamu, na sasa hivi kuna hii sayansi na teknolojia ni lazima tutumie vifaa vya kisasa, kama hatukuwa na utaalamu basi tutashindwa hata kuweka zile *database* zetu na mambo mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, niishukuru Idara ya Biashara na Uendeshaji wa Masoko ambayo ilikadiriwa kukusanya shilingi milioni 90 kwa mwaka 2013. Kwa kweli makusanyo yake yalikuwa si kidogo ni mazuri tu, kwa hivyo, yote hii ni kwamba waliwajibika vizuri, hivyo niwapongeze sana kwa kukusanya fedha hizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo moja ambalo nimeliona kwenye hivi viwanda kwenye Idara ya Maendeleo ya Viwanda. Kuna Kiwanda cha Sukari ambacho sasa hivi kuna changamoto nyingi ambazo zinawakuta.

Kwanza kutokabidhiwa nyumba za shirika. Kwa kweli kama kiwanda kile tokea mwanzo kilipokuwa kinafanya kazi huko nyuma kilikuwa na nyumba zake, na nyumba hizi mpaka hii leo kama ni mali ya kiwanda ni lazima wakabidhiwe. Kwa hivyo, tusifanye kitu ambacho kitamfanya huyu mwekezaji tukamchosha, tufanye uadilifu ili zile nyumba aweze kuzipata mwenyewe na kuweka wafanyakazi wake.

Kwa hivyo, hili ni jambo ambalo pia ni changamoto kwake yeye, kwa sababu anataka kufanya kazi lakini ukitizama katika zile *asset* zake ambazo zitamfanya mwenyewe aweze kufanya kazi vizuri, kwa sababu bila ya kuwepo na wale wafanyakazi karibu yake vile vile ni usumbufu. Tukifanya hivyo basi tujue kwamba tutakosa yale mapato au ule mchango mkubwa wa kuchangia pato la Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo jengine ambalo kamati walisema, kushindwa kulipa deni kwa wakulima wa karafuu. Nimuulize Mhe. Waziri hapa kuna utaratibu gani ambao sasa utafanywa ili wakulima hawa waweze kulipwa deni hili.

Nikiendelea kwenye kitabu hiki kikubwa *Vote Book*, nimeona kwamba kuna kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba, kifungu kidogo 220105, Vifaa vya Uchapaji hakijapangiwa shilingi kutoka mwaka 2011 mpaka hapa 2015. Mhe. Waziri atapokuja aniambie kwa nini kifungu hiki 0301 Ofisi Kuu Pemba hakikupangiwa pesa tokea mwaka 2011 mpaka 2015.

Vile vile kuna fungu 0401 Mipango na Sera kifungu kidogo 211104, Malipo ya Likizo. Kifungu hiki kwa mwaka wa tatu sasa hamna fedha za likizo. Je, hawa watu hawaendi likizo? Mhe. Waziri atwambie ni kwa nini, kama hawakwenda likizo hizi Sheria za Utumishi hazikiukwi? Kwa sababu naona kwa miaka mitatu hakuna fedha ya likizo na katika moja ya haki ya mfanyakazi basi ni kwenda likizo na kupata hizi fedha za likizo.
Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba tumo katika kutumia sayansi na teknolojia au niseme sijui kama wizara imeshaanza kutumia huduma ya elektroniki, kwani fungu 22010 Gharama za Vifaa vya Mawasiliano hivi vifungu vidogo kama gharama za simu, kuna *nil balance* tokea mwaka 2012 mpaka 2015 gharama za matangazo hamna kwa mwaka huu, tunajenga hofu.

Mhe. Waziri atakapokuja kwenye majumuisho aniambie ni kwa nini hata hivi vifungu kama gharama za matangazo, kwa sababu gharama za matangazo ni lazima, na mara nyingi huona matangazo hasa kupitia Shirika letu la Magazeti ambalo linajiendesha kibiashara, tunaona kwamba kuna taasisi nyingi huwa zinakopa na ndio chanzo chake cha mapato shirika lile.

Pia kifungu 220108 Huduma za *Internet*, pia kina *nil* miaka mitatu sasa, nipate maelezo atapokuja Mhe. Waziri ni kwa nini vifungu hivyo havikutiwa pesa.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi ina jukumu la kuweka mazingira mazuri ya kufanya kazi, kuendeleza rasilimali watu, kutunza majengo ya wizara na kutekeleza masuala yanayohusiana na Utumishi.

Kati ya malengo waliyojipangia kwa mwaka 2014/2015 ni ukarabati wa majengo. Sasa nataka nimuulize Mhe. Waziri fungu 220700 Matengenezo ya Ofisi, kifungu kidogo 220701 Matengenezo Madogo ya Ofisi na kifungu kidogo 220702 Matengenezo Makubwa ya Ofisi kwa mwaka 2013/2014. Mhe. Waziri anambie upatikanaji wa fedha hizo ambazo zilikuwa shilingi 160,000,000 ni kiasi gani ambazo zilipatikana kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine la kusikitisha tunaambiwa kwamba Kiwanda cha *Coca-Cola* kusitishwa. Kwa kweli ni hasara kubwa ambayo serikali imepata, ninaiomba wizara itupe ukweli wa suala hili tusidanganywe, sote humu ni watu wazima na tunawakilisha wananchi, kuvutana kwao taasisi na taasisi au mtendaji na mtendaji ndiko kulikopelekea kwa mwekezaji kung'oa mitambo yake, na sasa sina uhakika lakini nimesikia kwamba kang'oa mitambo yake na yuko Bagamoyo. Sasa tumekosa mtoto na maji ya moto, hivi tutafika wapi sisi kwa mtindo huu, ni wananchi wangapi sasa wamekosa ajira.

Mhe. Waziri atwambie ukweli ni kitu gani ambacho kimemfanya mwekezaji yule kuondoa mitambo yake. Kwa sababu tunasikia sikia tu, maana kwenye zile taasisi ambazo zinashughulika na mambo ya uwekezaji pia tumekwenda.

Sasa kama kulikuwa na mvutano labda wa kodi tumekosa mangapi sasa, kwa sababu yeye kaenda pale alipokwenda kodi kwa mwaka imeshuka, kaona bora niende kule kuliko hapa ambapo watu walikuwa wanavutana. Kwa hivyo, tumekosa yote kwa kweli, tumekosa ajira kwa wananchi wetu.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba kuunga mkono. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, na mimi niungane na wenzangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kukutana hapa leo kujadili hotuba ya Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

La pili Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii na mimi kusema machache katika hotuba hii. Kwa kweli sitokuwa na mengi nimesimama angalau kutia baraka katika bajeti hii, lakini pia kama nisingesimama nisingeitendea haki wizara yangu ambayo nilikuwa naitumikia kabla ya kuingia katika siasa.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nikiwa napitia kitabu hichi nilikuwa napata shida sana. Kwanza nilikuwa naona mbona Mhe. Waziri ametuwekea tu malengo ya 2012/2013, lakini Mhe. Mwenyekiti, leo nakubali kwamba kila mtu ana *style* yake ya kuwasilisha, wengine wanaanza chini wanakuja juu, wengine wanaanza juu wanakuja chini.

Wakati napitia kitabu hichi mbele kabisa nikaona kwamba Mhe. Waziri kumbe ameweka yale malengo ambayo anatarajia kutimiza katika mwaka huu wa 2014/2015, pamoja na kwamba tayari alishatoa shukrani kwa watu ambao alishirikiana nao katika kufanikisha kazi ambazo anazitekeleza, lakini mwisho wa yote nilifahamu lile ambalo Mhe. Waziri amelikusudia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanzia mimi nitaanza na ukurasa wa 31 Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Ukuzaji Ujasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza idara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya kwa kuona kwamba tunakuwa na viwanda ambavyo vinaendana na mahitaji yetu. Na wamekwenda mbali zaidi kwa kufanya utambuzi wa viwanda vile ambavyo tunahisi tungevipa vipaumbele Zanzibar na vikawa na manufaa kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika idara hii kuna kitu tu ambacho nilikuwa nataka nipate *attention* ya Mhe. Waziri, kwamba siku hizi kumekuwa na ongezeko kubwa sana la viwanda vya maji vinavyozalisha *pure water.* Yaani kumekuwa na maji mengi sana kwamba kuna kila aina ya maji hujui hata unywe yepi. Ukishika haya kuna yale, ukishika yale kuna mengine. Kwa hivyo, ushauri wangu kwa Waziri nilikuwa namuomba tu hawa wawekezaji wanapokuja kwa nini asishauri kwamba kukawa kunaanzishwa viwanda vya kusarifu mazao ya kilimo kuliko hivi viwanda vya sasa ambavyo vinazalisha maji?

Viwanda vya maji vimeshatosha, kwa hivyo ni vyema wanapokuja hawa wawekezaji, aidha hawa wazalendo au wa nje wakawashauri kuanzisha hivi viwanda vya kusarifu mazao. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, siku hizi tunapozidiwa kidogo tu na mazao kwa mfano kama machungwa au matikiti unakuta yamezagaa sana. Wakati kama kungekuwa na viwanda vinavyosarifu mazao angalau ingekuwa kuna manufaa ya mazao haya.

Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza na viwanda kidogo kulikuwa kuna taarifa ya kuwa kuna mwekezaji ambaye anataka kuanzisha Kiwanda cha Sukari Micheweni Pemba. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka kujua tu wizara inamsaidiaje mwekezaji huyu, ili kuona kwamba ule urasimu wa mwekezaji huyu kutaka kuanzisha huu uwekezaji unapungua.

Pia nilikuwa nataka kujua Serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imejipanga vipi kuona kwamba changamoto zinazojitokeza katika Kiwanda cha Sukari sasa, haziji kujitokeza baadae wakati mwekezaji huyu anapotaka kuja kuanzisha hichi kiwanda kwa upande wa Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niingie kwenye Taasisi ya Viwango *(ZBS).* Mhe. Mwenyekiti, mimi nakumbuka hapa nilishawahi kusema nafikiri nilikuwa namuuliza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora katika swali la nyongeza. Nilimuuliza kwamba kwa nini Serikali inapotaka kuanzisha jambo inakuwa haijipangi kwanza ili kutengeneza mazingira mazuri ya kuanzisha lile jambo halafu ndio inaanzisha.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu inaonekana Taasisi ya Viwango kwa kweli bado haijatulia, haijaanza kufanya kazi zake vizuri kama inavyotakiwa. Na hii yote ni kwa sababu kwanza haina jengo la kudumu, lakini pia inakosa hata maabara ya ku-*test* vile vitu ambavyo inaangalia viwango vyake. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa narudia tena kusema kwamba Serikali inapotaka kuanzisha jambo ni bora ikajipanga kwanza kabla haijaanzisha lile jambo, ili isiwe kwamba tunaanzisha mambo halafu inaonekana yale yanayoanzishwa hayafanyi kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikuwa nataka kujua hii Taasisi ya Viwango na Bodi ya Chakula na Vipodozi zinafanya kazi vipi, yaani ni jinsi gani taasisi hizi mbili zina-*link* ili kuona kwamba zile biashara ambazo zinaingia hazina madhara kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu hivi sasa na wenzangu mashahidi akinamama wamekuwa wakiathirika sana na vipodozi katika sehemu za ngozi na baadae hata kupata *cancer*. Kwa sababu hivi vipodozi vinaingia vinakuwa *supplied* na ndio maana akinamama wanavipata kupitia huko madukani.

Kwa hivyo, nilikuwa nataka kujua tu ni jinsi gani taasisi hizi mbili zinafanya kazi ili kuona kwamba vipodozi hivi haviwi *supplied* sana madukani, na vinazuiliwa kabla ya kuingia na kuona kwamba akinamama wenzangu wa Zanzibar wanakuwa wapo salama katika kutumia hivi vipodozi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ukurasa wa 36 katika kutekeleza lengo ambalo Taasisi ya Viwango imejipangia ni "Kuandaa viwango vya bidhaa mbali mbali na kutoa elimu kwa wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji wa bidhaa".
Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza lengo hili taasisi imefanya mambo yafuatayo:

1. Kuunda kamati 10 za kitaalamu kwa ajili ya kuzingatia mapendekezo ya viwango."

Mhe. Mwenyekiti, hizi kamati 10 kidogo nilikuwa naomba maelezo. Kamati hizi 10 zote zinafanya kazi ya kuzingatia mapendekezo ya viwango tu au vipi, lakini nilikuwa najiuliza kama ni kamati 10 za mapendekezo ya viwango, hizi kamati zote 10 zitakuwa zinafanya kazi moja. Mimi hapa mantiki ya kuwa na kamati 10 ambazo zinazingatia mapendekezo ya viwango nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija anielezee.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kidogo nilikuwa nataka ufafanuzi katika Baraza la Biashara ukurasa wa 38. Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Biashara kama nakumbuka vizuri ilikuwa na nia njema tu ya kuanzisha Mabaraza ya Biashara katika *level* za wilaya.

Nilikuwa nataka kujua tu hili suala limefikia wapi kwa sababu *level* ya Taifa sio wafanyabiashara sana, wanaonufaika na Baraza lile ni wale wafanyabiashara wakubwa wakubwa, lakini kuna wafanyabiashara wa kati na wadogo ambao hawanufaiki ipasavyo na hili Baraza. Kwa hivyo, nilikuwa naomba kuuliza kwamba ile nia ya kuanzisha Mabaraza ya Biashara katika wilaya imefikia wapi, ili kuona kwamba wafanyabiashara wa kati na wadogo nao pia wananufaika na uanzishwaji wa Baraza hili.

Lakini la pili, Mhe. Waziri wakati anawasilisha hotuba yake ameelezea tu malengo na utekelezaji, pia ameelezea malengo ambayo wamejipangia Baraza mwaka 2014/2015. Hatujaona mafanikio gani ambayo wafanyabiashara lakini na Zanzibar kwa ujumla wanapata kutokana na uundwaji wa Baraza hili.

Nilikuwa naomba Mhe. Waziri akija kufanya majumuisho atuelezee japo kidogo ni mafanikio gani yamepatikana kutokana na uanzishwaji wa Baraza hili, hasa ukiangalia kwamba Mwenyekiti wa Baraza hili ni Rais. Na sisi wengine Rais wetu anapoanzisha kitu tuna-*interest* ya kujua kile kitu kimekuwa na mafanikio gani kwa wananchi na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kama nilivyosema mwanzo kwamba sitokuwa na mengi ya kusema lakini nilitaka kutia baraka katika hotuba hii kama mfanyakazi mmojawapo ambaye niliitumikia. Niseme tu kwamba naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Zaidi ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kuwa salama mimi na familia yangu. Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa shughuli zake nzuri pamoja na watendaji wa ofisi hii kwa jinsi wanavyoendesha shughuli zao kikamilifu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anieleze ni lini Zanzibar itaweza kusafirisha bidhaa nyingi nchi za nje kwa ajili ya faida ya wananchi wetu wa Zanzibar. Hasa kwa vile kuna bidhaa nyingi hapa Zanzibar kwa sasa bado hatujapata masoko nchi za nje, na nchi yetu ina matatizo mengi ya fedha za kigeni. Hivi sasa wananchi wetu wengi wanajishughulisha na biashara, lakini biashara hizo ni ndogo ndogo ila zina faida nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia nchi yetu ina bidhaa adimu sana ambazo nchi za nje hazipatikani, lakini Serikali bado haijafanya mchanganuo wa kuweza kusafirisha bidhaa hizi ili wananchi wetu wakafaidika hata kuweza kupata fedha za kigeni kwenye nchi. Pia vijana wetu ambao wapo katika mikoa na majimbo yetu wakaweza kupata fedha za kujikimu katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, kuna biashara ambazo hivi sasa ni adimu nchi za nje na zinahitajika sana, lakini bado Mhe. Waziri hajazipatia ufumbuzi wa kuzisafirisha ili tukapata fedha hizo. Mhe. Mwenyekiti, biashara zenyewe ambazo zinapendwa sana nchi za nje hasa Oman ni mabungo, ubuyu, na boribo. Bidhaa hizi nchi za nje

zinahitajika sana. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri hili suala alifikirie, kwa sababu linahitajika sana na hakuna nchi katika dunia ambako kuna mbungo hivi sasa zaidi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, namuasa sana Mhe. Waziri ili aweze kufanya masuala haya angalau kufuata ule wasia wa mfanyabiashara wetu mzuri ambaye anaendelea na biashara na amefaidika sana kwa biashara ndogo ndogo kwenda nje pamoja na hapa Zanzibar.

Kwa hivyo, tumwone kama mfanyabiashara mzuri ambaye ni Said Salim Bakhressa, hata biashara za chapati anaziendeleza na ndio ukaona kwamba ameweza kununua meli kubwa na nyengine ndogo ndogo zinazokwenda kwa kasi ambazo zinatusaidia hapa Zanzibar kwa hivi sasa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri aifuate kampuni hiyo ambayo inazalisha mambo mengi, hasa kwamba haidharau biashara ndogo ndogo. Namuomba Mhe. Waziri japo ni Serikali ahakikishe naye anaweza kupata kampuni zikaweza kuleta maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, pia nichangie ukurasa wa 7 kifungu cha 15 kuhusu usafirishaji na uagiziaji wa bidhaa. Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa nchi yetu inaagiza bidhaa nyingi kutoka nje, na bidhaa zenyewe mara nyingi tunaagiza hasa hizi *used*. Ni biashara nzuri sana zinazosaidia wananchi na hasa wananchi wa chini ambao kipato chao ni kidogo, lakini Mhe. Waziri nilitaka kumpa mawaidha kwamba biashara hizi zinatia zogo jingi nchini, hasa zinapokuja *used* nyingi; nyengine ni mbovu zinakuwa muda mwingi hazipati kununuliwa.

Na biashara hizi kwa muda mwingi hazina maghala wala sehemu maalumu ya kuwekwa ili zikaondoa zogo katika nchi yetu. Sasa nchi yetu imekuwa kama ni jaa la kuleta vyombo vichakavu na hii inapelekea sifa kwamba Zanzibar ni sehemu ya watu maskini, kumbe tuna uwezo wetu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ahakikishe kwamba bidhaa hizi zinapoletwa zina maghala yake maalumu ya kuuzia bidhaa kama hizi. Sio zinawekwa nje kando kando ya barabara ni hatari hata kwa wananchi wetu. Unakosa kugongwa na gari kwamba sehemu nyingi utakuta mafriji yamezagaa katika eneo la barabara. Hii haipendezi na nchi yetu inakuwa kama jaa tofauti na nchi nyengine ambazo tunazitembelea katika Afrika. Namuomba Mhe. Waziri achague sehemu hata katika jimbo langu naweza kumpa sehemu ya Tunguu akajenga sehemu maalumu ya kuweka maghala kama haya, vitu vyote vichakavu vikaenda kuuzwa huko halafu ndio vikaletwa mjini mtu akatumia ndani ya nyumba yake na sio kuwekwa kando kando ya barabara.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitakuwa na mengi sana isipokuwa nichangie ukurasa wa 14 kifungu cha 26 kuhusu viwanda. Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu tuna matatizo makubwa sana ya kuwa na viwanda, lakini namshauri Mhe. Waziri kwa nini ashindwe kuleta viwanda vidogo vidogo hapa nchini hata angalau vya kusindika samaki, tungule, ndimu kama tulivyosindika sisi katika Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kati, Jimbo la Koani kule sehemu ya Uzi.

Mimi jana nilikuwa na Mwenyekiti alikwenda katika kijiji changu kimoja katika Jimbo langu la Koani tukaweza kwenda kufungua kiwanda ambapo kuna kikundi kinaitwa "Hapa Kazi" kimeweza kuvumbua achari ya ndimu ambayo ni ya kisasa kabisa, lakini kwa kuwa hatuna uwezo wa kuweza kupata viwanda vya kileo kwa kweli kampuni yetu haijaweza kujiendeleza.
Kwa hivyo, namshauri Mhe. Waziri atizame Jimbo la Koani kuweza kulipatia viwanda angalau vidogo vidogo vya kuweza kusindika vitu kama hivi tukaweza kujiendeleza hasa wananchi wetu ambao wapo katika hali ya chini.

Mhe. Mwenyekiti, namshauri Mhe. Waziri aendeleze maendeleo mengi sana ambayo tuna shida nayo hasa katika biashara nyingi ambazo hivi sasa zipo nchini kwetu za kuweza kupeleka nchi za nje. Hivi sasa tuna mbao nyingi sana katika mji wetu wa Jozani, ni mbao za kisasa ambazo zinatakiwa sana nchi za nje. Naomba tufungue tawi nchi za nje tuweze kupeleka mbao ambazo zinaweza kuuzwa kwa pesa za kigeni tukafaidika na wananchi wetu wakafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hayo, mimi sitakuwa na mchango mkubwa sana, isipokuwa namkumbusha, ingawa Mhe. Waziri leo ametoa tamko mbele yangu kwamba amesikia wito wangu wa kuweza kununua pilipili hoho kwa bei ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, nawatangazia wananchi wa Zanzibar kwamba Mhe.Waziri ameanza kukubali suala hili, na bajeti yake ikipita amehakikisha kwamba ataweza kununua pilipili hoho na kupeleka nchi za nje.

Kwa hivyo, Jimbo la Koani ninawapa hongera sana waweze kujitayarisha kwa kuweza kukaa mkao wa kula kuweza kulima pilipili hoho. Kwa sababu zina bei nzuri na bei safi na hazina mbwago isipokuwa bei baada ya kupitia bajeti hii Mhe. Waziri atajua atatoa bei ya kuweza kuwasaidia wananchi wetu. (*Makofi*)

Kwa leo sitokuwa na mchango mkubwa sana lakini namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kazi zake anavyozifanya za ukakamavu na kwamba hazina ubadilifu ni za uwazi.

Naomba ahakikishe kwamba anachukua mifano kwa wananchi hata wadogo wadogo, hasa wafanyabiashara, na mfanyabiashara maarufu Said Salim Bakhressa, kwa vile anauza hata ubuyu na sisi tuna uwezo kupeleka nje kwamba nchi nyingi hazina ubuyu. Kwa hivyo, Zanzibar ubuyu ni mwingi na unahitajika sana Oman. (*Makofi*). Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anitolee uamuzi ni lini ataanza kufungua milango wazi kuweza kupeleka biashara hizi ndogo ndogo nchi za nje.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, nitaunga mkono bajeti hii kama Waziri atakapokuja kunihakikishia haya yote niliyoyazungumza mbele yake anayatolea uamuzi. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mussa Ali Hassan. Sasa hivi anayefuatia ni Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadae atakuja Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ni mchangiaji wa mwisho.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii. Hotuba muhimu ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko; Mhe. Nassor Ahmed Mazrui. (*Makofi*)
Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na wasaidizi wake kwa kuandika kitabu kizuri chenye sura nzuri, inayopendeza. Ninampongeza sana lakini pia ninawapongeza kwa utendaji wao mzuri wa kusimamia shughuli hizi ambazo wamepewa na Mhe. Rais kuzifanya.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni miongoni mwa wizara ambazo zipo chini ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, na kwa bahati nzuri mimi ndiye Mwenyekiti wa Kamati hiyo. Kwa hivyo, tumekuwa tukifuatilia sana utendaji wao, shughuli zao kila pale ambapo shughuli za kamati zinapopangwa.
Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wenzetu hawa wamekuwa wakifanya kazi nzuri, kwa bidii na kwa uadilifu pamoja na changamoto mbali mbali ambazo wanapambana nazo, ikiwemo kasoro ya rasilimali fedha. Hili ndio tatizo kubwa ambalo linawakabili wenzetu hawa, lakini tunaamini kwamba pale ambapo watapata nyenzo za kuzifanyia basi wanaweza wakapiga hatua kubwa zaidi ya hapa walipo.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ni muhimu sana pamoja na kwamba zote ni muhimu lakini hii ina umuhimu wa aina yake. Kwa sababu hii ni wizara ambayo imepewa masuala mazima ya kusimamia uchumi, masuala ya biashara, masuala ya viwanda, masuala ya masoko ni masuala ya uchumi wa nchi.

Uchumi ndio kila kitu, kwa hivyo, ni wizara muhimu imepewa majukumu muhimu sana kwa ajili ya maendeleo ya uchumi wa nchi yetu. Hivyo, inapaswa kuangaliwa kwa umakini sana na kupewa kila nyenzo inayostahiki ili waweze kutekeleza majukumu yao hususan masuala haya ya uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza niwapongeze kwa kuweza kudhibiti bei za bidhaa muhimu hususan bidhaa ya mchele, sukari na unga wa ngano. Bidhaa hizi huko nyuma Mhe. Mwenyekiti, zilikuwa hazina utulivu lakini katika miaka hii mitatu ya karibuni, wenzetu kwa kushirikiana na wafanyabiashara wameweza kudhibiti huu mtikisiko wa bidhaa hizi muhimu. Hata wananchi wetu utawakuta kipindi kirefu wamekuwa watulivu sasa, kwa sababu bidhaa hizi ndizo bidhaa hasa wananchi wale wanyonge ambao ndio wengi katika nchi hii, ndizo wanazozitegemea.

Sasa pale zinapokuwa hazisimami, mara bei hii, mara imepanda, kwa hivyo na wananchi wetu nao wanapata mashaka makubwa. Hivyo tunawashukuru sana, tunawapongeza sana kwa kuweza kudhibiti mifumko hii ya bei hususan ya vitu hivi muhimu. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, sisi tupo hapa kwa niaba ya wananchi, sasa ikiwa wananchi wanakuwa wanapata shida, wanahangaika, basi na sisi tunakuwa hatuna raha.

Kwa hivyo, kwa upande mmoja katika miaka mitatu hii, kidogo hali imekuwa ni nzuri na wananchi wetu wanapata kufanya shughuli zao vizuri na bei zile za vyakula muhimu zimetulia. Kwa hivyo, ninampongeza sana Mhe. Waziri, tunamuomba aendelee kushirikiana na wafanyabiashara kuona kwamba bidhaa hizi muhimu za vyakula muhimu bado zinaendelea kuwa katika hali hii ya utulivu.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ni suala la urari wa biashara ambapo Mhe. Waziri hapa kwenye kitabu chake ametueleza jinsi ya hali ya biashara ulimwenguni, lakini pia na hali ya biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Kwa mujibu wa takwimu ambazo mwenyewe Mhe. Waziri amezichukua kutoka kwa Mtakwimu Mkuu wa Serikali, inaonekana kwamba Zanzibar tumekuwa tukisafirisha bidhaa nyingi zaidi zenye thamani zaidi kuliko wenzetu Tanzania Bara kuja Zanzibar, tena kwa kiwango kikubwa.

Sasa tunapata wasiwasi, tunajiuliza hivi ni bidhaa gani ambazo tunasafirisha kwa kiwango kikubwa kiasi hichi mpaka pale wenzetu tunawakiuka; wenzetu wa Tanzania Bara ambao wanaleta bidhaa Zanzibar, ambapo Wazanzibari asilimia kubwa wanategemea bidhaa kutoka Tanzania Bara. Sasa hapa Mhe. Waziri ninadhani kidogo aje atupe ufafanuzi. Ni namna gani Zanzibar inaweza kusafirisha bidhaa nyingi kupeleka Tanzania Bara, kuliko Tanzania Bara kuleta bidhaa Zanzibar.

Pamoja na hayo kama ndivyo ilivyo basi tuwapongeze wafanyabiashara, tuipongeze wizara kwa kuweza kusafirisha bidhaa nyingi kiasi hichi, ambapo unapoweza kusafirisha bidhaa maana yake na tija inapatikana ndani yake, si suala la kusafirisha tu. Unasafirisha, maana yake unasafirisha kwa ajili ya kuuza. Kwa maana hiyo, uchumi unakua, maana yake fedha zinapatikana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri aje atueleze tu ni namna gani wenzetu hawa wameweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa namna hii. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ni mradi huu wa mkakati wa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu la uchumi Zanzibar. Huu ni mradi ambao tumekuwa tukiuzungumza sana. Suala hili tumekuwa tukilizungumza sana na ni eneo ambalo kama serikali itaipa kipaumbele, itatoa umuhimu wa aina yake, linaweza likatutoa hapa tulipo na kutupeleka katika *angle* nyengine ya kiuchumi.

Bado inaonekana ni hadithi ya *"alfu olela olela"*, tunalizungumza lakini utekelezaji wake hasa unaonekana umekuwa ni mzito. Hata ukiangalia fedha zinazoingizwa katika utekelezaji wa mradi huu kwa kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu, kiwango kinachotolewa cha fedha ni kidogo mno ambacho hakiwezi kukidhi au hakiwezi kuwezesha kuwa na *speed* ya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe sana serikali eneo hili ilifanyie kazi ipasavyo. Ni eneo muhimu sana, ni eneo ambalo kila wakati wenzetu tunapowatembelea katika maeneo mbali mbali basi wanatuelekeza katika eneo hili. Wanasema hebu Zanzibar elekeeni katika eneo hili, munaweza mukavuka katika maeneo fulani.
Ninaamini wataalamu wa uchumi ambao wenzetu wameweza kushirikiana nao katika eneo hili, ninadhani hata na wao ushauri wao unaelekeza katika eneo hilo, lakini ni namna gani serikali itatoa kipaumbele katika eneo hili la kuifanya Zanzibar kuwa eneo tengefu.

Mhe. Mwenyekiti, mambo haya ya uchumi ambayo yanaweza kusaidia uchumi ni maeneo ya kuyaangalia sana. Tunayo maeneo ambayo yanaweza kutusaidia lakini inaonekana hatuyapi vipaumbele vinavyostahiki, na badala yake tutakaa hapa tunalaumiana kila siku, bajeti ndogo, Wizara ya Afya imepewa bajeti ndogo, hakuna madawa, hakuna hichi na hichi, lakini yale maeneo ambayo yanaweza kututoa katika maeneo haya hatuyapi kipaumbele kinachostahiki ili kuona kwamba tunanyanyua uchumi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu wakati tukizungumza na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, tuliwahi kuzungumzia juu ya suala hili la kuifanya Zanzibar eneo tengefu. Wenzetu walianza kwa kutafuta wataalamu wawaelekeze namna gani Zanzibar tunaweza tukaingia katika eneo hili.

Kuna changamoto nyingi ambazo wamezieleza, lakini kwa kweli hakuna lisilowezekana, kama kweli tunakusudia, na kwa kuwa yale maeneo ambayo tayari wenzetu wameshatuonesha njia, kama tutayafanyia kazi, ninaamini tunaweza tukafanikiwa. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri azidi kukaza kamba katika eneo hili pamoja na changamoto zilizopo, akaze kamba kuona kwamba Zanzibar baada ya muda mfupi unaokuja basi tunaigeuza kuwa ni eneo tengefu la kiuchumi, ili nchi yetu hii sasa iweze kubadilika kama wenzetu walivyobadilika. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala la maendeleo ya viwanda. Eneo hili nalo tumekuwa tukilizungumzia sana kwa Zanzibar kwamba bado Zanzibar inaonekana tupo nyuma sana katika maendeleo ya viwanda. Tumekuwa tukizungumza sana juu ya Zanzibar kuanzisha viwanda mbali mbali; viwanda vidogo vidogo na vile vya kati, lakini bado *speed* inaonekana ni ndogo pamoja kwamba kuna baadhi ya viwanda vipo, lakini sio vya kutosha na havitoi ajira ile inayostahiki.

Viwanda hivi mbali na kusaidia uchumi lakini viwanda vinaweza kuisaidia nchi kuongeza idadi ya ajira katika nchi. Eneo hili nalo linaonekana kwetu ni tatizo.

Mhe. Waziri nakuomba sana ujitahidi katika eneo hili, kwa sababu tutakapokuwa na viwanda, tunaweza tukawapatia vijana wetu wengi ajira. Juzi Mhe. Mwenyekiti, tulibahatika kidogo na Mhe. Waziri wa Fedha kutembelea Nairobi hapo Kenya kwenda kuangalia viwanda hivi vya mazao ya kilimo. Tukabahatika kwenda katika kiwanda kimoja. Tulikuta katika kiwanda hicho kimoja kimeajiri wafanyakazi wasiopungua elfu nane (8,000). Ni kiwanda kimoja tu, wanaingia kwa *shift*, asubuhi mpaka mchana, mchana wanaingia wengine mpaka asubuhi ni wafanyakazi elfu nane wanafanya kazi katika kiwanda kimoja tu.

Sasa *imagine* kama sisi Zanzibar tunakuwa na viwanda viwili vitatu ambavyo vina uwezo huo, ndio tuone ni kiasi gani vijana wetu wanaweza wakapata ajira, wanaweza kujiajiri kwa kufanya kazi. (*Makofi*)

Kwa hivyo, masuala haya ya viwanda, mbali na uchumi tu, lakini vile vile pia vitasaidia ajira kwa watu wetu. Kama hatukufanya hivyo, malalamiko ya ajira kwa watu wetu yataendelea kuwepo na tutakuwa hatuna vya kuwafanya. Hivyo, tuwahamasishe wawekezaji, waje wawekeze katika maeneo ya viwanda, tupeleke miundombinu katika maeneo ya viwanda. Kwa sababu mwekezaji unapomwita aje awekeze katika maeneo ya viwanda, atakapokuja katika maeneo yale ya viwanda, hakuna barabara, maji, umeme. Hawezi kuja kuwekeza. (*Makofi*)

Kwa hivyo, kwanza yale maeneo ambayo tumeyatenga kwa ajili ya viwanda, tupeleke miundombinu ambayo itawawezesha wenzetu wawekezaji wa nje kuja kuwekeza katika maeneo ya viwanda, kuliko ilivyo sasa.

Maeneo kama ya Micheweni, Fumba, tayari tumeshatenga maeneo kwa ajili ya viwanda lakini hakuna miundombinu itayowezesha wenzetu kuja hapa kuwekeza, wanakuja wanachungulia hatimaye wanaondoka.
Kwa hivyo, mambo haya ni ya pamoja, si ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko peke yake, ni ya serikali nzima. Ni mkakati wa pamoja wa kuona kwamba tunatengeneza ile miundombinu katika maeneo ambayo tumeyatengeneza kwa viwanda ili wenzetu wanapokuja kwa ajili ya kutaka kuwekeza basi waweze kuvutika. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, suala la *Zanzibar Bureau of Standards (ZBS)* ambayo sasa hivi tumeshaianzisha na imeshaanza ku-*develop* lakini bado inaonekana nayo ni changamoto, bado hatujatoa kipaumbele kinachostahiki.
Taasisi hii ambayo ni muhimu sana, tumeianzisha kwa mujibu wa sheria na tumeianzisha tulikuwa tunaihitaji sana na ni muhimu sana, na muhimu katika nyanja mbali mbali. Hata katika sekta ya utalii, bidhaa hizi zenye viwango zinasaidia sana kukuza utalii katika nchi, lakini bado inaonekana *speed* yetu ni ndogo, tena ni ndogo sana.

Pamoja na hali yetu ngumu ya kifedha lakini tunahitaji kuwapa kipaumbele sana hawa wenzetu ili waweze kuanzisha hii pamoja na kuwa na vifaa vya kufanyia kazi.

Kwa hivyo, *speed* ile ambayo tunakwenda nayo, viwango vile vya fedha tunavyowapa kwa ajili ya kuimarisha hizi maabara za kukagua, bado inaonekana ni ndogo na haiendani na umuhimu hasa wa hili jambo lenyewe lilivyo.

Hivyo, mimi niiombe serikali, iipe kipaumbele taasisi hii, iwe na majengo yake, iwe na maabara zake *at least* kwa kuanzia, pamoja na kwamba maelezo humu ya Mhe. Waziri ameeleza vizuri sana, wapi walipo lakini tunapotembelea tunaona *speed* ni ndogo sana na inahitajika *speed* hii iongezwe. Na hawezi kuongeza hivi hivi bila ya kuwapa nyenzo, yaani fedha. Vifaa vya maabara ni vifaa ghali sana. Kwa hivyo, ni lazima tufanye kila linalowezekana kuhakikisha wenzetu wanapata vifaa na majengo ili sasa shughuli hizi za taasisi hii ziweze kufanyika.

Sasa tunajua wanashirikiana na wenzetu wa *Tanzania Bureau of Standards (TBS)*, wanapata mashirikiano makubwa katika baadhi ya maeneo, lakini sasa sio kila wakati tuwe tunategemea wenzetu, kila wakati tunategemea cha ndugu, "*mtegemea cha ndugu hufa maskini*".
Kwa hivyo, tujikongoje tuone na sisi tunakuwa na maabara zetu, tunaangalia viwango vyetu, tunaweka bidhaa zetu, tunaziwekea viwango vinavyostahiki ili sasa tuweze kwenda kwenye *competition* hizi za kimataifa, ambapo sasa hivi watu wanakwenda kwenye viwango zaidi, sio hivi tulivyo sasa hivi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nisichukue muda wako mwingi, nije kwenye Shirika la Biashara la Taifa (*ZSTC*).

Mhe. Mwenyekiti, Shirika la Taifa la Biashara linafanya kazi vizuri sana. Mageuzi yale ambayo wametueleza wenzetu katika mwaka mmoja uliopita yanaendelea vizuri, tunawapongeza sana wamepiga hatua kubwa sana. Kwa hivyo, tunawapongeza, waendelee kusimamia zao la karafuu wakishirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kwa sababu zao hili linahitaji miundombinu ya kutosha, na wenzetu wanasaidia kwa kiasi fulani, kwa hivyo waendelee.

Mhe. Mwenyekiti, zao hili la karafuu ni zao ambalo linatupatia sisi fedha za kigeni. Kwa hivyo, *ZSTC* kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili wanahitajika kulifanyia miundombinu ya uhakika ili kuona uzalishaji unaongezeka zaidi.

Taarifa zilizomo humu kwamba manunuzi yale ambayo waliyapanga na waliyategemea yamepitiliza lengo, lakini pamoja na changamoto za magendo ya karafuu, lakini wameweza kukiuka lengo lile ambalo walikusudia la mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu hawa ambao bado wanaendeleza hii biashara ya magendo ya karafuu sijui dhamira yao ni kitu gani, na kwa sababu sasa hivi hapa bidhaa hizi zinanunuliwa kwa bei nzuri sana. Kilo moja ya karafuu sasa hivi inanunuliwa kwa shilingi 15,000 ni kiwango kizuri sana. Sasa sijui kwa nini wenzetu hawa bado wanaendeleza biashara ya magendo ya karafuu, hatujui dhamira yao, na bado magendo ya karafuu yapo.
Mhe. Mwenyekiti, sisi tunapotembelea kule Pemba kwenye maeneo mbali mbali, wenyewe wananchi wa kule walitwambia kwamba serikali bado haijaweza kudhibiti magendo ya karafuu ipasavyo, na karafuu bado zinasafirishwa zinapelekwa nje ya nchi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri bado una kazi kubwa ya kupambana na magendo ya karafuu, karafuu bado zinapelekwa nje ya nchi, haidhuru ile *speed* imepungua, lakini bado zinasafirishwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunawaomba sana wenzetu ambao wanafanya biashara hii kwamba hii biashara haifai, biashara hii inaua uchumi wa nchi na wala haitusaidii. Fedha hizi ambazo serikali inazipata ni kwa ajili yetu sisi na wananchi wetu pamoja na vizazi vyetu. Tunapozungumzia madawa maana yake ni faida inayotokana na karafuu, tunapozungumzia elimu, umeme, uwanja wa ndege na mambo mengine, hivyo vyote ni faida ya fedha zinazotokana na zao hili la karafuu, sio vyenginevyo.

Sasa wenzetu wanapozichukua karafuu wakazisafirisha nje ya nchi, wanajitazama wao kwa manufaa yao, kwa kweli hatutendi haki, na wananchi wengine basi wawe ni askari. Kwa sababu suala hili haliwezi likakamatwa na maaskari peke yao bila ya kupata mashirikiano na raia wema.

Kwa hivyo, wananchi wote kwa pamoja wanaokaa katika maeneo hayo washirikiane na vikosi vyetu vinavyozuia magendo ya karafuu, ili kuhakikisha kwamba karafuu zinazozalishwa kisiwani Pemba au hata Unguja zinapatikana zote kwa manufaa yetu, maendeleo yetu na vizazi vyetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mimi sina zaidi kama nilivyotangulia kusema kwamba wizara hii ni wizara ambayo inasimamiwa kwenye Kamati yangu ya Fedha, Biashara na Kilimo sina matatizo makubwa, wanafanya kazi vizuri sana. Kwa hivyo, tunawapongeza sana kwa mashirikiano yao ya hali na mali, na mimi ninaiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia juu ya mia.

Niwaombe Waheshimiwa wenzangu waiunge mkono hotuba hii, ili wenzetu hawa waweze kwenda kutufanyia shughuli zetu hizi. Ahsante Mhe. Mwenyekiti nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salmin Awadh Salmin. Anayefuatia sasa Mhe. Hamza Hassan Juma, baadaye atafuata Mhe. Bikame Yussuf Hamad.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa upande wangu nataka nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijaanza kuingia katika mchango wangu, nataka nitoe shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, lakini vile vile watendaji mbali mbali wa serikali, marafiki zangu pamoja na wananchi wa Jimbo langu la Kwamtipura, kwa kuweza kuniunga mkono katika shughuli ya mtoto wangu mpendwa, ambayo niliifanya siku ya Ijumaa. Kwa kweli nawashukuruni sana kwa *support* yenu kubwa.

Vile vile kuna shukrani maalum kwa Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, ambaye katika shughuli ya jioni Mhe. Mohammed Aboud Mohammed ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambaye alimuwakilisha Mhe. Makamu wa Pili wa Rais.

Namshukuru sana pale alipompa nafasi Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Mufti, aliweza kunipigia dua kubwa sana katika ule Msikiti wa pale mtaani ambapo ile shughuli yangu ilifanyika. Kwa kweli ile dua nimeshahudhuria shughuli nyingi, lakini sijawahi kuisikia dua kama ile. Kwa hivyo, ni dua nzito sana, na ile dua ile nisije nikaiharibu, basi naamini leo hotuba hii nitakuwa sina sababu ya kugonga buti hata sehemu moja, kwa sababu naamini dua ile itafanya kazi.

Kwa hivyo, namshukuru sana Mhe. Waziri, kumbe pamoja na kwamba Mhe.Waziri ni mwanasiasa, pia katika masuala haya ya elimu yuko mbali sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa kwa *support* yenu, vile vile kwa ile dua.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika mchango wangu. Mimi nataka niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mhe. Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa wizara hii.

Kwa kweli Mhe. Rais amewapa kazi kubwa na kazi ngumu sana, kwa sababu kwa kazi waliyopewa ni ya kusimamia suala zima la biashara kwa upande wa Zanzibar. Kama tunavyojua kuwa sisi Zanzibar ni visiwa na hatuna ardhi ya kutosha, ambayo labda tunaweza kulima kilimo na kikaweza kuwatosheleza wananchi wetu katika kujitegemea moja kwa moja au tukawa na mashamba makubwa. Kutokana na *geography* tuliyokuwanayo tumezungukwa na bahari, vile vile ardhi yetu ndogo, hivyo inabidi lazima tuelekeze nguvu zetu zote katika kuimarisha biashara hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, katika uimarishaji wa biashara kwa kweli kuna changamoto nyingi sana, ambazo tutamuomba sana Mhe. Waziri ajitahidi sana kupoteza muda wake mwingi kushughulikia kuondoa changamoto hizo za biashara. Kwa sababu Zanzibar kiasili tangu zamani nchi hii ilikuwa inaongoza kwa asilimia kubwa sana kwa biashara. Tunakumbuka wazee wetu hapo zamani, hata mimi Marehemu Babu yangu kule Chaani ilikuwa biashara yake kubwa alikuwa anasafirisha mbata, karafuu na vitu vyengine mbali mbali na pilipili hoho. Kwa hivyo, ni vitu ambavyo vilikuwa na soko kubwa na vilikuwa vinalimwa kwa wingi.

Kwa hivyo, suala la biashara kwa upande wa Zanzibar haliepukiki, ni lazima tuhakikishe kwamba tunaimarisha biashara na tunaondoa vikwazo mbali mbali, ili wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara kwa utulivu. Mhe. Mwenyekiti, nataka nije moja kwa moja katika maeneo mbali mbali.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niwapongeze sana wafanyabiashara mbali mbali hasa wa hapa Zanzibar, wazalendo walioamua kuwekeza biashara au uwekezaji wa aina mbali mbali kwa hapa Zanzibar.
Wawekezaji au wafanyabiashara hawa wanaisaidia sana serikali na wanaisaidia sana nchi yetu, kwa sababu ukiangalia ajira inayotolewa na serikali moja kwa moja basi sitegemei kama tuna wafanyakazi wanaozidi 35,000 lakini ukiangalia Zanzibar watu ambao wameajiriwa naamini hawapungui kwenye laki mbili mpaka laki tatu (200,000- 300,000), kwa hivyo sehemu kubwa ya ajira inatolewa na wafanyabiashara binafsi au na wawekezaji binafsi.

Kwa kweli tunawapongeza sana na tunawaomba wajitahidi, ili kuhakikisha kwamba biashara zao zinakua, ili kuhakikisha kwamba ajira katika nchi yetu inaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kama walivyosema wenzangu kumpongeza mfanyabiashara maarufu kwa hapa Zanzibar au kwa hapa Tanzania ndugu Salim Said Bakhressa. Mimi ni kawaida yangu mtu anapofanya vizuri huwa nampongeza na mtu anapokuwa hafanyi vizuri, simkosoi lakini najaribu kumuelekeza.
Mhe. Mwenyekiti, tunamshukuru sana ndugu Bakhressa kwa kuanzisha hiki kiwanda cha maziwa. Kiwanda hiki kama sikosei kwa sababu mimi sijawahi kwenda, lakini napata tu taarifa mbali mbali, tunaambiwa kiko katika maeneo ya Fumba, na mradi huu kama haujaanza basi wakati wowote unategemewa kuanza.

Kwa hivyo, pale tunategemea Mhe. Mwenyekiti, kutatoa ajira nyingi sana za vijana wetu, hasa wa hapa Zanzibar. Kwa kweli ndugu yetu huyu Bakhressa ataweza kutusaidia sana kupunguza tatizo la ajira kwa upande wa Zanzibar.

Mimi kitu ninachokiomba, kwa sababu uwekezaji wowote unaofanyika katika nchi, basi kwa upande wa serikali *priority* wananchi wataweza kufaidika vipi na mradi ule, ukiacha lile suala zima la kutoa ajira, lakini kama

wawekezaji hasa wenye viwanda, kama watawekeza katika viwanda ambapo mali ghafi yake inapatikana ndani ya nchi, basi Mhe. Mwenyekiti mwekezaji yule anakuwa amefanya kazi mara mbili au ametoa ajira mara mbili. Kuna ajira ile ya *direct* ambayo anaowaajiri anawalipa yeye mishahara, lakini kuna ajira ambayo ni *indirect* kwa wale ambao aidha watatengeneza bidhaa au watazalisha mali ghafi kwa kumuuzia mwenye kiwanda kwa ajili ya kuendesha kile kiwanda. Kwa hivyo, maana yake hapo atakuwa ametengeneza ajira mara mbili kwa wakati mmoja, na sisi Waswahili tunasema, anakuwa amepiga *ndege wawili kwa jiwe moja*.

Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi nilimsikia kama sikosei kulikuwa na sherehe ambayo ilifanyika, nafikiri kwa Mhe. Waziri wa Fedha. Katika bajeti yake ya Wizara ya Fedha naamini pengine hilo anaweza akaligusia. Tulisikia kuna mwekezaji alijitokeza wa Kiwanda cha Sukari, sasa sijui kama ndio yule yule wa hapa Mahonda au kuna mwekezaji mwengine ambaye yeye moja kwa moja ameamua kwenda kuwekeza Kiwanda cha Sukari kule Micheweni Pemba.

Kwa kweli mimi niliposikia taarifa ile nilifarijika sana, kwa sababu Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ilijaribu kutenga maeneo huru ya kiuchumi, na kwa muda mrefu tumekuwa tukizungumza sitaki kutumia lugha ya kwamba tumepiga kelele, kwa muda mwingi tumekuwa tukizungumza kwamba serikali baada ya kuweka maeneo huru basi wayapime, lakini baadaye waweze kuyawekea miundombinu. Kwa sababu haiwezekani mtu anakuja kutoka nje au mzalendo ameandika mradi wake, pengine ameomba fedha benki, mradi wake umekubaliwa na halafu leo lile jukumu la serikali waende wakalifanye wao, kujenga barabara, kusogeza maji na huduma ya umeme.

Mhe. Mwenyekiti, katika msafara tuliokwenda China, nafikiri awamu ya mwanzo Mhe. Mwenyekiti na wewe tulikuwa pamoja na Mhe. Spika, kama sikosei nadhani sijui kama na Mhe. Waziri wa Fedha, lakini na Mwanasheria Mkuu tulikuwa naye. Waziri wa Fedha nadhani alikuwa hayumo, lakini Mwanasheria Mkuu nakumbuka tulikuwa naye.

Mhe. Mwenyekiti, tulipofika kule wenzetu kitu ambacho walitueleza, ni kwamba wenzetu Serikali ya China katika kuondoa umaskini kwa wananchi wao. Kitu cha kwanza walitwambia kuwa kila kitu wanakula, lakini chengine walijaribu kufungua yale maeneo hasa yaliyokuwa kidogo hali yake ya umaskini iko mkubwa katika maeneo yale, basi maeneo yale yametengenezewa mazingira ya kuwekewa maeneo huru ya kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu huko kwa bahati nzuri walitwambia wanafungua maeneo huru kwa ma-*block*. Leo wanafungua mkoa huu ikishaimarika wanatafuta mkoa mwengine. Kwa hivyo, ndio maana leo China utakuta ina bandari nyingi na maeneo mengi na miji mingi, kila unapokwenda unakuta mji ule una viwanda na mambo mengine chungu nzima.

Kwa hivyo, kitu walichokifanya wenzetu, katika maeneo yale kwanza wanasogeza miundombinu kama ya barabara, umeme pamoja na maji, lakini vile vile huwa wanapunguza kodi kwa baadhi ya kodi mbali mbali za serikali ili kuwavutia wafanyabiashara kwenda kuwekeza kwenye yale maeneo yenye mazingira magumu.
Kwa hivyo na hapa Zanzibar tuna maeneo huru ya Micheweni na tuna maeneo huru ya Fumba. Mimi kwa kweli nasikitika sana, nilipomsikia Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, maarufu tunamwita Bhaa, kwa kusema kwamba mwekezaji yule ndugu Salim Said Bakhressa ile barabara ya kwenda katika ule mradi wake amejenga kwa kutumia fedha zake.

Kwa kweli mimi nadhani hiki kitu kidogo mimi sikukipendelea sana, na tunaiomba sana serikali yetu, kwa sababu maeneo yale tumeyapigia kelele sana, na tunashukuru mwekezaji wa mwanzo aliyeanza kujitokeza ndugu Bakhressa, basi tuangalie utaratibu sijui wenzetu Wizara ya Fedha kwa kupitia *ZIPA*, sijui kama wanaweza wakam- *compensate* ili kumpunguzia gharama za ule mradi wake, kwa sababu amefanya kazi ambayo kazi ile ilikuwa ifanywe na serikali. Kujenga barabara mimi najua kilomita moja tu ni fedha nyingi sana.

Mhe. Mwenyekiti, kitu ambacho naomba, kama kuna huyu mwekezaji ambaye kwa taarifa nilizokuwa nazo kama sio sahihi basi Mhe. Waziri anaweza kuja kuniweka sawa, yule anayetaka kuwekeza kiwanda cha sukari kule Micheweni, basi tunaomba basi ile miundombinu, kwa sababu huyu mzalendo yeye katumia pesa zake kajenga hiyo barabara. Sasa kule Micheweni ile miundombinu sasa hivi serikali tukaitengeneze. Tutengeneze ile miundombinu, tumtengenezee barabara na umeme, mimi nakumbuka pale Micheweni upo umeshafika, labda mambo madogo madogo kuwekwa *transformer* ili kipatikane hicho kiwanda ambacho kitaweza kutoa ajira.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa nilizokuwa nazo mwekezaji yule anasema atajaribu kutoa nyenzo au nguvu na kununua miwa kutoka kwa wananchi, ile mali ghafi basi atainunua kutoka kwa wananchi mbali mbali. Hivi ndivyo wenzetu katika maeneo mengine wanavyofanya.

Kwa hivyo, namuomba na huyu mwekezaji wetu mzalendo ndugu Salim Said Bakhressa, kwa kuwa hivi sasa Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa bahati mbaya bajeti yake sikuwahi na mimi kuitia nyama. Tuna wafugaji wengi sana wa ng'ombe kwa kupitia mradi wa *PADEP*, serikali ilitumia fedha nyingi kuwasomesha wananchi, kuhusu ufugaji wa ng'ombe, kuna mitamba mikubwa sana ya ng'ombe ambayo inatoa maziwa, lakini inafika pahala maziwa yanakosa soko.

Kwa hivyo, tunamuomba ndugu yetu huyu ndugu Said Salim Bakhressa katika hiki kiwanda chake basi kipaumbele cha mali ghafi ya hayo maziwa basi anunue kwa hao wananchi.

Ndio kama nilivyosema hapa atakuwa ametoa ajira mara mbili ya *direct* na *indirect*. Ajira ya mwanzo ile ya kuajiri katika kiwanda chake, lakini na ajira ya pili kwa wale wafugaji wetu kuweza kupata ajira ya uhakika kwamba anahakikisha anafuga ng'ombe, anakama maziwa na soko la uhakika linakuwepo. Kwa sababu kile kiwanda chake cha mwanzo pale Maruhubi alianza vizuri, alikuwa ananunua maziwa kwa wafugaji, lakini baadaye nilikuja kuwakuta siku moja pale wamepangana na madeli yao na baiskeli zao, maziwa hayana soko na wakati mwengine

yanarejeshwa, lakini kiwanda hichi naamini kilifanyiwa *feasibility study* na bila ya shaka kitakuwa ni kiwanda kikubwa na kitatoa maziwa mengi na pengine tunaweza tukapata maziwa ya bei nafuu, ili Wazanzibari sasa tukaadhimisha ile Siku ya Kunywa Maziwa, kwa sababu ipo siku hiyo na inaadhimishwa.

Kwa kweli hivi sasa wengi wanakunywa chai ya mkandaa, kwa sababu hakuna maziwa ya uhakika. Kwa mfano, ninavyokumbuka kule kwetu Kwamtipura kulikuwa na vibanda vile vya serikali na vilikuwa vinamilikiwa na wizara yake Mhe. Waziri wa Biashara, kuna maziwa yale ya vipakti sisi tunatumwa na tunakwenda, kwa sababu ilikuwa maziwa kwa foleni, tunapiga foleni pale yanaletwa maziwa tunanunua kwa ajili ya kwenda kunywa chai.

Mhe. Mwenyekiti, naamini hivi sasa ule mtindo Wazanzibari kunywa tena maziwa kwa mara ya pili kwa kiwanda hichi utaweza kutusaidia.

Jambo kubwa hapa ninaloliangalia mimi ni zaidi kuimarika kwa wafugaji wetu wataweza kufuga vizuri na soko la uhakika litakuwa lipo. Kwa kweli hili nimeamua niliseme sana kwa sababu najua wenzetu hawa wawekezaji wanapofanya vizuri tunatakiwa tuwasifu na pia tuwasaidie na ushauri ambao naamini wakiuchukua tunaweza kufanikiwa vizuri.

Suala jengine Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri, kwa bahati nilisafiri na Mwenyekiti wa *Zanzibar Chamber of Commerce* wakati tulipokwenda Seattle Marekani na katika ziara ile kwa bahati nzuri Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tulikuwa naye na kuna mazungumzo mengi tu kule yalifanyika. Nafikiri wale *COSCO* nadhani Mhe. Waziri kuna kazi bila shaka anaifanya kupitia kwao wale, ili soko la karafuu, sasa hiyo sitaki kumueleza kwa sababu yeye mwenyewe alifika pahala na aka-*negotiate* kule na ninaamini wamefikia hatua nzuri au watakwenda vizuri baadaye.

Kikubwa lakini nilijaribu kuzungumza na Mwenyekiti wa *Zanzibar Chamber of Commerce*, baada ya kufika kule Marekani nikamwambia Mwenyekiti na tukawaona wenzetu wa *Chamber of Commerce* kule kwa kweli wako *very active*, yaani ni watu ambao wamejipanga, wanayo mikutano yao ya kila mwaka, wanapanga masuala ya biashara tena kama wale *Chamber of Commerce* ya *Africa*, wao wanaimarisha au wameweka kiungo baina ya wafanyabiashara wa Marekani wenye asili ya Kiafrika na nchi zao zile. Kwa mfano, wenzetu Ethiopia hivi sasa wako mbele sana katika suala zima la biashara.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, umebakisha dakika tatu.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, watu hakuna na nilikuomba sawa.

Mhe. Mwenyekiti, katika ile *chamber* naomba sana wafanyabiashara wengi wakubwa ninaowajua mimi hapa Zanzibar hawamo. Mhe. Waziri naomba aifanyie kazi pia ile *Zanzibar Chamber of Commerce* naweza kusema iko *weak*.

Nadhani ni vyema Mhe. Waziri atumie *instruments* zake pamoja na maarifa yake kwa sababu na yeye Mhe. Waziri aliwahi kuwa Mwenyekiti wa *Zanzibar Chamber of Commerce*, ni vizuri akaifufua hii *chamber* awashawishi, na kama wana matatizo yao wafanyabiashara wa Zanzibar akae nao na awashawishi waache yale mambo ya kizamani.

Kwa kweli hivi sasa biashara kwa mfano wenzetu Marekani wametaka wao kufanya *Joint Venture* na wafanyabiashara wa Zanzibar, lakini sitaki kuwadharau na katika wafanyabiashara tuliokwenda nao sijui labda Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko anaweza akasaini *contact* za *Joint Venture* na wafanyabiashara wale wa Marekani, kwa sababu tuko *weak.*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na hili afanye kwenye malengo yake kabla hatujamaliza awamu hii uwakutanishe wafanyabiashara wakubwa wa Zanzibar ambao hawamo katika *Zanzibar Chamber of Commerce*, yaani wafanyabiashara wanafanya biashara za kimataifa ambazo ni kubwa tu, lakini hawamo kwenye *Zanzibar Chamber of Commerce*. Nadhani hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kama utakumbuka wakati tulipokwenda *Ras-el-Khaimah* wao pia wamesema katika maeneo yao huru, wamesema wanataka *Joint Venture* na mfanyabiashara yeyote waingie nao *Joint Venture*. Mhe. Mwenyekiti, nikizungumza sana nitaonekana ninawadharau wafanyabiashara wetu, kwa sababu wewe mwenyewe tulikwenda na uliona.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba aingilie kati *Zanzibar Chamber of Commerce*, na kama kuna matatizo yoyote yaondoke, ili tuimarishe *Zanzibar Chamber of Commerce*, kwa sababu hatuwezi tukajisifu kwamba Zanzibar ni nchi ya biashara na wale wafanyabiashara wakubwa katika ile *Zanzibar Chamber of Commerce* hawamo.

Mhe. Mwenyekiti, tulimuona Mhe. Rais Barack Obama wakati alipokuja Dar-es-Salaam amefuatana na wafanyabiashara wale wakubwa hasa, sasa hapa wale wafanyabiashara wetu wakubwa hawamo katika hiyo *Zanzibar Chamber of Commerce*, na hilo ni tatizo.

Sasa hata Mhe. Rais wa Zanzibar anapokwenda nje ya nchi na kusema kwamba mimi nataka nifuatane na wale wafanyabiashara wakubwa wa Zanzibar na wao hawamo kwenye hii *Zanzibar Chamber of Commerce*. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri suala hili atusaidie, tena hivi munaposafiri mukatuchukua ndio faida yake, kwa sababu tumeona udhaifu wetu tulipokwenda na tunaporudi tunakuja kuishauri serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba dakika tano za ziada, kwa sababu wewe Mhe. Mwenyekiti ni mwanamke na tumekuchagua kwa makusudi kwani una huruma. Vile vile wizara hii inatakiwa itiwe nyama, ili nchi yetu iweze kunyanyuka kiuchumi. Sasa haya yaliyobakia nitasema kwa haraka haraka na nilikuwa nikifanya mbwembwe kwa sababu najua nimeomba muda wa kutosha.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nakupa dakika tatu za kumalizia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Suala jengine namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuna viwanda hapa, na hivi sasa ninashukuru kwamba Wazanzibari wamehamasika kuwekeza katika viwanda tofauti, na wakati wa zamani walikuwa ni wafanyabiashara wanakwenda kununua vilivyotengenezwa, yaani walikuwa kama madalali, lakini hivi sasa wameamua kuwekeza hapa, wanatoa ajira pamoja na kulipa kodi mbali mbali.

Kwa hiyo, ninaomba kama hatuna sheria ya kulinda viwanda vya ndani, Mhe.Waziri naomba tulete sheria ya kulinda viwanda. Mhe. Mwenyekiti, kwa mfano, hapa kuna viwanda vya maji hapa na leo kuna maji yanaingia yanatoka mpaka Dubai wakati hapa tunavyo viwanda vya maji, ambapo viwanda vile vingeliweza kukua na kutoa ajira nyingi.

Sasa tukiruhusu tu kweli *Zanzibar ni njema atakaye aje,* na kila biashara lete, hivi viwanda vyetu vitakufa na juzi tu tumesikia *Coca Cola* kimeshafungwa na hawa viwanda vya maji wataamua kufunga na waje walete maji kwa makontena, nafikiri vijana wetu itakuwa tunawapunguzia ajira.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu usafirishaji na mwenzangu Mhe. Salmin Awadh Salmin ameeleza na ninashukuru kwamba hivi sasa karafuu imerudi katika ile hadhi yake, serikali inasafirisha sana karafuu, pia na mazao ya mwani, lakini bado Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri na ninajua

kwamba anafanya jitihada katika zao la mwani ameshakwenda mpaka Malaysia na sehemu nyengine kwa ajili ya kutafuta soko la mwani.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati anapokwenda nje au anapokaa na hawa wafanyabiashara wa Zanzibar awashawishi namna gani wanaweza wakawekeza kwenye viwanda vya *processing* ya mwani, ili kuweza kuinua soko la mwani pamoja na kuweka bei nzuri ya mwani.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, hivi juzi wakati tulipokuwa tukizungumzia mitumba, Baraza hili lina nguvu kubwa na nguvu ya Baraza inaweza ikamuua mtu na sisi tunaweza kupitisha sheria na kuna watu wakafa huko mitaani.

Sasa juzi Mhe. Mwenyekiti, tulipokuwa tukizungumzia mitumba hasa nguo za ndani, walikuja na kulalamika wakasema Waheshimiwa munataka kutuua, kuna mmoja akaniambia mimi nimefeli *Form II* na nimejisomesha kwa biashara hii nimefika *Form IV*, Chuoni na mpaka hivi sasa ninasoma *Open University* kwa biashara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikamwambia sikiliza nyinyi munataka kutuletea matatizo ya maradhi ya ngozi, akaniambia kwamba Mheshimiwa sio kama mitumba yote imevaliwa, akaniambia kuna mitumba mingine huko nje kwa sababu wao ndio wanaofungua, anasema mitumba mingine inakuja iko katika *quality* nzuri, tena mitumba ni bidhaa ambazo zimeshakaa sana pale dukani (*old stock*). Kwa hiyo, mukiizuia moja kwa moja ina maana hata ile biashara ya kule ambayo kuna bidhaa nyengine zinatoka moja kwa moja dukani...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, malizia na wenzio wapate nafasi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri wangu, maana yake naamini pengine baadaye Mhe. Waziri akaja na sera. Sasa katika hiyo sera, kwa sababu hivi sasa serikali sera wanafanya peke yao kwa mujibu wa taratibu tulizozipitisha.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri watakapokuja kuifanya hiyo sera ya kudhibiti bidhaa hizi, japo kidogo waje watufanyie semina, ili tuweze kutoa ushauri, kwamba kuwe na hii *ZBS* kama imeshapatiwa vifaa waweze kukagua na kuweka *conditions* maalum kwa ajili ya bidhaa zile, lakini tukisema tunaua moja kwa moja Wazanzibari wengi itakuwa biashara zao itakuwa zimekufa na wataanza kurudi tena mitaani, na Waheshimiwa Wajumbe mnapiga kelele inapokuwa foleni majumbani kwenu, hivyo hapa tutaua soko la ajira.

Baada ya hayo machache Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ninayo mengi ya kusema na mengine nitayabakisha siku ya Mhe. Waziri wa Fedha, na nitamuomba Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko awepo kwa ajili ya kumsaidia Mhe. Waziri wa Fedha, kwa sababu biashara inaendana na fedha.

Kwa hivyo, kuna mambo mengi tutakuja kushauri na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa yale yatakayomuhusu katika Wizara ya Fedha aje atusaidie majawabu.

Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa hotuba hii kama nilivyosema kwamba sina maneno ninaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kunipa fursa hii na mimi nikatoa mchango wangu mdogo sana na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad ajitayarishe, mimi sizishi dakika hizi.

Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia tukakutana hapa jioni hii tukiwa na hali nzuri na afya njema.

Vile vile nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Naibu Waziri pamoja na watendaji wao wote kwa jumla, kwa mashirikiano yao katika kutekeleza wajibu wao. Kwa kweli ni mashirikiano mazuri ambayo wanayo kwa ajili ya kufanikisha kitabu hichi kina manufaa ndani yake.

Mhe. Mwenyekiti, pia niipongeze Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambapo na mimi ni Mjumbe mstaafu, chini ya Mwenyekiti wao Mhe. Salmin Awadh Salmin Mnadhimu wa Chama cha Mapinduzi, nadhani Kamati hii iko makini sana. Pia Mhe. Jaku Hashim Ayoub ambaye ametuwasilishia leo, nataka nimpongeze na yeye kwa umahiri wake wa kuwasilisha ripoti ile ya maoni ya Kamati. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba sitokuwa na mchango mkubwa, isipokuwa suala langu la kwanza ni kwamba Mhe. Hamza Hassan Juma amenifilisi sana, kwa sababu yeye alisema anafarajika sana kwenye

taarifa hii ya mwekezaji huyu wa Kiwanda hichi cha Sukari kilichopo hapa Unguja, sasa yeye kama anafarajika mara mia 100 na mimi zaidi ya mara 100. *(Makofi)*

Kwa kweli nataka niishauri tu serikali kwa nia hii njema ambayo tayari ni dalili tosha za mafanikio katika maeneo yale yaliyotengwa kwa kipindi chote hicho kilichopita, na leo hii tukasikia faraja kama hii ni matumaini mazuri.

Kwa hiyo, ninaiomba serikali pamoja na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati waende wakaangalie yale maeneo kama alivyosema Mhe. Hamza Hassan Juma, waanze kuyafanyia ukarabati kama kuna matengenezo, ili wamuhamasishe mwekezaji huyu na nia yake njema, atakapofika pale aweze kuwaita wengine kwenda katika maeneo yale kwa ajili ya kuwekeza. Kwa kweli huo ni ushauri wangu kupitia taarifa hii, na tunaiomba serikali ifuatilie kwa ukaribu sana.

Suala jengine pia alilizungumza Mhe. Raya Suleiman Hamad, kwamba kuna Shirika la *ZSTC* kituo chao kilichopo Dar-es-Salaam siku nyingi tunazungumza katika kadhia wanayoipata ofisi ile iliopo pale Dar-es-Salaam kutokana na lile jengo la kukodi siku nyingi.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho anieleze kwa sababu kwenye kitabu sijaliona na suala hili limefikia wapi, kwa sababu ninakumbuka mpaka siku moja niliuliza swali hapa Barazani na niliambiwa kuna marekebisho au vipi.

Hivyo ni vyema aje atueleze kama jengo lile wanaendelea kukodi vile vile, kwa sababu wenyewe walisema ni gharama kubwa na wanafanya kazi kubwa, fedha wanapata, lakini hatimaye fedha zote zinakwenda kwenye ulipaji wa jengo lile, na tuliiomba serikali siku nyingi. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba wakati atakapokuja hapa anieleze ni hatima gani iliyofikia.

Jambo jengine ambalo sijalisikia hapa likizungumzwa kuhusu *ZSTC* nimesikia wanayo Ofisi yao Dubai na pia nimesikia kwamba kuna Kamati ya Fedha ya kipindi cha Awamu ya Sita walikwenda kutembelea huko katika afisi hiyo, lakini tangu siku niliyofika hapa mimi sijasikia mazungumzo ya afisi hii, nia na madhumuni, kazi zake katika eneo hilo huko la Dubai. Kwa hivyo, Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja kufanya majumuisho, aje anipe ufafanuzi ili na mimi nipate kuelewa.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 7 *paragraph* ya 18 kuhusu biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara katika kitabu chake ametueleza kwamba kuna upungufu wa asilimia kadhaa kwenye maelezo yake. Sasa naomba Mhe. Waziri aje anieleze kwamba ni sababu zipi ambazo zilizopelekea kupatikana kwa upungufu huo.
Kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza tena wizara katika kazi zao kubwa wanazozifanya na za mafanikio.
Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 13 *paragraph* ya 25 kuhusu mazingira ya kufanya biashara na Mhe. Waziri ametueleza hapa na ninaomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Ukurasa wa 13 *paragraph* ya 25 inaeleza hivi:-

> "... ufanyaji wa Biashara ambapo Zanzibar ilishika nafasi ya 155 kati ya nchi 183 ilizolinganishwa nazo. Serikali tayari imeanza kuchukua hatua za kutekeleza mapendekezo ya utafiti huo. Hatua hizo ni pamoja na kuandaa Sheria mpya ya Biashara, Sheria ya Usimamizi wa Utoaji Leseni ...."

Mhe. Mwenyekiti, niwapongeze kwa kuchukua hatua hizi, nafikiri katika mazingira haya ya kufanya biashara ni moja ya kutaka kuwepo na mafanikio mazuri ndio wakaweza kutueleza mafanikio yao hapa katika kuona kuwa Zanzibar ni nchi ya 155.
Suala jengine katika hali ya viwanda ukurasa wa 14 *paragraph* ya 26 pia Mhe. Waziri ametueleza na ninaomba kunukuu Mhe. Mwenyekiti.

Ukurasa wa 14 *paragraph* ya 26 inaeleza hivi:-

> "... kwa kipindi kirefu muitikio wa uwekezaji na wawekezaji wazalendo ulikuwa mdogo. Katika siku za karibuni hata hivyo, dalili za kukua kwa sekta hiyo zinazojitokeza kutokana na mambo yafuatayo:-

(a) Kwa kuanzishwa kwa viwanda mbali mbali... Nashukuru hilo Mhe. Mwenyekiti.
(b) Kuanza uzalishaji wa Kiwanda cha Sukari Mahonda ... Tayari nimeshalieleza".

Mhe. Waziri ameeleza kwamba wanafanya mpango wa kuanzishwa viwanda vya usarifu wa zao la mwani na karafuu. Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mhe. Waziri, kwa sababu kiwanda cha karafuu tayari tunacho ambacho pengine kinafanya makonyo na mambo mengine. Sasa kama wizara itakuwa na mpango huo wa kutafuta kiwanda cha usarifu wa mwani, nadhani ni jambo zuri tena ni jema. Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri na tunamuomba jitihada hii aiendeleze.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, kuhusu viwanda bado viwanda vipo pamoja na kwamba ni dhaifu, lakini tatizo vinahitaji viwezeshwe, ili viweze kuua na vitambulikane na wataweza kuuza bidhaa zao nje. Mhe. Mwenyekiti, nataka nimueleze Mhe. Waziri kama hajatembelea kwenye hivi vikosi nadhani ni JKU au KVZ, mbona wao utaalamu mzuri wa kutengeneza viatu, wanatengeneza viatu vya kwao wao kama vya kijeshi lakini mpaka tulifika pahali tukaona pale pana peya mbili tatu ambazo kuwa zinatengenezwa viatu vya watoto wadogo, kwa kweli wale watu wana utaalamu wa kutosha, utaalamu mzuri lakini kwa kusema kweli suala la upatikanaji wa mali ghafi ni tatizo, lakini kama Serikali itawawezesha kikosi kile basi nadhani inaweza kuwa ni kiwanda kizuri. Na kama watapatiwa wataalamu, kwa sababu tatizo lao pia wataalamu hawana, lakini na hivyo vifaa vyenyewe ni hafifu wanatumia ushonaji viatu vile kwa mikono, lakini kwa kweli ni watengenezaji wazuri wa viatu na namuomba Mhe. Waziri kupitia kikosi kile basi kama anawajua sawa, mawazo na nia atakuwa anayo yeye awaendeleze vipi, lakini kama hakijui hicho kiwanda basi afanye jitihada ya kukitafuta nitakupeleka, afanye jitihada ya kukitafuta, au kama unavyosema nikupeleke mimi nitakupeleka, ni Kamati yangu, twende tukawaangalie ili uweze kuwafanyia maarifa ya kuwatafutia mikopo au Serikali kwa ujumla iweze kuwawezesha ili kile kiwanda wakiendeleze, nahakikisha wale wakiendelezwa basi soko litapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sitaki nichukue muda wako mwingi, naunga mkono hotuba hii ya Waziri na ripoti ya Kamati nayo pia naiunga mkono kwa asilimia mia, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti awali ya yote haya nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia jioni hii kuwepo hapa katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi.

Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko kwa uwasilishaji wake mzuri katika hotuba yake hii.

Aidha nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo anatujibu masuala yetu katika Baraza lako kwa ufasaha na umakini wa hali ya juu kabisa. Niseme kwamba kwa ujumla nawapongeza watendaji wote wa Wizara hii ya Biashara kwa kazi zao wanazozifanya kwa kumsaidia Waziri majukumu yake. Mwanzo wa mchango wangu baada ya utangulizi huo nakwenda moja kwa moja katika zao la karafuu. Mhe. Mwenyekiti, zao la karafuu ni miongoni mwa mazao ambayo yanapatisha pato la Taifa katika nchi yetu ya Zanzibar. Zao hili ni muhimu kwa Zanzibar, na kama Serikali ambayo imepanga kuliwezesha hili zao liwe imara, basi hili nasema kwamba ni jambo zuri na lenye nia safi kabisa, itekelezwe ili zao hili liweze kuleta tija kwa Taifa na wananchi mmoja mmoja kwa ajili ya kujipatia maslahi yao ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitakuwa na mambo mawili ambayo naomba nimuulize Mhe. Waziri jinsi gani alivyojipanga katika wale wananchi ambao Serikali ilitangaza waoteshe miche ya mikarafuu kwa ajili ya Serikali kuinunua. Wananchi hawa wapo na mikarafuu, miche wanayo lakini bado Serikali hawajainunua miche hii na watu hawa ni wanyonge kiasi ambacho wameuza baadhi ya mali zao kwa ajili ya kuotesha miche hii ya mikarafuu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nimuulize Mhe. Waziri, lakini kabla ya suala langu nitoe maelezo. Tukitaja neno karafuu kuna wachumaji wa karafuu. Mhe. Mwenyekiti wachumaji wa karafuu ni watu, watu hawa kwa nia safi kabisa wanachuma karafuu, na uchumaji wa karafuu ni kazi ngumu kwa sababu ni kazi ya kupanda huo mkarafuu wenyewe wanapata madonda kwa sababu ya kuchorwa na majiti, na matokeo yake wengine wanaanguka wanapoteza maisha, wanapoteza viungo vyao, wanapoteza nguvu kwa ajili ya kuokoa zao la Taifa la Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri watu hawa ambao wanaanguka mikarafuu ni walemavu, na wengine bado wapo kitandani hivi sasa kwa zao hili hili lililopita mwaka jana, mwaka juzi na mwaka juzi, unawaangalia vipi, na Shirika lako lina mkakati gani endelevu kwa ajili ya kuwasaidia wahanga wa mikarafuu? Wahanga wa mikarafuu ni wengi, wanapata tabu wanapoteza roho, wanapoteza viungo, sasa naomba Shirika hili au Wizara hii ya Biashara suala

hili kwa kweli ilipe kipaumbele kwa watu hawa ambao wanapata tabu, wanapata misukosuko katika uchumaji wa karafuu.
Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 20 *paragraph* ya 36 hii (a) Inasema kufanya tathmini ya matumizi sahihi ya teknolojia katika uzalishaji na ukaushaji wa chunvi kwenye kiwanda cha chumvi cha Wawi Pemba.

Mhe. Mwenyekiti hii ni nia njema kabisa lakini nashukuru pia kuwa hii chumvi imetajwa katika kitabu hiki cha Biashara kwa wakati ambao tokea kipindi kilichopita hivi, cha bajeti hizi tulikuwa tukiangalia chumvi iko wapi, lakini leo tunaiangalia imo humu. Nimuombe Mhe. Waziri kiwanda hichi wakiwezeshe, kwa sababu kuna watu wengi katika kisiwa cha Pemba wanazalisha chumvi, wana ukulima wa chumvi, wazalishaji ambao wanahitaji taaluma wanahitaji wawezeshwe, nahofia kwamba inawezekana kiwanda hichi kama hakikuwezeshwa tukalishwa chumvi ambayo haina madini joto na mwisho wake ni kuambulia maradhi.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri suala hili alipe nafasi kubwa na pia baada ya kwishalipa nafasi kubwa wakulima hawa wa mazao haya ya chumvi wawezeshwe na watafutiwe masoko, iwe hakuna sababu ya kisiwa hichi cha Unguja na Pemba kuagizishia chumvi kutoka nchi za nje wakati ambao wananchi wetu wameitikia wito wa uzalishaji wa chumvi, na chumvi inazalishwa, kwa hivyo ni wajibu wa Serikali hivi sasa kuwawezesha wakulima wa chumvi ili chumvi yao kuwa na ubora ikauzwa ndani na nje ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya hapo niende katika kitabu hichi ukurasa wa 23 unaozungumzia utekelezaji wa mpango wa mageuzi ya *ZSTC* niende 44(c) kuratibu shughuli za kikosi kazi cha karafuu ili kupambana na magendo ya karafauu.

Mhe. Mwenyekiti kwa kweli hili ni suala zuri kwa kuwa magendo ya karafuu katika kipindi cha miaka iliyopita yalikuwa ni makubwa na karafuu nyingi zilikuwa zinasafirishwa kwa magendo kuliko kuuzwa katika nchi yetu, lakini kuanzia mwaka juzi, mwaka jana na mwaka huu kutokana na ongezeko la bei ya karafuu watu wengi wamepunguza kabisa kabisa upelekaji wa karafuu kimagendo nje ya nchi yetu.

Lakini kikosi kazi hichi nahisi kwamba hofu yangu ni kuwa kikosi hichi kinaweza kikawa na watu wengi sana au watendaji wengi sana, kwa sababu katika kipindi kilichopita nilisikia tu kwamba wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Polisi wa Mikoa, Wakuu wa Polisi wa Wilaya, masheha, KMKM na vikosi vyote vinaunda *task force* hii, nahofia *task force* hii kuwa kubwa na ikatumia gharama kubwa ya fedha kuliko lile lengo ambalo limekusudiwa. Kwa kuwa kuna kikosi maalum cha kuzuia magendo; KMKM, nafikiri kingewezeshwa kikosi hichi kikaboreshwa vizuri kikosi hichi ili kikaweza kupambana na masuala haya ya magendo ya karafuu, kuliko kuandaa *task force* kubwa ambayo inaweza kupoteza pesa nyingi zaidi kuliko lile lengo ambalo limekusudiwa la kudhibiti mazao haya ya karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende kidogo katika kitabu cha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kitabu hichi kinazungumzia ripoti ya Mkaguzi ya Ukaguzi wa Hesabu kwa Mawizara, Mashirika na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2011/2012.

Hapa nitakuwa na mambo mawili ambayo nataka nizungumzie mbali na kunukuu nukuu za kitabu hichi. Ukurasa wa 195 Shirika la Biashara la Taifa linazungumza hivi.

" Nyumba ya Sinza. Shirika la biashara la Taifa linamiliki nyumba No. 82 katika eneo la Sinza ambayo imekodishwa kwa ndugu Ramadhan Mwita kwa kodi ya Shilingi laki tano kwa mwezi ni sawa na shilingi milioni sita kwa mwaka, ukaguzi uliofanywa umebaini hali ya nyumba hiyo hairidhishi kutokana na kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu".

Mhe. Mwenyekiti hapa hofu yangu ni kwamba mambo yetu mengi kwa kweli tunayafanya kinyume na matarajio au kinyume na lengo, nyumba hii inakodishwa kwa pesa si kidogo, lakini kwa nini nyumba hii ifikie hatua ya kuwa haifanyiwi ukarabati. Mhe. Waziri kulikoni nyumba hii ni nyumba ya shirika inakodishwa, lakini Mdhibiti kafika na karipoti kwamba nyumba hii haifanyiwi ukarabati kwa muda mrefu uliopita, kwa hivyo hapa nahitaji maelezo kutokana na tatizo hili.

Jengine alilizungumza hapa Mhe. Bikame nataka mimi nilizungumze katika kitabu hiki cha Mdhibiti tawi la Dar es Salaam.

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Biashara la Taifa tawi la Dar es Salaam halionekani kuwa na tija kwa shirika, kuendelea kuwepo kwa Tawi hilo ni kuongeza gharama za uendeshaji ambapo kuna

wafanyakazi wawili wanaoendesha shughuli za tawi hilo ambapo hulazimika kulipa gharama ya kukodi nyumba kwa ajili ya ofisi na ghala kwa shilingi 4,131,298/= kwa mwezi ambapo ni sawa na shilingi 49,575,576/= kwa mwaka.

Mhe. Mwenyekiti hili ni tatizo kwa kuwa Mheshimiwa Bikame amelitaja na mimi naliongezea kulitilia nyama, tunaomba maelezo ya kina kuhusiana na Tawi hili la *ZSTC* lililopo Dar es Salaam.

Mwisho kwa kuwa kuna Mhe. Subeit alitajwa hapa na yeye nisimnyime haki hii vile vile ningechangia maneno yangu ya mwisho kuhusiana na kwamba Zanzibar ni visiwa vya matunda, kwa kuwa Zanzibar ni kisiwa au visiwa ambavyo vina matunda mengi, Mhe. Waziri umefika wakati sasa Wazanzibari kutafutiwa viwanda vya kuyahifadhi matunda haya, matunda tunayo mengi; embe, machungwa, ndimu nk. iweje leo matunda haya yawe yanaozeana tu? Nakuomba Mhe. Waziri kwa makusudi Serikali ijipange kwa makusudi kuwe na mpango maalumu wa kuweka kiwanda cha Serikali mbali wawekezaji, kiwanda cha Serikali ili kuyahifadhi matunda haya.

Unakwenda dukani unanunua chupa ya *juice* ya embe imetengenezwa nje ya hapa, kwa nini Serikali ya Zanzibar isiweke kiwanda kwa ajili ya kuyasanifu matunda. Tuna matunda mengi, tuna uwezo wa kuyasanifu matunda tukatumia *juice* za matunda ndani na nje ya nchi.

Wizara yako ijipange kwa kushauriana na Serikali, kwa kushauriana na hao wawekezaji lakini ni vyema matunda yetu yasiozeane, bali tuyatumie na kuingiza fedha za kigeni,na vijana wetu wengi kupata ajira katika visiwa hivi vya Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti kwa heshima na taadhima nakushukuru na nitaunga mkono hotuba hii baada ya kupata maelezo ya kina katika masuala ambayo nimeyauliza. Ahsante sana.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hapa tuna dakika tisa zilizobakia nataka nimuulize Mhe. Subeit kama zitamtosha.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, naomba kama kuna uwezekano mimi naomba unipe nichangie kesho kwa sababu naona dakika zilizopo ni kidogo sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nichukue fursa hii kuwashukuru sana kwa michango yenu pamoja na utulivu. Sasa naakhirisha kikao hadi kesho tarehe 24/06/2014 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:36 Usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 24/6/2014 Saa 3:00 Asubuhi)